
# 1. Uislamu na Waislamu

Magaidi wa Kiislamu, wahanga wa Kiislamu wa kujilipua mabomu, mauaji ya wapinzani wa siasa, vitisho vya kuuawa dhidi ya Wakristo huko katika nchi za Arabuni – hizi ndizo habari zinazomiminika nyumbani mwetu kwa njia ya radio, televisheni na magazeti. Woga, hasira na chuki ya waziwazi dhidi ya mwingiaji huyu asiyetakiwa yumo katika akili za watu wengi, haidhuru iwe kwa Wakristo au kwa watu wa kawaida waliostaarabika kidogo.



Isitoshe kuna mambo mengi yasiyojulikana kuhusu asili halisi ya dini hii. Wachungaji wengi na hata Wakristo wa kawaida wamepata wasiwasi kubwa juu ya wafuasi na jamii za Wakristo kusilimishwa, mara nyingi, kama ilivyowahi kutokea, ghafla bila mpangilio.

Siyo ajabu basi, kwamba watu wengi wamepigwa mshangao kuhusu Uislamu kuwa "tishio kubwa kwa Kanisa hivi leo", au wengine huamini na kufundisha kuwa "Waislamu wameshikwa na balaa na hawawezi kuponywa." Hata wachache wamejaribu kuwashuhudia hawa "Waislamu": au "wafuasi" wa Muhammad, vyovyote vile watakavyoitwa kimakosa, lakini walichovuna ni upinzani mkali. Badala ya wao "kuwaongoa Waislamu" walijikuta wanashambuliwa na kugeuzwa kuwa ndio "wanaostahili kuhubiriwa", tayari wamekwisha kuwekwa sawa, wanapigwa mabomu ya hoja dhidi ya Ukristo, au wanabembelezwa kwa kila aina ya ushawishi kukumbatia Uislamu.

Kama Kristo ndiye Bwana wako utapenda kumsikia na kutii amri zake, na kufuata mfano wake. Maneno na amri zake, na kufuata mfano wake. Maneno ya Yesu aliyowaambia wanafunzi wake bado yana maana hata hivi leo:

*"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili. Na hao nao* ***imenipasa*** *kuwaleta." (Yohana 10: 16)*

Naye Mtume Paulo anathibitisha kwamba

*"Mungu Mwokozi wetu, anataka watu* ***wote*** *waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli." (1Timotheo 2:4)*

Je, ni jambo ambalo haliwezekani kwa wafuasi wa Kristo kushirikisha ujumbe wa msamaha, furaha na ukweli? Hapana, *"maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na akili timamu, na moyo wa kiasi." (2 Timotheo 1: 7)*

Kwa hivyo tunaweza kujifunza nini kuhusu dini hii? Kwa lugha ya Kiarabu, neno *"Uislamu"* maana yake ni "kunyenyekea", na *"Mwislamu"* maana yake

ni “mtu aliyenyekea”. Msingi wa kuielewa imani ya Kiislamu inatokana na maneno hayo kama yalivyoandikwa katika Surah19:93: *“Hakuna yeyote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa mwenyezi Mungu mwing wa rehema hali ya kuwa ni mtumwa wake.”*

## *1.1 Uislamu una umri gani?*

Tunapoangalia mwaka 2002 katika kalenda ya Kiislamu huonyesha kwamba ni mwaka 1424 BH (maana ya BH ni baada ya Hijra), na Hijra ni wakati ambapo Muhammad, mwanzilishi wa Uislamu, alipokuwa matatani kwenye mji wake alikozaliwa Maka, na kutorokea mji mwingine (Medina). Kukimbia kwake huku ndiko kulikokuwa mwanzo wa Uislamu.

***Je, Uislamu umekuwako kwa muda mrefu kuliko imani ya Kikristo?***

La! Uislamu ni changa kwa Ukristo kwa karibu miaka 600. Hiyo ndiyo sababu Waislamu nao wanaweza kusema wao pia humwamini Mungu (Allah), Nuhu, Abraham, Musa, Daudi na Suleman, Yona na manabii wengine wa Biblia, pamoja na Yesu.
Lakini, kwa nini Uislamu ulianzisha dini nyingine mpya?Kwa nini Waislamu hawaridhiki tu kuamini manabii hawa wachache pamoja na Yesu?
Ni kwa sababu kitabu chao kinawaambia vinginevyo, jambo linalowafanya wajione bora zaidi kuliko watu wengine wote.

> *Surah 61:9 “Yeye ndiye aliyemtuma Mtume wake (Nabii Mohammed) kwa uwongofu na kwa Dini ya haki ili kuifanya ishinde dini zote, ijapokuwa washirikina watachukiwa.”*
>
> *Na Surah ya 3:110 “Nyinyi ndio Umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishwa watu (ulimwenguni)-mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu na mnamwamini mwenyezi Mungu.”* (S = Surah = sura ya Kurani, kitabu kitakatifu cha Uislamu)?

Kadhalika, ile asili hasa ya Allah, kama ilivyoonyeshwa kwa mara ya kwanza ndani ya Kurani, sivyo kama sisi tumjuavyo Mungu wa Biblia na Yesu Kristo. Uislamu na imani ya Kikristo huonekana zinafanana kwa juu juu tu.

| **Wakristo na Waislamu hukubaliana kwamba:** | **Lakini Uislamu hupinga Biblia kwa kudai kwamba ….** |
|---|---|
| Mungu aliumba ulimwengu na vyote vilivyomo pamoja na mbingu na jehanam.<br><br>Mungu ana uwezo wote, anajua kila kitu na yuko kila mahali wakati wote.<br><br>Mungu alifunua mapenzi Yake kwa wanadamu kupitia kwa manabii fulani.Mungu aliwapa wanadamu sheria za kuyaongoza maisha yao na kuwazuia wasitende mabaya.<br><br>Mungu atawahukumu watu wote. Watu fulani wataruhusiwa kuingia mbinguni na wengine wote watakwenda jehanam. | Yesu alikuwa nabii tu. Hakuwa Mwana wa Mungu (Surah 5:78). Yesu alikuwa mtu mwema tu. Hakuwa Mungu (Surah 5:19).<br><br>Mungu si utatu (Mungu Baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu) na kuamini hivyo ni kumkufuru Mungu (Sura 4:171; 5 :75-78,119). Yesu hakufa msalabani kwa ajili ya wenye dhambi (Surah 4:157).<br><br>Hakuna upatanisho wa mtenda dhambi na Mungu kwa njia ya kifo cha Yesu msalabani wala kwa njia yoyote ile (Surah 22:36, 37). |

## *1. 2 Kiini cha Ukweli wa Mambo*

**Ukweli na 1:** Kama Yesu si Mwana wa Mungu, lakini ni nabii tu, kama si sehemu ya Utatu, yaani si sehemu ya Mungu, na kama hakufa msalabani kwa ajili ya wenye dhambi ili kuwapatanisha na Mungu – basi Wakristo wote wameamini uongo. Itafuatia kwamba Biblia yetu siyo Neno la Mungu, Ukweli, kwani Biblia ile ya asili imebadilishwa na watu, sawa na Waislamu wasemavyo! Kwa hiyo bado hatujaokolewa na tutakwenda jehanam, kwa sababu tunaamini kitu ambacho Mungu hakukisema!

**Ukweli na 2:** Lakini, kama Yesu ndiye mtukufu Mwana wa Mungu, kama Biblia ndio ukweli, kwa sababu ni Neno la Mungu lisiloweza kubadilika, na kama Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu, basi Waislamu wote wamepotea na watakabiliwa na hukumu na kwenda jehanam kwa sababu wamekataa kupokea huruma ya Mungu ya wokovu.

**Waislamu husema:**

"Tunao ukweli wa mwisho. Biblia siyo kweli, kwa sababu ilibadilishwa, ndiyo sababu Mungu alileta Kurani ili watu wote wapate kuamini njia iliyo sahihi."

**Wakristo husema:**

"Biblia tuliyonayo ndiyo Neno la Mungu lisilobadilika. Tunaweza kuamini yote Biblia inayosema."

**Je ni nani walio na ukweli?**


Waislamu husema: "Sisi".
Wakristo husema: "Sisi".

Tunawezaje kujua? Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba kile tunachokiamini sisi ndio ukweli wa Mungu?

Inatubidi tuyachunguze maswali haya kwa uangalifu sana, kwa sababu maisha yetu ya milele yanategemea uamuzi wetu!

## *1.3 Tuangalie Historia*

Bwana Yesu alizaliwa katika nchi ya Israel, aliishi maisha yake yote katika nchi hiyo na alisulubiwa na kuuawa huko. Alifufuka kutoka kwa wafu akapaa mbinguni. Nchi ya Israel ipo katikati ya mabara matatu yaliyo makubwa sana: Bara la Ulaya, Bara la Asia na Bara la Afrika.
Mitume na Wainjilisti walipoanza kuwahubiria watu Habari Njema, yaani Injili, na Agano Jipya lilipokamilika kuandikwa, Injili ilienea kwa haraka sana, kwanza kwa mataifa yaliyo karibu na Israel na pia kwa nchi ya Uhabeshi (Ethiopia) na kaskazini mwa Afrika, kisha katika Ulaya na baadaye kwa mataifa mengine. (Soma Matendo 2) na zingatia nchi zilizotajwa. Ndiyo sababu wewe uliweza kujifunza habari za Mungu na Bwana Yesu Kristo na yale aliyokufanyia!



Lakini jirani na marafiki zako wengi hawamjui. Je watafahamuje?

Katika zama zile za Agano Jipya nchi kadhaa zilikuwa haziwezi kufikiwa kwa urahisi na Mitume na Wainjilisti. Kati ya nchi hizo ilikuwapo nchi ile yenye jangwa kubwa ya Arabia. Walikuwako Wakristo wachache katika taifa hili lakini hatuna hakika hata kidogo kama kweli walimpenda Bwana Yesu. Pengine hata hawakuwa na Biblia. Vivyo hivyo, Wayahudi waliofanya makazi katika nchi ya Arabia hawakuweza kuendelea kushikilia mapokeo ya maandiko ya Agano la Kale.

Shughuli kubwa ya watu wa nchi ya Arabia ilikuwa ni ufugaji wa wanyama kama mbuzi, kondoo, farasi na ngamia, na wengine walikuwa wafanyabiashara. Kwa vile wakati huo hapakuwa na malori makubwa wala reli, usafiri wote wa nchi kavu ulifanyika kwa kuwabebesha mizigo ngamia. Njia moja kuu ya biashara kutoka Afrika kuelekea Ulaya na Asia ilipitia nchi ya Arabia. Wafanyabiashara walileta watumwa na bidhaa kutoka Afrika na kuziuza kwingineko, na pia walirudisha bidhaa nyingine Afrika kama vile hariri na viungo.

# 2. Muhammad, Mtume wa Uislamu


## *2.1 Uislamu ulivyoanza*

Idadi kubwa ya watu wa Arabia walikuwa wanafuata dini za asili. Waliamini miungu wengi ambao walikuwa wanaabudiwa katika nyumba maalum takatifu inayoitwa "Ka'aba". Neno "Ka'aba" ni neno la Kiarabu linalomaanisha kitu chenye umbo la miraba sita iliyo sawa. Katika nyumba hii, sanamu ya mungu aliyeitwa Hubal iliwekwa. Sanamu hiyo ya Hubal lilitoka katika nchi ya Moabu iliyokuwa mashariki mwa Israel. Huko ndiko "ha-Baal" alikoabudiwa, ambaye Jahweh Elohim, Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, Mungu wa Israel, aliwakataza watu wake mara nyingi wasimwabudu wakati wa Agano la Kale! (Hesabu 25:1 -3; Walawi 18:1- 5; Waamuzi 2:10 - 13; 1Wafalme 18:16-40). Unaweza kuona kufanana kwa 'Hubal' na 'ha-Baal', na hata zaidi tunavyofahamu katika lugha za Kiebrania watu hawakuandika vokali (yaani a, e , i, o, u) bali herufi h – b – i tu.

*Mambo yote tunayojua kuhusu Muhammad,*
*jamaa yake na marafiki zake, na historia ya awali ya Uislamu,*
*yanatokana na vyanzo vya Uislamu.*
*Bila vyanzo hivyo tusingeweza kujua lolote.*

## *2.2 Kabla ya kuzaliwa kwa Muhammad*

Vyanzo vyetu vya habari vinatuambia kwamba babu yake Muhammad hakuwa na wana wa kiume. Alikwenda Ka'aba kusali akiomba apate watoto wa kiume. Aliweka mikono yake juu ya sanamu ya Hubal na kusema: "Tafadhali Allah, nipe watoto wa kiume." Aliahidi kwamba ikiwa angepata watoto kumi wa kiume, angemtoa mmoja wa watoto hao kama kafara kwa Hubal/Allah. Alipata watoto 10 wa kiume! Aliporudi kwenye sanamu ya mungu Hubal – ambaye alikuwa anaitwa 'bwana wa mji huu' – bahati ikamwangukia Abdallah (jina hili linamaanisha 'mtumishi wa Allah'), ambaye baadaye ndiye aliyekuwa baba yake Muhammad. Kutokana na mwongozo na ushauri wa mchawi fulani, Hubal aliombwa akubali ngamia 100 badala ya Abdallah, naye akakubali. Hivyo ndivyo Abdallah alivyoweza



kuishi. Naye katika uhai wake akamzaa Muhammad.
Hayo yote yanaonyesha kwamba Muhammad alizaliwa katika ulimwengu uliotawaliwa na dini ya kuabudu sanamu na uchawi. Hakika mambo hayo yalimuathiri. Tunasoma hivi katika Kurani:
“Nimeamrishwa nimtumikie Bwana wa mji huu” (Surah ya 27:91).
Bila shaka Waislamu wote watasema kwamba anayemaanishwa hapa ni Allah. Huenda pengine wako sahihi! Lakini wakati huo Bwana wa Maka alikuwa Hubal. Licha ya hilo, Allah ndilo jina lililokuwa likitumiwa vile vile na mungu-wa-juu (“il-lah” = yule mwenye nguvu), ambaye pia ndiye aliyekuwa akiitwa baba wa ile miungu mitatu ya wanawake, al-Lat, al-Uzza na al-Manat. Hawa “mabinti wa mungu” ndio waliokuwa wakiabudiwa katika sehemu kubwa ya nchi ya Arabia wakati ule.

### *2.3 Maisha ya Ujana wa Muhammad*

Muhammad alizaliwa mwakawa 570, mjini Maka ambao ulikuwa mji mkuu wa kibiashara wa nchini za Arabia. Baba yake alifariki kabla Muhammad hajazaliwa. Mama yake alifariki alipokuwa na umri upatao miaka sita. Kwa hivyo Muhammad aliachwa yatima. Alitunzwa kwanza, na babu yake, ambaye naye alifariki baada ya kukaa na Muhammad kwa kipindi cha mwaka mmoja hivi. Ndipo Muhammad akachukuliwa na mjomba wake. Kwa jumla, Muhammad alitunzwa na baba walezi watano kabla hajatimiza umri wa miaka minane.
Muhammad alipokuwa na umri wa miaka 25 alifunga ndoa na mwajiri wake, Bi mkubwa mjane aliyefiwa na waume wawili, aliyeitwa Khadija. Tunaambiwa kwamba Muhammad aliishi maisha safi na alikuwa kijana mkimya. Ile ndoa na Bibi Khadija, ambaye alimzidi umri Muhammad kwa miaka 15, ilidumu kwa miaka 25 na iliishia kwa kifo cha Khadija. Yaonyesha wawili hawa walikuwa na uhusiano mzuri katika ndoa yao. Walijaliwa kupata watoto kadhaa, lakini aliyekuwa mtoto wao pekee wa kiume, alifariki alipokuwa mchanga. Muhammad hakusahau kifo cha mtoto huyo hata siku moja.

### *2. 4 Mafunuo ya Kwanza ya Muhammad*

Alipokuwa na umri wa miaka 40 Muhammad alianza kutafuta maana ya ndani ya maisha. Mara nyingi alitoka nje ya mji hadi kwenye pango lililokuwako kwenye Mlima Hira ili kutafakari, wakati mwingine alikaa huko kwa siku kadhaa. Sikumoja alipokuwa katika pango hili, alisikia sauti za ajabu-ajabu ambazo baadaye alidai kuwa ni mafunuo yaliyotolewa na malaika Gabriel. Mafunuo hayo ndiyo hatimaye yakawa “kitabu kitakatifu” cha Kiislamu, Kurani.
Mwanzoni, Muhammad aliogopa sana. Lakini baada ya hapo aliendelea kupokea

mafunuo hayo kwa miaka ipatayo 22 au 23 hadi kifo chake. Mapokeo ya Kiislamu yanaripoti kwamba Muhammad aliathiriwa vya ajabu na kuingiwa na wasiwasi mkubwa kuhusu mafunuo hayo. Waislamu husema kwamba wakati wa kupokea mafunuo hayo, Muhammad alisumbuliwa sana. Wakati mwingine alitoka povu kinywani na kunguruma kama ngamia. Alionekana kama mtu aliye nyang'anywa roho yake na alionekana kama amelewa. Kutokana na hali hiyo, si jambo la kushangaza, kwamba marafiki zake wengi walimpachika majina mengi, kama vile " kama *aliyeshikwa na mapepo*" (Sura 37:35; 44:13; 52:29; 68:2; 81:22); "*mchawi"* (Sura ya 10:2; 15:16; 38:3) *"aliyerogwa"* (Sura ya 17:50; 25:9; 44:13; 81:25). *"Mpiga ramli"* Surah 52:29; 69:42) na *"mshairi"* (Surah ya 37:35; 52:30; 69:43).

Mafunuo ya kwanza ambayo Muhammad alipokea yalisisitiza kwamba kuna mungu mmoja tu, naye ni Allah, na kwamba sanamu zote sharti ziharibiwe. Yakaongezwa maonyo mengine kwamba kuna hukumu inayokuja, hitaji la watu kuishi maisha mema, na uwezekano wa maisha ya milele mbinguni au jehanam. Mambo hayo yote yalielezwa wazi kwa lugha ya picha, na bilashaka yaliwapendeza sana watu walioyasikia.

Mwanzoni Muhammad alihubiri na kupata mafanikio kidogo. Watu wa Maka walimdharau. Mkewe ndiye aliyekuwa muongofu wake wa kwanza. Lakini, kadiri miaka ilivyopita watu kama mia mbili wengine raia wa Maka walimfuata. Siku moja Muhammad alipokea mafunuo ambayo yaliwapendeza sana watu wa Maka. Je, mwawafikiriaje hawa watatu, al-Lat, al-Uzza na al-Manat? Maombi yao yatarajiwe." Hayo ndiyo maneno yaliyosemwa kila mara wapagani walipokuja kufanya karamu zao za kidini kwenye Ka'aba na kutembea wakilizunguka Ka'aba mara saba huku wakiyakariri maneno hayo. Hivyo watu wengi wa Maka waliingia Uislamu na mateso ya Muhammad na wafuasi wake yalikoma kwa muda. Lakini muda mfupi baadaye, Muhammad alibadili mawazo yake, akidai kwamba aya hizo zilikuwa na uvuvio wa Shetani (ndizo ziitwazo aya za Shetani) na kwamba malaika Gabriel alikuwa ameyaondoa yale maneno ya mwisho yasemayo: "... maombi yao yatarajiwe." Kufuatana na mtindo huo, aya kadhaa za Kurani zilifutwa, na nyingine zikaingizwa badala yake.

### *2.5 Muhammad atorokea Medina*

Kubadilishwa kwa "mafunuo" namna hiyo kuliwafanya watu wa Maka kukasirika zaidi. Hivyo Muhammad aliamua kukubali wito wa kwenda kuishi mji wa Yathrib ulio umbali wa kilomita 250 kaskazini mwa Maka. Hili lilitokea mara baada ya kifo cha Khadija na Abu Talib, mjomba wake ambaye alikuwa mtu maarufu na mlinzi wa Muhammad wakati wote. Watu wachache mjini Yat-

hrib walikuwa Waislamu, lakini kulikuwako huko pia Wayahudi wa makabila matatu na wapagani wachache. Hawa walihitaji kupata mtu wa kuwaongoza na kusuluhisha migogoro inayotokea miongoni mwao. Hivyo mnamo mwaka 622 Muhammad 'alitoroka' kwenda Yathrib, mji ambao baadaye ulijulikana kwa jina la Medina (Mji wa mtume).

Kama tulivyojifunza mapema kutoroka kwa Muhammad kutoka Maka kwenda Medina kunaitwa *Hijrah* na kwamba huo ndio ulikuwa mwanzo wa Uislamu (622BK) na mwanzo wa kalenda ya Kiislamu. Ilikuwa Medina ambako Muhammad alitambuliwa kama kiongozi wa jamii, yaani *"umma"* wa Kiislamu kwa mara ya kwanza. Huo ndio msingi ambao juu yake sheria ya Kiislamu ilianzishwa, na Muhammad aliinukia kuwa kiongozi wa dini na vile vile kiongozi mashuhuri wa siasa katika mji huo wa Serikali. Mtu mmoja alisema hivi:

**"Uislamu unakuwa Uislamu tu pale Uislamu unapotawala."**

## *2.6 Mabadiliko katika maisha ya Muhammad*

Kuanzia wakati huo, mfumo mpya, kwa Muhammad, akiwa sasa na umri wa miaka 52, na katika Uislamu: yule mwanaume asiyependa makuu, mkimya na mkweli alikuwa kiongozi wa siasa mwenye mamlaka makubwa. Alifunga ndoa na wanawake 13, na siyo tu kwa ajili ya kuwapa makazi na ulinzi wajane wenye shida, kama vile ambavyo Waislamu wangependa kufikiri hivyo. Jambo hili limeandikwa kwa upana katika mapokeo ya Uislamu ya miaka ya mwanzoni.

**Maisha ya Muhammad – kwa muhtasairi:**

**Mwaka wa 570: Alizaliwa mjini Maka**
**Mwaka wa 595 : Alifunga ndoa na Khadija**
**Mwaka wa 610 : Alipokea mafunuo ya kwanza**
**Mwaka wa 622: Alihamia Yathrib= *Hijrah* na mwanzo wa kalenda ya Kiislamu**
**Mwaka wa 632 : Alifariki mjini Medina akiwa na umri wa miaka 62**

Mke mdogo wa Muhammad aliitwa Aisha (Ayesha). Alikuwa na umri wa miaka saba alipofunga ndoa naye, lakini "hakumjua" hadi alipotimiza umri wa miaka tisa. Ni jambo la kusisimua kweli kuambiwa kwamba "Aisha alichukua madoli (wanasesere) yake alipohamia nyumbani kwa Muhammad kutoka nyumbani kwao. (Sahih Muslim, Vol. 3, uk 716).

Ili kuweza kutosheleza mahitaji yake mwenyewe, familia yake na mahitaji ya watu wapatao 100 waliofuatana naye kuja Medina, alilazimika kutafuta njia

ya kujikimu maisha. Kwa hivyo walivamia mojawapo ya misafara ya ngamia ya watu wa Maka. Wakanyang'anya bidhaa zao zote na ndugu walilazimishwa kulipa fedha ili kuwakomboa ndugu zao walioshikwa mateka ndipo waruhusiwe kurudi nao Maka. Sisi leo tunawaita watu kama hao "majambazi" au "wanyang'anyi" kwenye njia kuu. Lakini katika Uislamu vita hivyo vilikuwa ndio mwanzo wa "vita vitakatifu" *(jihad).* Tunasoma hivi katika mapokeo ya Uislamu:

"Hii ndiyo njia nzuri kabisa ya kupata faida za kiroho na za kimwili pia. Ushindi ukipatikana, nchi inapata mali nyingi iliyokamatwa kwa adui ambayo haiwezi kulinganishwa na mali iliyopatikana kutoka vyanzo vyovyote vingine vya mapato. Kama kuna kushindwa au kifo, kuna ahadi ya kukaa mbinguni milele …"(Mishkat Vol. 2, uk 253).

Kama kawaida, watu wa Maka nao walilipiza kisasi, hivyo Waarabu wakapigana vita vya Badr. Katika vita hivyo, jeshi la Waislamu 300 wa Medina lilijipanga sehemu nzuri na kupata ushindi dhidi ya jeshi la Maka lenye askari 1000, jambo ambalo lilitafasiriwa kwa kujidai, kwamba ushindi ulipatikana kwa Allah (Mungu) kuingilia kati. Mapambano kadha yalifanyika, na Waislamu ambao majeshi yao yalikuwa yanazidi kuwa makubwa walipata ushindi isipokuwa katika pambano moja tu. Ni katika wakati ule Muhammad alipopata "mafunuo" yafuatayo:

> *"…… piganeni na kuwaua wapagani popote mtakapowakuta, na kuwakamata, wavizieni na wangojeni mafichoni .. Kwa hivyo mnapokutana na makafiri, wakateni shingo zao … Piganeni dhidi ya wale wasiomwamini Allah wala siku ya mwisho, wala hawaharamishi alivyoviharimisha mwenyezi Mungu na mtume wake (yaani Muhammad!) .. Piganeni hadi pale watakapolipa Jizya (kodi maalum inayolipwa na wasio Waislamu) kwa hiyari na kunyenyekea. .. Endeleeni kupigana nao mpaka yasiwepo mateso na ukandamizi mpaka kutakapo kuwa haki na wote kila mahali kumwamini Allah …." (Surah 9:5; 47:4; 9:29; 8:39)*



Uislamu umeugawanya ulimwengu katika himaya mbili yaani: *'Dhar-ul-Islam'* (nyumba ya Uislam – eneo/nchi inayo tawaliwa na Uislam) na *Dhar-ul-Harb* (nyumba ya vita, yaani eneo/nchi ambayo bado haija tawaliwa na Uislamu).

Lengo ni kuutawala ulimwengu

wote, na nchi yoyote isiyo ya Kiislamu inayotawaliwa na Sharia (Sheria ya Kiislamu) kila jitihada ifanyike ili kuileta nchi hiyo chini ya himaya ya Uislamu.

### *2.7 Muhammad kule Medina*

Hebu sasa tuyaangalie kwa karibu matukio ya kule Medina. Tulisha arifiwa kwamba kulikuwako na makabila matatu ya Wayahudi ambayo yaliishi kule Medina ambayo yalikataa kumtambua Muhammad kama nabii aliyetoka kwa Mungu. Walilazimishwa kulipa deni kubwa kwa ajili hiyo. Aidha walifukuzwa kutoka mji huo au waliuawa. Tukio moja lilikuwa ni Muhammad kuamrisha wanaume wote kutoka kabila moja la Wayahudi kuchimba mitaro kwenye soko la Medina. Baada ya kuikamilisha kazi hiyo, aliamrisha wanaume wote, watu kati ya 600 na 800 wauawe kwa kukatwa vichwa. Wake zao waligawanywa miongoni mwa Waislamu kama wake vimada. Muhammad mwenyewe alimchukua mmoja aitwaye Rihana, na huyo hakuwa kimada pekee aliyekuwa naye (kwa kuongezea na wake zake wengine) ! Jinsi Muhammad alivyoongezeka kuwa mwenye nguvu zaidi ndivyo jinsi tabia yake ilivyobadilika. Alitoa amri ya kuuawa kwa wanaume wengi, ambao aliwataja kuwa ni ‘adui’ wa Allah na mtumishi wake. Jumla ya mauaji 27 ya aina hiyo yamerekodiwa (Habari zinapatikana ndani ya kitabu kiitwacho *Siratu’l Rasul* kilichoandikwa na Ibn Ishaq, na kuhaririwa upya na Ibn Hisham).

### Mafunuo ya Muhammad yalimletea faida nyingi

‘Mafunuo’ mengi Muhammad aliyopokea yalikuwa ni kwa faida binafsi na manufaa yake mwenyewe. Mathalan, Kurani inaruhusu mwanaume wa Kiislam kuoa hadi wanawake wanne (ambapo mwanamke haruhusiwi kuwa na mume zaidi ya mmoja), lakini Muhammad tu alikuwa na ruksa ya kuoa wanawake wengi kadiri alivyopenda.

> *“Ewe Nabii! tumekuhalalishia wake zako … na wale uliowatamalaki kwa mkono wako wa kulia (wasichana watumwa) … na tumekuhalalishia mwanamke yeyote anayeamini ambaye anajikabidhi roho yake kwa Nabii kama nabii atapenda kumuoa. Hii ni kwa ajili yako tu na siyo kwa ajili ya waumini wengine! Na waweza kumuahirisha (kumpumzisha) yeyote miongoni mwao kama upendavyo, na waweza kumpokea yeyote kama upendavyo. Huwezi kulaumiwa endapo utapenda kumualika (kumrejesha) mmoja kati ya wale ambaye ulimpumzisha.” (Surah 33:50 –51)*

Tunajifunza kutoka mapokeo ya Kiislamu hali ilivyokuwa mafunuo hayo yalipo funuliwa: mke kipenzi cha Muhammad, mtoto Aisha aliripoti hivi:

*"Nilikuwa nikiwasengenya wale wanawake waliojitoa kwa Nabii wa Allah. Kwa hiyo nikauliza, Je, mke hujitoa mwenyewe? Hapo ndipo Mwenyezi Mungu mwenye nguvu akafunua akisema: 'Waweza kumuahirisha umtakaye na unaweza kumsogeza yeyote umtakaye' … nikasema, 'kwa mimi nionavyo Bwana wako anaharakisha kuyatimiza mapenzi yako." (Mishkat 1, uk 210)*

**Wake wa Muhammad + vimada:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Khadija (umri wakati wa ndoa ) | 40 |
| 2. | Sa'uda Bint Zama | 30 ? |
| 3. | Aisha binti Abu Bakr | 9 |
| 4. | Hafsah Binti Umar | 18 |
| 5. | Zainab Bint Khusaima | 30 |
| 6. | Umm Salama | 29 |
| 7. | Zainab Bint Jahsh | 38 |
| 8. | Juweiriyah | 20 |
| 9. | Rayhanah (kimada wa Kiyahudi) | ? |
| 10. | Maryam (Mkristo – kimada) | ? |
| 11. | Safia | 35 |
| 12. | Umm Habiba | 17 |
| 13. | Maimuna | 27 |

***Muhammad alikuwa na umri wa zaidi ya miaka 50 alipofunga ndoa na wanawake hawa wote, isipokuwa mkewe wa kwanza, Khadija.***

Haikuruhusiwa kupinga mamlaka ya Muhammad.

> *"Endapo suala limeamuliwa na Allah na Mtume wake (Muhammad), si halali kwa muumini …. kuwa na maoni yanayopinga uamuzi wao." (Surah ya 33:36)*

Suala lililoleta ubishi ni kwamba, kinyume na sheria za zamani zilizokuwapo, Muhammad alifanya mapenzi na kufunga ndoa na mke wa mwanawe wa kumlea, Zaidi, baada ya kumrubuni Zaidi ampe mkewe talaka. Siku moja, Muhammad alimtendea vibaya mmojawapo wa wake zake. Akaapa mbele yake na mbele ya mkewe mwingine, kwamba atawafanyia kitu kizuri endapo wataficha siri ya kosa lake. Hata hivyo, wanawake hao walikataa. Papo hapo funuo lifuatalo likaletwa: *"Unatafuta radhi kutoka kwa wake zako …. Hakika Mwenyezi Mungu amekupa sheria ya kufungua nadhiri zako…na Allah ndiye mlinzi wako katika hili….".(Surah ya 66:1- 2)*

Kutokana na mafunuo hayo alitiwa moyo kuvunja nadhiri zake. Basi tusishangae kwamba kuelekea mwishoni mwa uhai wake alisema:

*"Yeyote anayenitii ataingia paradiso na yeyote asiyenitii ameikataa paradiso."* (Mishkat 1, uk. 173).

## *2.8 Mwisho wa maisha ya Muhammad*

Muhammad alifariki mwaka 632BK, lakini siyo kabla ya kuuteka mji wake wa zamani Maka mnamo mwaka 630BK. Aliukabili mji huo na wapiganaji 10,000


ndipo hatimaye wakazi wa Maka walisalimu amri bila hata ya kufanya jitihada zozote za kuupigania. Muhammad alivunjilia mbali sanamu zote za miungu, lakini alibakiza mapokeo mengi ya ibada za kipagani katika dini yake ya Kiislamu hasa yaliyokuwa yanahusu Ka'aba, na mapokeo mengineyo.

## *2.9 Tathmini ya Muhammad*

Mafanikio aliyoyapata Muhammad katika uhai wake kwa kweli yanashangaza sana. Alianza maisha akiwa mvulana yatima, fukara lakini aliinukia katika mamlaka na kuwa mtawala wa ghuba yote ya Uarabu. Ni lazima, vile vile, apewe sifa kwa kuwachukua watu wa mataifa mbali mbali ya Uarabu kutoka hatua ya kuabudu sanamu na ibada za miungu wengi hadi kwenye imani thabiti ya mungu mmoja tu. Hata hivyo, hakufikia kilele cha maadili na kustahili kuitwa mtu wa mfano kwa binadamu wengine, na wala hakutosheleza kabisa sifa za utume kama zilivyo katika Biblia.

## *2.10 Kuenea kwa Uislamu*

Muhammad aliacha dola ya Kiarabu iliyojengeka vya kutosha ikiwa na jeshi imara lenye kujaa moyo wa kizalendo. Lakini baada ya kuondoka kwake, migogoro yenye sura mbaya, wivu na mfarakano ilijitokeza kati ya wafuasi wake wa karibu kabisa ambayo ilisababisha uasi na vita vya wenyewe kwa wenyewe vijulikanavyo kama *"ridda"*. Migogoro hiyo ilifikia kilele chake kwa kuuawa watu mashuhuri wawili, Uthuman, na Ali, warithi waliokuwa wenzi wa karibu sana wa Muhammad. Lakini licha ya migogoro hiyo ya ndani kwa ndani, majeshi ya Kiarabu yalianza kupata ushindi wa kuiteka Mashariki ya Kati yote,




**RAMANI YA ULIMWENGU
KUONYESHA KUENEA KWA UISLAMU**

Afrika ya Kaskazini, sehemu za Bara Hindi na Hispania. Baada ya muda, hapakuwa na haja tena ya Uislamu kuenezwa kwa vita, bali ulienezwa na wafanyabiashara. Wafanyabiashara hao walipenya Sahara kwa kutumia usafiri wa ngamia, na wengine kusafiri kwa meli zao kuteremka chini kuja pwani ya Afrika, na kuanzisha makazi sehemu nyingi za visiwa kama vile Mombasa, Zanzibar, Visiwa vya Ngazija (Comoro), Ibo na visiwa vingine vya Msumbiji); na kutoka huko walieneza himaya zao kwenye maeneo yote ya pwani.

**Leo, kila walipo watu watano, mmoja ni Mwislamu.** Kwa hili tunaona kuwa Uislamu ni dini ya pili kwa ukubwa hapa duniani, ikishindwa kwa idadi na jamii ya Kikristo.

## *2.11 Malengo ya Uislamu katika Afrika hivi leo*

Hebu tuangalie nguvu ya Uislamu kama ilivyo sasa katika Bara la Afrika. Siyo siri, kwamba kila jitihada inafanywa ili kugeuza Afrika kuwa Bara la kwanza la Kiislamu hapa ulimwenguni.

❖ Je, ulifahamu kwamba mwaka 1989 Wawakilishi wa Kiislamu kutoka nchi 24 za Afrika walikutana Nigeria kwa ajili ya kuanzisha *'Umoja wa Uislamu katika Bara la Afrika'?* Kwa mujibu wa maazimio yaliyoafikiwa katika mkutano huo, imeelezwa wazi wazi kuwa malengo yake ni kuimarisha kamati zote za Kiislamu kama sharti la awali kwa ajili ya kuimarisha Uislamu kila mahali, na kwamba katika nchi zote 24 wanachama vyeo vyote vikubwa vya siasa havinabudi kushikwa na Waislamu tu!

❖ Je, unafahamu kwamba fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa misikiti na shule za Kurani kila mahali, hata katika nchi ambako kuna Waislamu wachache tu? Mathalan, nchini Malawi, misikiti mingi inajengwa kwa gharama ya nchi za Kiislamu. Waislamu wa Ethiopia sasa wanajigamba kwamba idadi yao imeshavuka hesabu ya waumini wa Kanisa la Orthodox. Hata nchini Botswana, ambako mpaka miaka ya hivi karibuni kwa kweli ilikuwa sawa na kusema hakuna Waislamu lakini hivi sasa misikiti mingi imejengwa, mara nyingi misikiti hiyo inaunganishwa na shule ambazo elimu hutolewa bure hadi kiwango cha digrii, na hata wanafunzi hupelekwa ng'ambo kusomeshwa katika vyuo vikuu vya Kiislamu.

❖ Je, una habari kuwa Waislamu wanawekeza fedha nyingi sana katika sekta ya uchumi katika nchi za Afrika kuzifanya nchi hizo kuwa tegemezi kwa nchi za Kiislamu na kwa jinsi hiyo kuweza kumiliki uchumi wao, na hatimaye kuzitawala nchi hizo?

Hili si jambo la ajabu, kama mtu atazingatia Kurani na mafundisho yake. Utajiri wa mafuta wa nchi za Kiarabu umezipa nchi hizo utajiri mkubwa usiokwisha, na utajiri huo sasa hutumiwa kueneza Uislamu na kuihujumu imani ya Kikristo, ambayo Waislamu wanaona ndiye mpinzani mwenye nguvu kupita wote katika Bara la Afrika. Jambo hili linaonekana dhahiri kila mahali barani Afrika. Nani atapata ushindi katika pambano hili la kuwania kuziteka roho za watu wa bara

hili? Je, sisi Wakristo tutazinduka usingizini na kutia jitihada zetu zote kuinjilisha watu, kuwafanya mitume na kuwafundisha? Je, tunayo malengo yoyote ya kuwavuta Waislamu wakubali kwamba Yesu Kristo ndiye hasa njia yao ya pekee ya kupatia uzima wa milele? Au, tuwaache Waislamu, wanaume kwa wanawake waendelee kuwa watumwa wa Uislamu?

**Sisi Wakristo tunaweza kufanya nini kuhusu jambo hili?**
Bwana wetuYesu Kristo alisema:
*"Mkinipenda, mtazishika amri zangu." (Yohana 14:15)* Alitupatia Amri Kuu na Agizo Kuu: *"Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote .. Mpende jirani yako kama nafsi yako." "Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi" (wakiwamo Waislamu wa Kisomali, Kituaregi, Kihausa, Kiyao, Kimakonde, Kimakua, Kimwani, Kiswahili, Kiarabu, Kipakistani…)"na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi." (Mathayo 22:37- 39; 28:19 - 20)*

**Hebu fikiria:**
Tulipoamua kumfuata Bwana Yesu, tulikubali kutii mapenzi Yake. Sharti tufanye juhudi zote na kukua kiroho, kwa kulisoma Neno la Mungu kila siku. La sivyo, tutawezaje kuwa na tumaini la kuieneza imani kwa watu wengine, ikiwa sisi wenyewe hatuijui kikamilifu? *Mpango wa kuisoma Biblia kwa mwaka mmoja unaweza kuagizwa kutoka kwenye ofisi zetu.* Inatubidi pia tujifunze kuhusu Uislamu, tupate kujua jinsi Waislamu wanavyofikiri na kujisikia, ili tuweze kuongea nao kwa njia itakayowezesha waufahamu kikamilifu ujumbe wa Kristo, yaani Injili.

**Lakini kamwe tusisahau:**
Hatujaitwa ili tugombane na Waislamu ambao ni wananchi wenzetu! Tumeambiwa kwamba tusiishi kwa amani tu na maadui zetu, bali pia tuwapende – hata kama wao hawatupendi na wanakataa kumjia Mwokozi!


*Mfumo wote wa Uislamu ni uadui wa imani ya Kikristo*
*lakini Waislamu wenyewe ni watu wanaopendwa na Mungu!*
*Bwana Yesu Kristo alikufa msalabani kwa ajili yao pia.*
*Naye ametuamuru tuwafundishe Habari Njema.*

**➔Tafadhali pekua hadi ukurasa 106.**
**Yapitie yale maswali ya kujifunza sasa**

# 3. Kurani – Kitabu cha Uislamu

### *3.1 Ni kwa njia gani Kurani ilipatikana?*

Muhammad pekee ndiye aliyepewa Kurani katika kipindi cha miaka 23. Waislamu huamini kwamba ilitolewa sehemu kwa sehemu kutoka kwa "mawe ya mbinguni" na kufunuliwa kwa Muhammad na Malaika Gabriel (Jibril). Yote yaliyofunuliwa, Muhammad aliwafundisha wale aliokuwa nao na wao wakayakariri. Sehemu kadhaa ziliandikwa. Kwa kuwa Kurani inapinga Biblia katika mambo mengi muhimu, inatubidi tujiulize ni kitabu kipi kilicho sahihi kati ya vitabu hivi viwili. Kuchagua kwa makosa kutatuelekeza kwenye hukumu ya milele (yeyote ambaye bado hajafikia uamuzi wowote, tayari ameamua kumkataa Mungu!)



Je, Kurani ikoje? Kila Mkristo anayenuia kuwashirikisha Waislamu Injili, sharti aisome Kurani ili aweze kufahamu jinsi Waislamu wanavyofikiri.

### *3.2 Mpangilio wa Kuran*i

Kurani ina maneno machache zaidi ikilinganishwa na Agano Jipya, lakini ni kama lilivyo Biblia, Kurani pia imegawanyika katika sura na aya: Sura 114 na aya 6616. Katika Kurani, mlango unajulikana kama Surah na mstari ni aya, maana yake 'ishara'. Sura zote zimepangwa kulingana na urefu wake, isipokuwa tu ile ya kwanza, ambayo ni aina ya sala. Sura ya pili ndiyo ndefu kuliko zote, ikifuatiwa na ile ya tatu na kuendelea hadi Surah ya 114 ambayo ni fupi kuliko zote. Hakuna mfuatano wowote wa kihistoria. Unapofungua Biblia unakuta habari za uumbaji wa ulimwengu katika kitabu cha Mwanzo mlango wa kwanza, na tunatarajia mfuatano wa matukio uendelee: baada ya kuumbwa kwa Adamu, tunasoma kuhusu watoto wake, kisha Nuhu, Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, Yoshua, Samsoni, Daudi, Suleimani; na tunapotaka kusoma habari za Yesu tunafungua vitabu vya Injili. Katika Kurani hakuna mfuatano kama huo. Watu wengi na matukio mengi kutoka kwenye Biblia hutajwa katika Kurani, lakini hupatikana kiholela holela, bila uhusiano wowote wenye maana.

١ بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ
٢ الْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ
٣ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ
٤ مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ
٥ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ
٦ اهدِنَا الصِّرَاطَ المُسْتَقِيمَ
٧ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنعَمتَ عَلَيهِمْ غَيرِ المَغضُوبِ عَلَيهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ

**Surah 1 (in Arabic)**

### *3.3 Kurani hupinga Biblia*

Mambo mengi yaliyomo kwenye Kurani yametokana na Biblia. Hata hivyo ukweli wa mambo hayo umegeuzwa na kutoeleweka. Tutazame mifano kadhaa na kulinganisha na Biblia;

☪ Nuhu alikuwa na mtoto mmoja tu wa kiume – na mtoto huyo alikufa kwenye mafuriko (Surah 11:42-43).

✞Je, katika Biblia Nuhu alikuwa na watoto wangapi wa kiume? Na, je, walikufa kwa maji? (Mwanzo 6 + 7)

☪ Baba yake Ibrahimu, kwa mujibu wa Kurani, aliitwa Azar (Surah 6:74).

✞Je, kufuatana na Biblia, baba yake Ibrahimu aliitwa nani? (Mwanzo 11:31)

☪ Kwa mjibu wa Kurani Musa alipokelewa kama mtoto na mke wa Farao (Surah 28:89).

✞Nani aliyempokea Musa kama mtoto katika Biblia? (Kutoka 1:5-10)

☪ Farao alimwambia Hamani ajenge mnara mkubwa, ili yeye (Farao) "aweze kumfikia Mungu wa Musa." Bila mnara unaomaanishwa hapa ni ule wa Babeli (Surah 28:38).

✞Je, ni nani aliyeujenga ule mnara wa Babeli? (Mwanzo 10:32 - 11:4). Je, Farao na Hamani waliishi kwa wakati mmoja? La! Hapana. Farao aliishi miaka 800 baada ya kujengwa kwa mnara wa Babeli, naye Hamani aliishi miaka 900 baada ya Farao!

☪ Kurani hufundisha kwamba dhabihu ni nzuri kwa chakula tu, lakini si damu wala nyama ambayo humfikia Mungu, ila tu uchaji wa mwenye kuitoa hiyo dhabihu (Surah 22:37).

✞Biblia inaeleza wazi kwamba ni damu ya dhabihu ambayo huzifunika dhambi zetu (Walawi 16; 17:10), na kwamba kwa kumwaga damu yake, Bwana wetu Yesu Kristo "amewakamilisha hata milele hao wanao takaswa" (Waebrania 10:14); na kwamba "mara moja tu, katika ukamilifu wa nyakati, amefunuliwa, azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake." (Waebrania 9:26).

☪ Kurani hufundisha kwamba Mariamu, mama yake Bwana wetu Yesu, alikuwa dada yake Haruni na binti wa Imrani (Sura 19:17-28).

✞Je, ni kweli? Je, Musa alikuwa mjomba wa Bwana Yesu? Miriamu alikuwa dada yake Haruni, lakini yeye aliishi karibu miaka 1400 kabla Yesu hajazaliwa!

***Haya yote yanaonyesha kwamba haiwezekani vitabu hivi viwili, yaani Biblia na Kurani, viwe vyote vimetoka kwa Mungu. Muhammad alikuwa na habari za juu juu tu kuhusu Biblia, akaandika tu yale ambayo alidhani ni ya ki-Biblia.***

### *3.4 Vyanzo vya Kurani*

Hadithi nyingi za Kurani ni rahisi kubaini kuwa zimetoka sehemu nyingi kama vile Talmud, Mishna na vitabu vingine vya Kiyahudi. Hadithi nyingine kuhusu Yesu hazikuwa za ki-utume na hatimaye ilishindikana kuzifanya kuwa sehemu ya Agano Jipya.

Mbali na hadithi za ki-Biblia, kuna hadithi nyingine ambazo zinahusiana na zama za Muhammad. Hizi, bila ya shaka, ni zile aya zinazompendelea Muhammad na mitindo yake ya maisha na kuhalalisha amri na maagizo yake.Hadithi hizo zinaonekana kwa wingi katika Surah zile wakati Muhammad alipokuwa Medina.

**Vyanzo vya Kurani**

- ✪ Vitabu vya Kiyahudi
- ✪ Vitabu vya Pershia vya Imani ya dini
- ✪ Ibada za Kipagani za Waarabu
- ✪ Hadithi za Biblia
- ✪ Fikra za Muhammad


Kukariri Kurani ni tendo linalochukuliwa kuwa jema sana na Waislamu. Hata wengine wanaweza kukariri Surah nzima katika lugha ya Kiarabu, na kujivunia kuitwa *hafiz,* hata kama hawajaelewa kabisa ujumbe wa yale wanayo yakariri. Kwa hiyo kukariri kunaleta sifa kubwa kuliko kuelewa ! Manufaa ya kiroho hupatikana tu kutokana na kukariri "kitabu kitakatifu", na wala siyo kutokana na kukielewa. Katika jambo hili sisi Wakristo tunatofautiana sana na Waislamu.

Hatuna mashaka kwamba sehemu fulani za Kurani zilifunuliwa kwa Muhammad. Hata hivyo hatuamini kwamba mafunuo hayo yalitoka kwa Mungu, kwani ujumbe wa Kurani unapinga Biblia katika mambo mengi ya kimsingi kabisa. Kwa hiyo hatunabudi tuelewe kwamba uvuvio huo ulitoka kwa Shetani. Tunaamini kwamba Biblia ndilo Neno la Mungu, na tunazo sababu za kutosha kama tutakavyoonyesha baadaye.

### *3.5 Nini Kingine Tunastahili Kufahamu Kuhusu Kurani?*

***Kurani ilifunuliwa kwa namna saba***

Hata wakati wa Muhammad, sehemu fulani za Kurani tayari zilikuwa zinakaririwa na Waislamu. Hadithi moja ya kuchekesha inasimuliwa katika mapokeo:



*Umar, ambaye baadaye alikuwa Khalifa, yaani, aliyechukua nafasi ya Muhammad, aliripoti kwamba siku moja alikwenda msikitini akawasikia Waislamu wawili wanakariri Surah fulani, ambayo ilikuwa tofauti na jinsi alivyokuwa amejifunza kutoka kwa Muhammad. Kwa hasira, Umar aliwapeleka wote kwa Muhammad, akamwelezea kwamba wanakariri tofauti tofauti. Muhammad aliwasikiliza wote wakikariri (kwa njia mbalimbali), akasema kila mara "hivyo ndivyo ilivyo funuliwa". Umar alikiri kwamba hapo kutokuamini kulimwingia kutokana na tukio hilo. Muhammad alimgusa Umar kifuani na kusema: "Kurani hii imefunuliwa kwa namna saba, kwa hiyo kariri ile inayoonekana kuwa ni rahisi." (Mishkat 3, kur. 702 - 704)*

***Sehemu fulani za Kurani zimeondolewa na zingine kuwekwa badala yake***

Waislamu wa siku hizi wanatulazimisha sisi tuamini kwamba Kurani haijabadilishwa hata kidogo, hata sehemu ya herufi kama vile kidoti juu ya herufi 'i' isipokuwa iko sawa na maandiko yale ya awali yaliyoko mbinguni. Bila ya shaka huu ni upuuzi mtupu, ambao huonyeshwa wazi katika aya zifuatazo za Kurani yenyewe.

> *"Aya yoyote tunayoifuta au kuisahauliza tunaleta iliyo bora kuliko hiyo au iliyo mfano wake. Hujui kwamba Mwenyezi Mungu anao uwezo wa kila kitu?" (Surah 2:106) Na tunapoibadili aya kwa aya (nyingine), na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anajua anayo yateremsha, wanasema 'wewe ni mzushi tu!. Bali wengi katika wao hawajui (lolote). (Surah 16:101)*

Kilichotokea ni kwamba Muhammad alizibadili sehemu kadhaa za Kurani kwa kuondoa aya moja au mbili na kuweka nyingine. Aya ambazo Muhammad alizitoa zinaitwa *'mansukh'* na zile ambazo aliziweka badala yake zinaitwa *'nasikh'*. Hiyo ndiyo inayojulikana kama 'Sheria ya Kutangua'. Lakini kwa kuwa aya hizo zote za aina mbili bado zipo kwenye Kurani, Waislamu leo hawawezi kirahisi kutwambia aya za karibuni na kuacha zile za zamani. Kwa kuwa jambo hilo lilitokea kabla ya Kurani kuandikwa kama ilivyo sasa, hatuwezi kuwa na uhakika kwamba ni sehemu zipi zilizobadilishwa. Msomi mmoja wa theolojia

ya Kiislamu (Jalalu'd Din) alikadiria huenda ikawa kati ya sehemu tano hadi mia tano. Hata hivyo tuna uhakika kuhusu yafuatayo:

- ⌦ Upande wa kuangalia wakati wa sala ulibadilishwa (S. 2:142-144)
- ⌦ Utaratibu wa kugawanya urithi ulibadilishwa (S. 4: 7, 11)
- ⌦ Sala ya usiku ilibadilishwa (S. 73: 2, 20)
- ⌦ Adhabu ya uasherati ilibadilishwa (S. 4:15-16; S. 24 : 2)
- ⌦ Sheria zinazohusu 'vita vitakatifu' (Jihad) zilibadilishwa (S 2: 256; 9 : 3-5; 2:217; 47:4; 8:39)
- ⌦ Kulipiza kisasi kwa ajili ya matendo (S. 2: 178 ya jinai kulibadilishwa S. 5: 48; 17:33).

*[Angalizo: Neno "chafu" katika Surah 4:15 maana inayokusudiwa ni uasherati au matendo yenye kuleta aibu au kashfa.]*

Yote haya yalitokea, licha ya kauli za kusisitiza zilizomo ndani ya Kurani zisemazo:

***"Hakuna abadilishaye Maneno ya mwenyezi Mungu Allah (Surah 6:34).***
***"Hakuna mabadiliko katika maneno ya mwenyezi Mungu" (Surah 10:64)***

Kauli nyingine inayochanganya sana ni ile isemayo: *"Kama tungeliependa, bila shaka tungaliondoa yale tuliyokufunulia" (Surah 17:86).*

Kutokana na mgongano mkubwa wa kauli ndani ya Kurani, je, ni Mwislamu gani anaweza kuwa na uhakika juu ya ujumbe wake?

### *Kulikuwa na nakala mbali mbali za Kurani zilizotofautiana*

Tunafahamu kwamba sehemu kadhaa katika Kurani ziliondolewa au zinatofautiana na nakala za awali.

Baada ya Muhammad kufariki, Khalifa wa kwanza (Abu Bakr) alitoa amri kwa mara ya kwanza ya kuikusanya na kuiandika Kurani. Waislamu fulani waliandika yale waliyokuwa wamejifunza kutoka kwa Muhammad na ambayo walikuwa wameyakariri. Maandiko hayo yalifikia ishirini na manane. Hata hivyo, yale yaliyokuwa maarufu sana ni yaliyoandikwa na Ibn Masood, Ubai Ibn Ka'b na Abu Musa.

### *Kurani iliandikwa baada ya kifo cha Muhammad*

Baada ya kitambo kidogo, Khalifa Uthman alifahamishwa kwamba askari wake waliokuwa katika jeshi walikuwa wakikariri Kurani kwa namna mbali

mbali. Kutokana na hali hiyo, aliagiza kwamba aletewe nakala zote za Kurani zilizokuwako wakati huo. Kutokana na nakala hizo, nakala moja ilibuniwa na zingine zote za hapo awali zikateketezwa. Nakala hiyo iitwayo 'Uthman' ndiyo inayotumika hadi leo. Tunajua mambo hayo kwa undani kabisa kutokana na maandiko ya kitheologia ambayo yamehifadhiwa (Mishkat 3, uk 708). Licha ya hayo yote, bado Waislamu wanaendelea kudai kwamba hakuna badiliko lolote ambalo Kurani imefanyiwa, na kwamba Kurani ya Kiarabu iliyoko siku hizi ni sawasawa kabisa na ile iliyofunuliwa kutoka mbinguni. Lakini sisi tunafahamu ukweli wenyewe.

### *3.6 Wakristo wanapaswa kuichukulia vipi Kurani?*

Hapana shaka hata kidogo kwamba Waislamu huipa Kurani heshima ya juu kabisa, wengi wao wakiwa wameridhika kwamba vitabu vya Kurani vilivyopo sasa ni sawa kabisa na kile kitabu cha kwanza cha Kurani ambacho kiliunganishwa na Uthman. Kwa ajili ya ushuhuda wa Wakristo, hakuna haja ya kuwashambulia Waislamu juu ya 'kitabu chao kitakatifu' na kuwatenga wasitusikilize. Lakini basi, kila tunapoona ni muda muafaka tuulize maswali ya chemsha – bongo kama hivi:

🕮 Kama Kurani ilikuwa inapatikana hata wakati ule wa kifo cha Muhammad, kwa nini kulikuwa na ulazima kwa warithi wake kuihdika (tena) baada ya kupita miaka 20?

🕮 Kitabu chenu kinafundisha kwamba "hakuna mabadiliko yanayoweza kufanyika kwa Neno la Allah", ni kwa jinsi gani basi kwamba aya kadhaa za Kurani zimepotea kama mapokeo yenu yanavyofundisha?

🕮 Kwa nini maandiko ya Kurani yalitofautiana katika kipindi cha karne nzima baada ya kifo cha Muhammad, kwa kuzingatia kwamba ninyi mnasema ilinakilishwa kwa imla na malaika Jibreel (Gabriel) kama yalivyochukuliwa kutoka katika mawe ya mbinguni?

🕮 Madaam Kurani ndicho Kitabu Kitakatifu cha Waislamu, kwa nini ilionekana ni lazima kwanza kuteketeza makala mengi ya maandiko ya kwanza yaliyoandikwa kwa mkono? – **Kanisa la Kristo halikuthubutu kuharibu hata ukurasa mmoja wa maandiko ya Biblia; bali daima ilikuwa ni maadui wao, ndio waliounguza Neno la Mungu.**

# 4. Mapokeo ya Uislamu

Katika karne chache za mwanzo wa Uislamu, hali ya utulivu ilirejeshwa ndani ya Uislamu na mfumo wa theologia na miundo-mbinu mbali mbali ilianzishwa. Lakini ilibainika wazi wazi mapema kuwa haitawezekana kuwa na mfululizo mzuri wa kuitafasiri Kurani. Ni lazima matatizo yatatokea. Kwa hivyo, wanatheologia walitangaza kwamba anayeweza kuitafasiri Kurani kwa usahihi ni yule ambaye alipokea mafunuo yake.

## *4.1 Mapokeo yalihitajika ili kuifafanua Kurani*

Lakini, yule aliyepokea mafunuo ya Kurani amekwisha kufariki! Kwa hiyo, yale maelfu ya hadithi yaliyokuwa yamekaririwa na mamia ya watu kuhusu Muhammad yalianza kutafutwa na kukusanywa. Je, alisema nini? Alifanya nini? Aliruhusu mambo gani na kukataza mambo yapi?

Ukabuniwa mfumo wa kutafasiri Kurani. Waislamu wakaupa jina mfumo huo kuwa ni 'kutengeneza *tafsiri* ya Kurani.' Msingi wake ni yale ambayo Muhammad alisema, alifanya na aliruhusu; na jinsi alivyotenda. Maisha yake na mwenendo wake katika maisha, ndivyo vilionekana ni tafsiri sanifu ya Kurani.

## *4.2 Jinsi mapokeo yalivyokusanywa*

Hali hii ililazimisha *Hadithi* (mapokeo au hadithi) zote zikusanywe. Miaka ipatayo kati ya 250 na 300 baada ya kifo cha Muhammad, wanatheologia kadhaa wa Kiislamu walijitoa kufanya kazi hiyo kwa kujitegemea moja kwa moja. Anayejulikana zaidi kati yao, Al-Bukhari, alikusanya Hadith zipatazo 600,000. Baada ya kuzifanyia upembuzi, alichagua Hadith 7,200 (ambazo nusu yake zinafanana) zinazoaminika, na kuacha nyingine zote. Huu ulikuwa ni uamuzi wa peke yake bila ya kushirikisha jopo la wasomi wengine!

> **Maandiko yaliyokusanywa na Al Bukhari**
>
> **Miaka 250** baada ya Muhammad kufariki
> Hadithi zilizopokewa – **600,000**
> kutoka maripota **40,000,**
> na kuchaguliwa **7,200.**
> Hii ni asilimia **1.2 (1.2 %)** ya hadithi zilizoonekana zinaaminika, au zinakaribia kuaminika.

Vitabu sita vyenye mkusanyiko wa hadith mbali mbali ndivyo sasa vinavyokubaliwa kuwa ni "Sihahu sitta" = vitabu sita vilivyo sahihi, ambavyo ni vya al-Bukhari, Muslim, Abu Da'ud, at Timizi, Abu-Abdir-Rahim na Abu Abdullah Mohammad.

Kuaminika kwa kila Hadith kulithibitishwa kwa kuchunguza mstari wa maripota *(isnad)* waliokuwa na hadithi hizo, kama ni wanawake au wanaume wa kuaminika kwa kiasi gani. Je, wale maripota wa kwanza walikuwa katika duru ya wenzi wa Muhammad? Na, ni wanawake na wanaume gani walioendeleza mapokeo haya hadi hatimaye yaliporekodiwa?

Hivi ndivyo mkusanyiko wa methali na matendo ya kuaminika kweli kweli ya Nabii Muhammad yalivyochaguliwa kutoka kwenye mkusanyiko wa 'Hadith fasaha' za kuaminika kabisa uliofanywa na Al-Baghawi, ambao kwa kifupi unaitwa *'Mishkat*' jina kamili '*Mishkatu'l Masabih'*.

## *4.3 Hadith zinafundisha nini?*

Mkusanyiko wa Hadith zote umewekwa katika mpangilio fulani ulio na mada za aina mbali mbali kama vile imani, sala, ufahamu, kutawadha, mazishi, zaka, hajj, kufunga, biashara, utumwa, wosia na urithi 'vita vitakatifu', sifa za Muhammad, ndoa, talaka, chakula na ulaji, madawa, dhabihu, nguo na adabu, 'kuchaguliwa', viapo, adhabu na jinsi ya kuwatendea watu wanao acha Uislamu, ndoto, usafi, hukumu ya mwisho, na hata mambo madogo madogo kama kupiga chafya, kupiga miayo, kukata nywele na kunyoa ndevu, matumizi ya uturi (pafyum), usafi wa meno na pua, na mengineyo.



**The six accepted collections of the Hadith (Sihahu Sittah)**

Nyingine kati ya Hadith hizo zina uzito na maudhui yenye maana, lakini nyingine ni za kuchekesha.

Baadhi ya nukuu za Hadith:

> *"Mjumbe wa Allah alisema: Nzi akiangukia katika bakuli la mmoja wenu, mwingize kabisa, kwa sababu kuna ugonjwa katika bawa lake moja na madawa katika bawa la pili, na pia kwa sababu anaingiza bawa lenye ugonjwa kwanza. Kwa hiyo umzamishe kabisa." (Mishkat 2, uk 152)*

> *"Ibn Umar alimkaririri Mjumbe wa Allah (amani iwe juu yake) akisema: Muumini hula katika utumbo mmoja, bali asiye muumini hula katika matumbo saba."(Sahih Muslim 3, uk 1137)*
>
> *"Jabir aliripoti kwamba Mjumbe wa Allah (amani iwe juu yake) aliagiza watu walambe vidole vyao pamoja na bakuli, akisema: "Yeyote kati yenu anapokula chakula asifute mkono wake kabla hajaulamba mwenyewe au kumruhusu mtu mwngine aulambe!" (Sahih Muslim 3, uk 1119 - 1120).*

Kitabu kama kile cha mwongozo wa mambo *"yanayoruhusiwa" na "yasiyoruhusiwa"* kutenda (kilicho andikwa na Abdul Rehmad Shad, Kazi Publications, Lahore, 1983) ni maarufu, na kimejaa kanuni za kushangaza na za ajabu:

**Uk. 148** ♠ Yeyote yule aliye na mvi Allah atamwandikia thawabu moja kwa kila mvi na kumwondolea dhambi moja." Kwa hivyo, si vyema mtu anapokuwa mtu mzima kuondoa hataunywele mmoja wa mvi zake.

**Uk. 146** ♠ Inashauriwa mtu asichane nywele zake kila siku, kwa sababu mtume wa Allah alikataza kuchana nywele, isipokuwa mtu achane nywele kila siku ya pili.

**Uk. 93** ♠ Kumpa *talaka (tahlil)* mke mmoja ni jambo baya sana, na Mwislamu haruhusiwi kumrejea mke aliyemwacha hadi pale mume(wa pili) atakapoonja utamu wa mwanamke huyo kama ule aliofaidi mume wa kwanza.

**Uk.192** ♠ Kusema uongo hakuruhusiwi, isipokuwa katika mambo manne: (1) kusuluhisha Waislamu wanaogombana. (2) kupatanisha mume na mke waliogombana. (3) kusingizia madikteta na wakandamizaji, na (4) katika vita vya *jihad.*

**Uk. 299** ♠ Ni halali kutafuta *baraka* kutoka makaburi ya watakatifu fulani.

**Uk. 203** ♠ Haifai kwa mtumishi wa Allah kuwa na tabia ya kujikweza. Ni baraka kubwa sana kwa binadamu kuishi kwa amani, ambayo inaweza tu kupatikana kwa kujishusha.

**Uk. 82** ♠ Ni halali kabisa kumpa mkeo adhabu ndogo kutokana na tabia yake mbaya, lakini hairuhusiwi kabisa kumpa kipigo kikubwa... mwanamke ameumbwa kutoka ubavu – sehemu ya ubavu iliyojikunja sana - ile sehemu ya juu. Endapo utajaribu kuinyoosha utaivunja, na kama utaiacha ilivyo, basi itaendelea kujikunja.

**Uk. 183** ♠ Ni kosa kutengeneza au kuchora picha zinazofanana na wanadamu walioumbwa na Allah."

Waislamu wengi hujifunza mambo kama haya tangu utoto wao na kuhamasishwa kuiga Muhammad aliyofanya. Kama nabii wa Uislamu alikuwa mfano bora, basi njia iliyo salama kabisa ya kufikisha Waislamu mbinguni itakuwa "kutenda kama alivyotenda" (Sunnah). Jambo hili limesababisha Uislamu kuwa

dini ya nje. "Kufanya" mambo sahihi ndilo muhimu zaidi kwa Waislamu kulikoni 'kuwa' mtoto mtii kwa Mungu na kuonyesha shukurani kwake.

> *Waislamu hutimiza majukumu ya dini yao kupata uzima wa milele – Wakristo huchagua kufanya yaliyo mema kwa ajili ya kushukuru kwa yale Kristo aliyowatendea.*

## *4.4 Sunnah – Kuiga matendo ya Muhammad*


Muhammad amenukuliwa akisema:

> *"Ninawaachieni vitu viwili, mkivishika kwa makini vitu hivyo, hamtapotoshwa: Vitu hivyo ni – Kitabu cha Allah na Sunnah ya Mtume wake," (Mishkat 1, uk. 159).*

Ni dhahiri, kitabu cha Allah kinachosemwa hapa ni Kurani. Nayo 'Sunnah' ni uigaji wa yale Muhammad aliyoyafanya, aliyoyasema, aliyoyaruhusu au aliyoyakataza. Uigaji wa maisha ya Muhammad umekuwa mfano kwa Waislamu wote, na kwa hiyo Waislamu hujaribu kuiga maisha hayo kadiri wawezavyo.

## *4.5 Shariah – Mfumo wa Sheria wa Kiislamu*

Hapana shaka lolote kwamba Waislamu wataitaja Kurani na Hadithi kuwa ndiyo misingi ya maumbile ya maisha yao. Lakini jamii iliyo ya Kiislamu kwa kweli daima itatawaliwa na Shariah. Neno hili *'shariah'* maana yake ni "njia" (ya kwendea palipo na maji). Ni mfumo wa sheria na kanuni zilizopangwa kufanyika katika vitendo ambavyo havina ubishani, vya lazima, kama vilivyoainishwa na Muhammad, ambavyo mwenyewe alivifanya kwa nadra na kwa wakati aupendao. Vitendo hivyo vimeendelezwa katika historia ya Uislamu juu ya misingi ya kanuni hizo mbili zinazokubaliwa na wasomi wote wa Kiislamu na vile vile kwa kulinganisha na masuala ya kisasa yanayolingana na mambo kama hayo katika zama za Muhammad. Madhehebu ya Sunni wanafuata sheria kwa mujibu wa misingi hiyo minne ambayo ni Hanbali, Hanafi, Shafi'i na Maliki. Sheria hizi zinakubalika katika maeneo mengi, mathalan katika Afrika ya Mashariki, sheria ya Ash-Shafi'i ni maarufu sana.



Khomeini

**→ *Tafadhali fanya mapitio ya maswali ya Sura ya 3 na Sura 4***

# 5.0 Imani na Utendaji katika Uislamu


## *5.1 Imani ya Uislamu*

Imani ya Uislamu kwa kawaida hujumuishwa katika mambo matano ya msingi ambayo Waislamu ni lazima wayaamini. Mambo hayo ni:

- **Allah:** Mungu mmoja tu (umoja au upekee wa Allah, unaoitwa 'Tawhid' hutiliwa mkazo mkubwa.

- **Malaika zake:** wa aina zote mbili – malaika (malaikah) wema na wale wabaya (jinni) Surah 16:2; 19: 17; 2:31-32.

- **Vitabu vyake:** vyote vilivyofunuliwa (Surah 2:136; 4:136). Vinavyotajwa ni:
    - *Torati* (vitabu 5 vya Musa, au Agano la Kale lote)
    - *Zaburi* za Daudi
    - *Injili* – aliyopewa Nabii Isa (Yesu) au Agano Jipya.
    - *Kurani.* Kwa bahati mbaya, Waislamu hufundishwa kwamba vitabu vyote vilivyotajwa kwanza, leo havina maana, kitabu wanachotakiwa wakifahamu ni Kurani tu.




- **Manabii wote:** waliotumwa na Mungu (Surah 16:36; 4:164).
  Waislamu huamini kwamba jumla ya manabii waliotumwa na Mungu kwa mataifa yote ni 124,000 lakini ni manabii 25 tu waliotajwa majina. Miongoni mwao ni Adam, Nuhu, Abraham, Isaka, Yakobo, Yusufu, Musa, Daudi, Yesu na Muhammad.


- **Maisha baada ya kifo:** hii inajumuisha kuchaguliwa na kuja kwa Siu ya Hukumu ambayo hujulikana tu kwa jina la 'saa' (Surah 25:11; 9:29) ambayo ndiyo itakayoamua kama Mwislamu yupi atakwenda paradiso au jehanam.

(Tutazichunguza imani hizo katika sura ya 6. Habari zaidi zinapatikana katika vitabu vyetu vya Walimu).

## *5.2 Utendaji wa Uislamu*

Hizi pia hujulikana kama "Nguzo Tano za Uislamu: Nguzo hizo ni:

- **Ungamo***: (Shahada)* Kutamka wazi imani yake: "Hakuna mungu isipokuwa Allah na Muhammad ndiye nabii wa Allah." Hili ndilo ungamo la kwanza na la mwisho Mwislamu atakalosikia katika maisha yake, na lazima alitaje kila mara - kwa lugha ya Kiarabu tu. Maana ya ungamo hilo ni utii kwa imani ya Uislamu. Kwa hivyo, Waislamu watafanya kila jitihada ya kumlazimisha Mwislamu aliyeongoka kuingia Ukristo akariri ungamo hilo na kwa jinsi hiyo kumrejesha kwenye mfumo wa Uislamu.
- **Sala** (Salat) Sala tano za kila siku. Hizi ni mtungo wa sala ambazo hazinabudi kutamkwa mara 17 kwa siku wakati muumini anafanya vitendo vya ibada vinavyofahamika, (kama kupiga magoti, kusema sala, kusimama, n.k.) La kuzingatia ni kwamba sala hizi zinakuwa na maana tu zinaposemwa kwa lugha ya Kiarabu na kwa wakati na saa ile ya siku baada ya muumini kuwa ameyatii masharti yote ya lazima ya ibada na kutamka dhamira ya ibada.





- **Saum** (sawm) kufunga mwezi wote wa Ramadhan. Anayefunga anatakiwa asile chakula cho chote au kunywa (hata kumeza mate), na ajizuie kufanya starehe nyinginezo, tangu kuchomoza kwa jua hadi machweo. Kwa kuwa mfungo ni kitu kinachoangaliwa sana na jamii ya Waislamu, Ramadhan huwapa Waislamu-jina muda mgumu, na hasa kwa Mkristo aliyetokea kwenye Uislamu. Hata hivyo, Waislamu wanaruhusiwa kula, kunywa au kushiriki sherehe yoyote saa za usiku, na hii kwa kawaida hufanyika ki-anasa.
- **Zaka** (Zakat) – tamka *Zakah*, ni utoaji wa *sadaka*. Kiwango maalum cha sadaka inayotakiwa kutolewa kimetajwa na Waislamu wanatakiwa kutii bila kukosea ili waweze kupata thawabu baada ya kufariki kwao. Mwislamu anaruhusiwa kutoa sadaka nyinginezo kwa hiyari kama atakavyoona inafaa.
- **Hajj:** Safari ya kwenda Maka mara moja au zaidi katika uhai wa kila muumini, kama anao uwezo wa kufanya hivyo. Hajj inathaminiwa na kuonekana kama ndilo tendo la kilele cha kiroho katika maisha ya Mwislamu; na hata baadhi ya Waislamu huamini kwamba hija itawapatia masamaha ya dhambi zao zote. Wanaume Waislamu (au wanawake wakifuatana na waume zao au ndugu zao) aghalabu huhiari kutumia uwezo wao wa kifedha na kuacha starehe nyingine zote ilimradi wafanikishe lengo hili kuu.

# 6. *Mafundisho ya Uislamu*

## *6.1 Allah*

Waislamu humheshimu sana Allah na kumwogopa. Yeye ni *'tawhid'* yaani umoja usioweza kugawanyika, umoja pekee. Mkazo huo unapingana na 'miungu' wengi wanaoabudiwa na Waarabu (wanaoabudu miungu wengi), lakini hapana shaka, vile vile, inapinga uungu wa Yesu Kristo, Bwana wetu, na asili ya Utatu wa Mungu.



Allah hana mfano kabisa, hafanani na kiumbe chochote. Yuko peke yake na alivyo ni mkamilifu, nia yake, mamlaka au ujuzi wake, ni muumbaji wa kila kitu, vyema na vibaya, hakuna kinachoweza kutokea bila ridhaa yake – na hiyo hujumuisha dhambi. Allah yuko juu ya vipimo vya kibinadamu vya mema na mabaya, haki na makosa. Yeye ndiye mwenye haki katika lolote alitendalo, hata kama sisi wanadamu tunafikiri silo sahihi. Ni yeye pekee anayestahili kuabudiwa na kutiiwa.

Allah anaitwa *"al-Rahman"* na *"al-Rahim"* katika Kurani, yaani mwenye huruma na rehema, ingawa kwa kweli tabia hizo hupingana na nafsi yake kama inavyoelezwa katika Kurani yenyewe, Allah amepewa jumla ya majina 99 "yaliyo mazuri kabisa" katika Kurani na inafikiriwa ni jambo la sifa njema kuyataja majina hayo wakati mtu anaposali. Waislamu hutumia *'tasbih'* ushanga wenye aidha kokwa 33 au 99 pamoja na kokwa moja inayofanana na tone la maji pale kwenye kiungio inayomaanisha Allah. Wakati Mwislamu anaposali huyataja majina hayo 'mazuri kabisa", lakini la kusikitisha ni kwamba Waislamu hawajui kabisa jina la "Baba" (Isaya 9:6).

Kwa hakika inaonekana ni dhambi mbaya sana kudhani kuwapo kiumbe mwenza wa Allah. Yeyote afanyaye hilo anaitwa *'Mushrik'* na tendo la kumwita hivyo Mungu huitwa *'shirk'*. Kwa hivyo, mwongofu aliyetoka Uislamu kuingia Ukristo amefanya dhambi *'shirk'* ambayo haina masamaha, isipokuwa huadhibiwa kwa adhabu ya milele na mateso makali kuanzia hapa hapa duniani sasa hivi.

Pengine njia iliyo dhahiri kudhihirisha tabia halisi ya Allah inapatikana katika imani ya Kiislamu ya 'kuchaguliwa'.

## *6.2 Imani ya Kuchaguliwa*

Maana ya 'kuchaguliwa' kwa mujibu wa imani ya Kiislamu imewapa waumini wengi wa Kiislamu zaidi ya homa ya kuumwa kichwa. Pale Biblia inaposema juu ya 'kuchaguliwa' au 'kuteuliwa' haina maana ya hatima isiyojulikana, bali

inazungumzia matukio kwa mujibu wanavyomfahamu Mungu kama unavyojulikana (1Petro 1:2; Warumi 8:29) kwa sababu Mungu anajua ya kwamba ni lazima tutatubu na kumgeukia yeye kwa ajili ya kupata wokovu, yeye ndiye hututeua au kutuchagua sisi na “kutufananisha na Mwana wake”. Mtazamo wa Kiislamu ni tofauti kabisa. Katika Uislamu kinachomaanishwa ni kwamba kuchaguliwa (au kuteuliwa) ni Mungu anavyotekeleza mamlaka na utashi wake:

*“Hakuna litakalotusibu isipokuwa lile Allah alilotuandikia” (Surah 9:51).*

Hili lingekuwa jema, kama Allah angekuwa Mungu wa upendo anaye tutakia mema tu. Lakini halionekani kuwa liko namna hiyo.

*“Hakika huu ni ukumbusho: Anayetaka atashika njia ya kwenda kwa mola wake. Wala hamuwezi kutaka asipotaka mwenyezi Mungu…(Surah ya 76:29-30).*

Maneno ‘kama Akipenda ... au wale Awatakao....’ au ‘kama Apendavyo’ yanatokea mara kwa mara katika Kurani.

*“Allah humwacha kupotea amtakaye na humwongoza anayempenda ...” (Surah 14:4) soma pia katika Surah 5:20; 4:88; 32:13.*

Kwa hivyo kila Mwislamu yumo moja kwa moja ‘katika huruma’ ya Allah na atavuna kile alicho mchagulia. Siyo ajabu basi, kwamba kila mdomo wa Mwislamu hutamka maneno haya “insha-Allah” kila wakati.

Mojawapo ya kifungu cha maandiko kinacho fadhaisha sana kuhusu suala hili ni kile kisemacho:

*“Laiti kama Allah angependa, angewafanyeni nyote kuwa kabila moja (au waumini wa dini moja). Lakini humwacha apotee yule amtakaye na humwongoza asipotee yule amtakaye, lakini ni hakika kila mmoja ataitwa kuhukumiwa kwa makosa yake”. (Surah ya 16:93)*

Endapo utaambiwa juu ya tafsiri ambayo inasomeka hivi: Allah “huwaachia kupotea” badala ya “kuwaongoza kupotea” hiyo ni kupotosha maana hasa inayotakiwa, ambayo ni jaribio la kukwepa kuaibishwa kwa andiko hili.

Je, Muhammad angeitafsiri vipi imani hii? Hebu tuiulize Hadith:

*“Nabii mtakatifu alisema hivi: Allah alimuumba Adam. Alipomaliza akamgusa bega la kulia na kutoa kabila la watu weupe wanaofanana na mbegu, na kisha aligusa bega lake la kushoto na kutoa kabila la watu weusi wanaofanana na mkaa. Halafu akawaambia wale waliokuwa upande wake wa kulia: Elekeeni paradiso, na sijali. Akawaambia wale waliokuwa upande wake wa bega la kushoto: Elekeeni jehanam, na sijali.” (Mishkat 3 uk 117)*



Muhammad alitamka jambo fulani ambalo linastahili kumtia wasi wasi mkubwa kila Mwislamu. Siku moja Muhammad aliulizwa hivi na mwenzake:

*"Oh, Nabii wa Allah ! Mimi nakuamini wewe na kile ulichokuja nacho (imani katika Allah na Kurani). Je, bado unatuogopa?"*

Jibu la Muhammad lilikuwa:

*"Ndiyo! Mioyo (ya binadamu) iko kati kati ya vidole vya Allah. Huibadilisha kadiri apendavyo." (Mishkat, 3. uk. 111).*

Hata Muhammad alikuwa hana uhakika wa maisha yake ya milele:

*Kwa kweli Allah mwenye nguvu na utukufu aliushika mmoja kwa mkono wake wa kulia na mwingine kwa mkono wake mwingine na kusema: "Huu ni kwa ajili hii na huu ni kwa ajili ya hii, na sijali. Sijui niko mkono upi kati ya (mikono) hiyo miwili" (Mishkat 3 uk 118).*

Kwa kweli ingependeza kama hili lingefafanuliwa kwa uwazi zaidi, lakini ni hakika maana yake ilikuwa hakuna Mwislamu yeyote, pamoja na nabii wa Uislamu, anayeweza kufahamu Allah amepanga kumfanyia nini. Naam! Yawezekana Allah alimpangia kufanya uzinzi:

*"Mtume wa Allah alisema: 'kwa kweli amewachagulia waana wa Adam (yaani binadamu) kila mmoja fungu lake la uzinzi. Nalo litamshinda, bila ya shaka." (Mishkat 3, uk. 103)*

Hili linathibitishwa na Hadidthi nyinine:

*"Kwa hakika Allah amekwisha kuandaa fungu la zinaa kwa kila mwanadamu. Hakuna njia ya kulitoroka !" (Sahih Muslim 4, uk 1396)*

Yote haya msingi wake unatokana na imani potofu kwamba binadamu hana hiyari. Mwenyezi Mungu anayetawala hamruhusu binadamu kuchagua kati ya jema na baya.

Hadithi nyingine ya Kiislamu iko juu ya mstari huo huo:

*"Kulitokea ubishi kati ya Adam na Musa. Musa alimwambia Adam: Wewe ni Baba yetu. Ulitupa madhara na kusababisha tufukuzwe kutoka paradiso. Adam alimjibu Musa: Wewe ni Musa, Allah alikuchagua wewe na kuandika kwa mkono wake mwenyewe Kitabu kile kwa ajili yako. Licha ya hayo, unanilaumu kwa tendo ambalo Allah alinipangia miaka arubaini kabla hajaniumba." (Sahih Muslim 4, uk. 1307).*

Hebu tufunge mada hii kwa kauli moja ya mwisho.

*"Nabii mtakatifu alisema: Ujaposikia habari kuhusu mlima kwamba umejihamisha wenyewe kutoka mahali pake, yasadiki maneno hayo. Lakini unaposikia kwamba mtu amebadili tabia yake, usiamini kabisa. Atarudia tabia ile ile aliyoumbwa nayo." (Mishkat 3, uk. 121)*

Yote haya ni mambo ya kusikitisha sana na yaliyo kinyume kabisa na ma-

fundisho ya Biblia yasemayo:

> *Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya." (2 Wakorintho 5:17)*

Tunapoichunguza imani hii ya ajabu kuhusu "kuchaguliwa" iliyomo katika Uislamu, hatunabudi kuzingatia kwamba pengine hakuna Mwislamu anayeifahamu. Endapo utaigusa mada hii, unaweza kuambiwa mambo ya ajabu kama ulivyo mfano huu: "Simba amechaguliwa kula nyama, na punda milia amechaguliwa ale nyasi au majani ya miti tu. Hivyo hivyo, Allah ameumba utaratibu unaomwekea kila kiumbe mipaka kwa njia hii au nyingine.

Sisi tunaona imani hii ni ya kufadhaisha sana. Lakini hata hivyo, inatupa sisi bahati ya kutupatia zana ya uinjilisti. Tunapowafahamu Waislamu kwa kiasi cha kutosha tunaweza kuwauliza kama wanaamini juu ya uhuru wa binadamu. Kama ilivyo kawaida, watathibitisha kulijua hilo. Basi hapo unaweza kusema: "Lakini ukiwa kama Mwislamu, ni lazima ukubali imani ya *'taqdir'* (kama inavyofahamika kwa Kiarabu), na kushirikiana nao kama ulivyojifunza. Huenda wataona karaha kwa hilo, hasa pale unaposhirikiana nao kuwafafanulia maana ya ki-Biblia, lakini ni hakika itakuwa hapanabudi wafikiri kwa upya imani zao, kwani hakuna anayependa kuishi katika hali ya kutokuwa na uhakika kama hivi!

### *6.3 Dhambi na Hukumu katika Uislamu na Biblia*

Hii ni hoja nyingine ambayo tunaweza kuitumia katika uinjilisti. Wayahudi, Wakristo na Waislamu, wote huamini kwamba Siku ya Hukumu inakuja.

Hebu kwanza tuhakikishe kwamba tunayafahamu mafundisho ya Biblia: Biblia hufundisha kwamba dhambi, haijalishi imo katika hali ya namna gani, inatutenga na Mungu na inastahili kutufanya tupewe adhabu ya kifo, kwa sababu dhambi, kwa kiini chake, ni uasi dhidi ya Mungu na mapenzi Yake, sheria na utaratibu wake.

Lakini Mungu ametupatia njia ya ukombozi, ya upatanisho na Yeye. Dhambi haiwezi kulipiwa kwa 'tendo jema' fulani. Matendo mema yanatazamiwa kutoka kwetu kwa vyovyote vile ! Lakini Mungu ametupatia njia 'badala'. Dhambi hainabudi kushughulikiwa, kwa sababu iko moja kwa moja dhidi ya asili ya utakatifu wa Mungu. Hii ina maana kwamba, mtu awe mwanaume au mwanamke ikiwa ana dhambi hawezi kumkaribia Mungu hata milele na milele. Kwa hivyo Mungu amekubali kwamba dhambi hii ilipiwe na mtu mwingine asiye itenda. Katika Agano la Kale (Walawi 16:21- 22) ilikuwa ni kafara za wanyama (mbuzi wa kafara) ambaye alitwishwa mzigo wa dhambi (kwa kufikirika) na hatimaye walichinjwa. Wakati Bwana Wetu Yesu alipomjia Yohana Mbatizaji kule kwenye mto wa Yordani (neno Yordani maana yake ni kifo) ili abatizwe,

Yohana alionyesha mshangao kwa kusema: “Tazama! Huyu ni mwana kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!” (Yohana 1:29)

*Dhambi ndio sisi tulivyo: uwaasi dhidi ya mungu*
*Dhambi ndio vile tufanyavyo: tunavunja sheria za mungu mara kwa mara.*

Zingatia vyema kwamba hapa kinachotajwa ni kuhusu “dhambi” – moja – siyo “madhambi” – dhambi nyingi. Dhambi kwa wingi ni matendo maovu ya mtu yanayopingana na mapenzi ya Mungu na sheria zake. **Dhambi kwa umoja wake, au asili yake ni kanuni kuu inayotumiwa na Shetani katika kutawala wanadamu.** “Mwana – kondoo” alitolewa na Mungu maalum ili kuondoa kabisa asili ya dhambi (na kwa njia hii, dhambi za dunia nzima), yaani kutoka kila mwanadamu.



Kuna sharti moja tu, kwamba kila mtu binafsi atakaye dhambi yake iondolewe, naye awe tayari kumkiri Yesu Kristo kama Bwana wake. Kumkataa Yesu kama Mwokozi na Bwana maana yake ni kukataa msamaha wa Mungu unaotolewa kwa njia Yake Yesu. Ni sawa na kumwambia Mungu: “Mimi ninaweza kujitegemea mwenyewe”. Mimi naweza kufanya mwenyewe, ninao wema wa kutosha kustahili kwenda mbinguni, au, nataka kuishi maisha yangu bila wewe.

Wale wote, ambao aidha bila kujua au kwa ufidhuli hawapendi kuutumia ukarimu wa Mungu wa msamaha, wanangoja hukumu ya Mungu ya siku ya mwisho, siku ambayo walio hai na wafu watakapo hukumiwa kila mmoja kwa aliyotenda (Ufunuo 20:11-15).

Ni wale tu ambao majina yao yataonekana ‘yameandikwa katika Kitabu cha Uzima’ hawataadhibiwa na kutupwa katika jehanam (mahali pa kutengwa na Mungu milele na milele). Dakika ile ile mtu anapoomba kwa dhati msamaha wa Mungu na kuamini kwamba Yesu alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zake,

ataokoka na jina lake 'litaandikwa' katika Kitabu cha Uzima. Ungamo la kweli linajumuisha mtu kuungama dhambi zake akiwa na nia thabiti ya kuzikimbia kabisa na kumfuata Yesu Kristo. Zaidi ya hayo, mara kwa mara, majivuno, choyo, wivu, na kadhalika, humnasa muumini. Lakini tunaweza kukaa wasafi kwa neema ya Mungu.
*"Tukiziungama dhambi zetu Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu zote na kutusafisha na udhalimu wote"( 1Yohana 1:9).*

**Yote hayo ni tofauti katika Uislamu.** Mwislamu anatakiwa kutii maelfu ya sheria zinazohusu kila aina ya maisha. Ni dhahiri kuwa anazivunja mara nyingi, kwa kuzingatia ule msururu usio na mwisho wa sheria za 'fanya' hili na 'usifanye" lile. Hapana shaka pia, kwamba idadi kubwa ya Waislamu ni watu wakweli wanaojaribu kwa bidii kutii sheria hizi, lakini bado wanashindwa.
Kama unavyoona, Waislamu wana tatizo kubwa la msingi, la uelewa mbaya wa dhambi. Kwa Waislamu, kuna dhambi moja tu iliyo kubwa, yaani 'shirk', tendo la kudai kwamba Allah ana mwenza, (sanamu ya aina yoyote, au 'mungu mwingine' – kama vile sisi tufanyavyo machoni pao, tunapomtambua Yesu kama Mungu). Kufanya hivyo ni sawa na kuukana Uislamu. Uislamu umezipanga dhambi zote nyingine katika madaraja (gredi) ya dhambi kubwa, dhambi kubwa kidogo; na umetoa maelezo nini la kufanya juu ya dhambi hizo. Baadhi yake, zinaweza kupuuzwa tu. Nyingine zinahitaji tu kufutika mtu afanyapo matendo mema, na nyingine ni lazima mtu aombe msamaha. Kuhusu zile 'dhambi kubwa' ni lazima mtu atubu. Hakuna adhabu iliyotajwa kufuatana na ukubwa wa dhambi. Ni vigumu kabisa kwa mtu kutazamia Mwislamu kukubaliana na tathmini hii ya dhambi yenye asili ya ubinadamu.

> *".... Mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi Maana sijui nifanyalo; kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi, bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Ni ile dhambi ikaayo ndani yangu." (Warumi, 7:14-20)*

Maneno hayo hayakuandikwa na Mkristo dhaifu, bali ni ya mtu aliyefahamu kabisa uzito wa dhambi na matokeo yake. Lakini vile vile alimfahamu Bwana. Ni kutokana na kufahamu utakatifu na usafi wa Mungu tu ndiko kulimwezesha kugundua ubaya wake. Kabla hajawa Mkristo, mtu huyu alikuwa mtu wa dini kweli kweli. Alikuwa Paulo aliyeandika:

> *"… Mtu wa taifa la Israeli, wa kabila la Benjamini, Mwebrania wa Wae-*

*brania, kwa habari ya kushika Torati, ni Farisaya... kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia." (Wafilipi 3:5- 6)*

**Kutambua utukufu wa Mungu kunatufanya sisi tufahamu uzito na ubaya wa dhambi na hali Yetu ya kuwa wenye dhambi.**

Kwa kawaida, Waislamu wana uelewa mbaya wa Mungu, Dhambi na Upatanisho. (Pia soma maelezo kuhusu uinjilisti katika sura ya nane). Kwa sababu hawaelewi kabisa maana ya dhambi, wanaona haina uzito wowote. Kutokana na hayo, hawaelewi hali halisi ya binadamu, ambaye wanaamini anaweza kumridhisha Mungu kwa kufanya matendo yanayofidia dhambi. Hilo nalo linatokana na kuto kumfahamu Mungu, ambaye wanafikiri anaweza kusamehe dhambi pasipo kuishughulikia na kuiondoa, hali isiyokubaliana kamwe na utakatifu Wake.

Wakati tunapomshirikisha Injili Mwislamu kwa njia ya kawaida, mara nyingi atashtuka na kukataa: "Mimi si mwenye dhambi! Ninyi Wakristo ndio mnaojaribu kuwafanya watu wajisikie kuwa na dhambi mbaya. Lakini Allah ni mwenye rehema, huruma na msamaha. Nami ni Mwislamu halisi, nasali mara tano kila siku, nafunga mwezi mzima wa Ramadhan, na natoa zaka nk…"

Mfano mmoja unaokuja akilini ni:

> *"Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja Farisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule Farisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake: Ee, Mungu, nakushukuru kwa kuwa mimi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wazinzi, wala kama huyu mtoza ushsuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma; hutoa zaka katika mapato yangu yote. Lakini yule mtoza ushuru alisimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipiga-piga kifua akisema, Ee, Mungu, uniwie radhi mimi mwenye dhambi." (Luka 18:10 -13)*

Kristo alitoa kauli thabiti kama ifuatavyo:

> *"Nawaambia, huyu alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule; kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa, naye ajidhiliye atakwezwa." (Luka 18:14)*

Tofauti ilikuwa kwamba yule Farisayo alijiamini sana na kujidai kwa matendo yake aliyotenda na ambayo angeendelea kuyatenda; wakati yule mwenye

dhambi alimtegemea Mungu na neema yake pekee. Yule Farisayo alikuwa na imani potofu juu ya Mungu, na yeye mwenyewe, na dhambi.

Tukiwa tumekwishachunguza mambo hayo ya msingi, hebu tuangalie sasa Mwislamu anayo matazamio gani juu ya hukumu na maisha ya milele.

### *6.4 Maisha Baada ya Kifo katika Uislamu*

Kwa mujibu wa Waislamu, jambo la kwanza ni "adhabu ya kaburini" wakati wa kufa.

> *"Macho yanang'olewa, mishipa inaondoshwa, uti wa mgongo unasagwa na mwili mzima huwekwa katika mateso makali ambayo hakuna binadamu anayeweza kuelezea. Kama kuna jeraha mwilini, mwili mzima husikia maumivu. Hebu fikiria, hali ya mwili ilivyo, wakati viungo vyote vya mwili vinapokuwa vinanyofolewa kimoja baada ya kingine. Hii ndiyo saa ya mabadiliko kwa binadamu kutoka hatua moja kuingia hatua nyingine, kutoka maisha ya mwili wenye nyama kwenda maisha ya kiroho." (Mishkat IV, uk 83)*

Mahali pengine tunasoma:

> *"Muumini, ambaye anafariki, anasikia maumivu katika kila mshipa mmoja. Wakati ule anapofariki, Shetani, adui wa Allah, anakuwa yupo karibu sana na yule mtu aliye kifoni." ("Kunatokea nini Baada ya Kifo" kitabu kilichoandikwa na Ahmed Saeed Dehlwi, uk. 55)*


Kuhusu mateso ndani ya kaburi tunasoma pia katika kitabu hicho hicho kama ifuatavyo:

> *"Kwanza kaburi linajipunguza kuwa finyu ili kubana (maiti) hadi mifupa ya kifua ivunjike na kutoboana Pili, moto huwashwa ndani ya kaburi lake. Tatu, nyoka anatumwa ili kumdhibiti nguvu. Sura ya nyoka huyo macho yake ni kama mpira wa moto……na nyoka huyo anasema: 'Nimepewa mamlaka juu yako na Bwana wangu nikuume hadi jua litakapo chomoza kama adhabu ya kukosa sala za alfajiri … tena nikuume hadi alasiri kwa kukosa sala ya adhuhuri… na kadhalika Marehemu ataendelea kupata mateso hayo kwa mfululizo hadi siku ya Hukumu".*

Hiyo ndiyo adhabu ya mtu ambaye amekosa kuhudhuria sala. Nani hakukosa sala mara fulani? Katika Uislamu, kila Mwislamu lazima aseme sala mara tano kwa saa maalum kila siku.

Katika kitabu *"Yanayotokea Baada ya Kifo"* vimetajwa visababishi vya adhabu

mbali mbali ndani ya kaburi kama:




- Uzembe wakati wa kukojoa.
- Kusema sala zilizotajwa kana kwamba ni kujitua mzigo au kuziona sala hizi kama udhia mtupu.
- Watu ambao matendo yao yalikuwa tofauti na maneno yao, midomo yao itachanwa pembeni.
- Misumari inapigiliwa kwenye macho na masikioya wale waliojaribu kuona na kusikia mambo yasiyoruhusiwa.
- Mama aliyekataa kunyonyesha mtoto wake matiti yake yataumwa na nyoka.
- Waliofungua mapema wakati wa kufunga (Ramadhani) wanaangikwa kichwa chini na kulazimishwa kulamba matope.
- Wachezaji wa mchezo wa sataranji (chess) watachapwa kwa mjeledi wa moto.

Mwisho wa mateso hayo yote ni Siku ya Ufufuo ambayo hufuatiwa na Siku ya Hukumu. Masimulizi ya Hadith kuhusu matukio ya baada ya kifo, nayo vile vile yanatisha.

> *“Allah atasema, hebu watenge wale watakaopelekwa kwenye moto (jehanam) Naye (Adam) atauliza: Ni wangapi, hao watakaopelekwa motoni? Naye (Allah) atasema: 999 kati ya kila 1000!”*

### *6.5 Wokovu katika Uislamu*

Waislamu huamini juu ya kitabu cha Matendo, na mizani ambayo ndiyo itakayotumiwa kupima matendo mema ya mtu dhidi ya matendo yake mabaya. Daraja jembamba kama upanga litawekwa juu ya jehanam kwenda Paradiso ambalo wote lazima walipite, ndilo hufanya hatima ya binadamu kuwa jambo nyeti kweli kweli. Ni wale wanaostahili tu ndio watakaofika pale kwenye “Bustani” inayotamaniwa na kila mtu, Paradiso.



Hayo yote ni maajabu kwetu kwa sababu kamwe hayalingani na Biblia. Je, yanaweza kuwa na ukweli? Au, ni kwamba yameandikwa kwa ajili ya kuwatisha Waislamu wasiache Uislamu wao wala kuishi maisha ya kutojali majukumu ya dini yao?

Tunaambiwa (katika kitabu cha UISLAMU kilichotungwa na Ismail R. Faruqi, 1979, uk 9):

> *"Kwa mtazamo wa Uislamu, binadamu 'hawakuanguka' zaidi ya vile walivyo 'okolewa'. Kwa kuwa 'hawakuanguka' hawana haja ya mwokozi. Lakini kwa kuwa pia 'hawakuokolewa' wanahitaji kufanya matendo mema – na hawanabudi kuyafanya ki-maadili – ambalo ndilo jambo pekee litakalowapatia huo 'wokovu' unaotakiwa.*
>
> *Kwa kweli 'wokovu' si neno muafaka, kwa sababu, ili kuhitaji 'wokovu' ni lazima mtu awe katika janga kubwa ambalo hana matumaini yoyote ya kujinusuru nalo (maelezo ya ajabu sana). Lakini, wanaume na wanawake hawamo katika janga kama hilo. Si kwamba binadamu ni wapungufu wa mamlaka ya maadili. Sio vibweka dhaifu wasiojiweza katika mema na mabaya. Binadamu wanajiweza katika yote. Binadamu 'hujiokoa' wenyewe kwa matendo na kazi zao, ndiyo fahari na utukufu wao."*

**Wokovu kama sisi tunavyoufahamu kutoka Biblia haufahamiki kamwe kwa Waislamu.**

Kukiri imani ya Kiislamu na kutenda yale yaliyoelekezwa katika nguzo tano pamoja na matendo mema mengi kunawapa Waislamu matumaini yasiyo na maana. Bila shaka kila Mwislamu anamtegemea Allah ili amhurumie. Ni kweli, Mungu ni mwenye rehema. Lakini rehema yake imedhihirishwa kwenye msalaba ambao kila Mwislamu anaukataa. Kutokana na msingi wa Neno la Mungu, yaani Biblia, hakuna Mwislamu hata mmoja atakayefika mbinguni asipomjia Yesu ili apate wokovu. Ndiyo sababu ni wajibu mkubwa wa kila Mkristo kuwashuhudia Waislamu, ambao hawajui wala hawafahamu Injili, kwa sababu Uislamu umewafumba akili wasipate kuijua.

**➔ *Tafadhali sasa soma na kujibu maswali ya kutafakari kwa masomo ya sura ya 5 na sura ya 6.***

# 7. Pingamizi za Waislamu Dhidi ya Imani ya Kikristo

Tayari tumeshagundua Kurani inafundisha kwamba Biblia ni neno la Mungu. Haikosi Muhammad lazima aliamini kuwa Uislamu ni muendelezo wa 'dini za kitabu' zilizopo, yaani dini ya Kiyahudi na Ukristo. Muhammad aliyapitia mafundisho ya Agano la Kale kuhusu Yesu, Mwana wa Mungu ndani ya Utatu, na kifo chake msalabani badala ya kifo cha binadamu, na kuyaona kama ni kufuru kubwa. Je, alidhani tu kwamba hayo hayakuwa mafunuo ya kweli ya Mungu, bali yameongezewa na binadamu, ni uheresi? Au, alishambulia kwa makusudi maandiko makuu ya Biblia kama inavyoonyeshwa ndani ya Kurani kama hivi:

> *"… Wakristo wanasema Masihi ni mwana wa mwenyezi Mungu. Haya ndiyo wasemayo kwa vinywa vyao. Wanaiga maneno ya wale waliokufuru kabla yao. Mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gain hawa?" (Sura 9:30)*

Haya ni maneno mazito kweli kweli, na ndiyo yanayomfanya kila Mwislamu wa kweli kujenga chuki kubwa dhidi ya imani ya Kikristo.

Waislamu wanaamini kwamba Biblia yetu siyo kama ile ya asili, ambayo ni Torati ya Ibrahim (Sheria), Zaburi za Daudi na Injil (Injili) ya nabii Isa (Yesu). Wanashikilia kwa nguvu kwamba Wayahudi na Wakristo wameifuja Biblia na kubadilisha ile ya mwanzo, na kuongezea mafundisho ya uungu na uana wa Yesu, wakaongeza na maudhui ya utatu, na vile vile wakaongeza maudhui ya kusulibishwa sambamba na imani ya upatanisho. Maandiko yao mengi ya kupinga Kristo, ambayo huyaeneza kuanzia misikitini, Vituo vya Uenezi wa Uislamu na maduka yao ya vitabu, yanashambulia kwa ukali misingi ya imani yetu, na kutuchagiza ati tuangukie na kukubali dini pekee iliyo kweli, Uislamu.

> "*anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa)" (Sura 3:85).*

Je, sisi yatupasa tujibu kwa jinsi gani? Biblia ina njia nzuri ya kutoa majibu hayo.

***"Bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. Muwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu. Lakini kwa upole na heshima." (1Petro 3:15).***

Hebu sasa tujifunze masomo machache sana ya muhimu kutokana na maandiko hayo:

- **Ubwana wa Kristo:** Lolote tusemalo, kwa njia yoyote ya tabia, tunalifanya akiwapo, na chini ya Ubwana wa Kristo!
- **Kuwa tayari:** Hatubishani juu ya hoja ambazo hatuzijui au kuzielewa. Tunachotafuta ni kupata habari sahihi kisha kutoa majibu ya busara na hekima yanayoridhisha.
  Tena, hilo haliwahusu wachungaji wakisimama kwenye mimbari, lakini linawahusu Wakristo wote DAIMA, wanapokuwa mahali popote.
- **Tayari sisi tunalo jibu:** Mara nyingi, Wakristo wanapowashirikisha Injili watu wa tamaduni au dini nyingine, hujibu maswali ambayo wameyabuni. Kwa kweli majibu hayo hayana maana yoyote, kwa sababu Waislamu hufikiri na kutafakari kwa njia zilizo tofauti kabisa. Injili hainabudi kuhubiriwa kwa njia zinazolingana ('aha') na akili za Waislamu.
- **Kagua msimamo wako, na kuhubiri matumaini:** Tunapozungumza na Waislamu, hatuji mbele zao kama 'wapiga vita' bali kama washuhuda. Hatupigani, hatuwasumbui au kuwalazimisha watusikilize! Upendo wa Kristo ndio unaotuongoza. Hatuwaburuzi bali tunashirikiana nao, tukifafanua hoja moja baada ya nyingine juu ya kile wanachohitaji kufahamu na kuelewa.
- **Tufanye hivyo kwa upole na heshima:** Usithubutu hata kidogo kutumia habari ulizojifunza katika mwongozo wa kitabu hiki kama silaha dhidi ya Waislamu. Habari hizo ni zana za kukusaidia wewe ili uweze kuwadhihirishia kwa upole na ukarimu tofauti ya maisha yaliyo na uhakika wa upendo wa Mungu kwa njia ya kifo cha Kristo, kinyume na matarajio ya Uislamu yasiyo na uhakika kwa wafuasi wake.

Tafadhali zingatia sana kanuni hii:

*Mwislamu ataelewa yale tunayosema kulingana na jinsi tunavyomwelewa yeye.*

Ni nadra sana 'kuhubiri' kwa Waislamu kukaweza kufanikisha kupata matokeo mazuri. Na, kuwakaribisha Waislamu kuhudhuria mikutano ya kanisa kunaweza kuleta madhara makubwa zaidi ya faida! Inatupasa tukae chini pamoja nao, tuwasikilize, tuwaulize, tuwaangalie ili tupate kuwaelewa vizuri. Ni lazima kwanza tujifunze kutoka kwao kabla ya sisi kuweza kuwafundisha. Siyo tu kuwatupishia aya za Biblia kana kwamba aya hizo zina uchawi fulani ndani yake wa kuwafanya waelewe. Neno la Mungu halinabudi kueleweka kwanza ! "Imani huja baada ya kusikia ujumbe (Warumi 10:7)" lakini kwa hakika hilo halinabudi lisababishe kuelewa. Jambo hilo huchukua muda, mara nyingi, muda

mrefu zaidi. Matokeo mazuri ya papo kwa papo ni adimu sana kupatikana katika kazi ya kuhubiri Injili kwa Waislamu, isipokuwa kama yakipatikana, labda mhusika alishakuwa na uzoefu mkubwa juu ya Ukristo, au imani yake ya Uislamu ilikuwa dhaifu. Kumpenda Mwislamu maana yake ni kumjali kiasi cha kujiunganisha naye kabisa katika maisha yake!

> *"Vivyo hivyo, nasi tukiwatumaini kwa upendo mwingi, tuliona furaha kuwapa, si Injili ya Mungu tu, bali na roho zetu pia, kwa sababu mmekuwa wapendwa wetu"(1Wathesalonike 2:8).*

*Jinsi ya kujibu pingamizi za Waislamu*

Kwa kuwa Biblia na Kurani ni vitabu vinavyopingana, haiwezekani vitabu hivyo viwili viwe vimetoka katika chanzo kimoja, ni lazima kimoja wapo, au vyote viwili vimevurugwa na binadamu na kubadilishwa.

Kwa hivyo ni kazi yetu sasa kukaa pamoja na Waislamu ili tukubaliane nao juu ya ukweli kwa pamoja. Hakuna haja ya kushikilia msisitizo wa kwamba sisi ndio tuko sahihi kwa sababu Biblia ni ukweli, wakati huo huo Waislamu nao wanashikilia kwamba Kurani ina uvuvio, na ndicho kitabu cha kweli. Tunahitaji "kuyapima matumaini yetu". Kwa nini tunaamini kuwa Biblia ndiyo iliyo na ukweli? Na yule mtu mwingine, kwa nini anaamini kwamba Kurani ndiyo kitabu cha kweli?

*Basi jiandae kujibu hoja hizi kutoka kwa Waislamu.*

## *7.1 "Biblia imebadilishwa na kuchafuliwa !"*

Sasa tumefahamu ya kwamba Waislamu wote wanapaswa kuikubali Biblia na Kurani. Hakuna mtu yeyote anayeweza kudai kuwa yeye ni Mwislamu bila ya kukubali kuwa Biblia ni Neno la Mungu, kwa vile jambo hilo limeandikwa wazi wazi katika ('Iman',) imani ya Kiislamu:

> *"Semeni: Tunamwamini Allah, na yale tuliyoteremshiwa, yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na is-haqa ya Yaqubu na kizazi chake. Na waliopewa Musa na Isa na pia yale waliopewa nanabii wengine kutoka kwa mola wao. hatutofautishi baina ya yote katika hao." (Surah 2:136)*
>
> *Enyi mlioamini! Mwaminini mwenyezi Mungu na mtume wake na kitabu alicholiteremsha juu ya mtume wake, na vitabu alivyoviteremsha zamani. Na mwenye kumkanusha mwenyezi Mungu na malaika wake na vitabu*

*vyake na mitume wake na siku ya mwisho, basi bila shaka amepotea upotofu ulio mbali na haki (Surah 4:136).*

*"Tunayaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu. Mungu wetu na Mungu wenu ni mmoja." (Surah 29:46)*

Bila shaka, Waislamu hawaamini Biblia yetu. Wanasema kwamba Biblia wanayoiamini ni ile yenyewe ya "ya kwanza" ambayo baadaye ilichafuliwa na Wayahudi na Wakristo. Kwao, ile Biblia ya 'asili' haipo tena. Huu ni upuuzi mtupu, kwani hati zote zilizoandikwa kwa mkono ni za zamani sana, za muda mrefu hata kabla Muhammad hajazaliwa, au kabla Kurani haijaandikwa. Kurani inathibitisha jambo hilo.

*"Enyi, mliopewa kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na mnaficha ukweli na hali mnajua?" (Surah 3:71)*

Muhammad aliwashitaki "Watu wa Kitabu" (Wayahudi na Wakristo) kuwa wamepotosha maana ya Kitabu kwa ndimi zao (lakini siyo kwa kalamu!).

*"Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa kusoma kitabu ili mpate kufikiri maneno yao hayo kuwa ni yakitabu cha mwenyezi Mungu. Wala si ya kitabu cha mwenyezi Mungu na hali hayakutoka kwa mwenyezi Mungu na hali wanamsingizia mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua kuwa huo ni uwongo." (Surah 3:78)*

Waliwezaje kujua, ilihali hawakuwa na nakala ile ya awali? Kurani inasema walificha ukweli na kusema uwongo kwa kujua wamekwisha kugeuza maandiko ya Kitabu. Hii ingeweza kumaanisha tu kuwa walikifahamu Kitabu chenyewe, kwa sababu walikuwa nacho!

Kwa hivyo, sasa ni juu ya Waislamu kuthibitisha, kwetu na kwao wenyewe, ni kwa jinsi gani na mahali gani Biblia imebadilishwa.

Yafuatayo ni baadhi ya **maswali mazuri** yaliyowafanyaWaislamu kufikiri sana:

- **Kwa nini** mtu yeyote abadilishe Biblia, wakati imeandikwa kwamba wale watakaoongezea maneno yake au kuyapunguza hata neno moja wataadhibiwa milele? (Ufunuo 22:18-19)
- **Kama mtu yeyote** angebadilisha Biblia, basi Wayahudi wote na Wakristo ambao wangegundua mabadiliko hayo wangeweza kuibua pingamizi dhidi ya mabadiliko hayo. Hakuna mtu yeyote ambaye angeweza kubadilisha

kwa mkono wake peke yake Biblia zote au baadhi ya sehemu za Biblia.

- **Lini** Biblia ilipobadilishwa? Kama ni baada ya Muhammad, inawapasa Waislamu wote wafahamu ya kwamba hati zote za Biblia za kuandikwa kwa mkono ni za tarehe ya nyuma sana kabla Muhammad hajazaliwa. Kama ni kabla kwa hakika Kurani ingekuwa na sababu ya kuwashitaki Wayahudi na Wakristo kwa uhalifu huo. Licha ya hayo, Muhammad mwenyewe alitoa wito kwa Biblia kukubaliana na mamlaka ya ujumbe wake.
- **Nani** alibadilisha Biblia? Je, ni Wayahudi, Wakristo, au Wayahudi na Wakristo kwa pamoja?
- **Iko wapi** ile nakala ya kwanza, ili tuweze kuliinganisha na maandishi ya Biblia yetu ya sasa?
- **Anawezaje** Mtu yeyote kuamini kwamba Biblia imebadilishwa, isipokuwa angalau mojawapo ya maswali yetu mengi lingejibiwa vya kuridhisha?

**Licha ya hayo,** Kurani yenyewe inasema wazi wazi, kwamba Torati, Zaburi na Injil zimetoka kwa Allah!
Na Kurani, vile vile inatamka kwamba:
'Hakuna abadilishaye maneno ya (waadiwa) mwenyezi Mungu. " (Surah 6:34; na 10:64).

Inawezekana baadhi ya Waislamu wanaweza kusema Injili ya asili ni ile **"Injili ya Barnaba."** Huu ni ubunifu wa karne ya 14 na kwa hivyo unaweza kuanikwa hadharani kwa urahisi kabisa. (Hapa tunarejea vitabu vyetu vya Kiongozi cha Walimu).

Waislamu, vile vile, wanaweza kubisha, kwamba – kwa mujibu wa Kurani – Yesu ndiye aliyepewa Injili sahihi, na kwamba Injili iliyomo ndani ya Biblia imeandikwa na Mathayo, Marko, Luka na Yohana, kwa hivyo haiwezi kuwa sawa na ile ya asili. Lakini Yesu hakukabidhiwa hata kitabu kimoja cha Injili. Yeye mwenyewe ndiye Habari Njema! Na ni Yeye mwenyewe aliyehamasisha na kukumbusha watumishi wake kuwa wasisahau kuandika Ujumbe!

Waislamu waliopewa mafunzo maalum watajitokeza wakiwa na hoja chungu nzima kuhoji maandiko ya Biblia, au kutoa maandiko kuthibitisha hoja zao. Sisi tunayo maandiko mengine yanayofaa kujibu swali hili. Tuandikie nasi tutafurahi kusaidia!

## 7.2 “Unawezaje Kuamini Miungu Watatu na Kudai ya kwamba Yeye ni mmoja? Hii haileti Maana”

Kurani inaushambulia Utatu kwa maneno haya:

> *“Na kumbukeni Mwenyezi Mungu atakaposema: Ewe, Isa bin Maryamu! Je, wewe uliyewaambia watu, nifanyeni mimi na Mama yangu, kuwa waungu badala ya mwenyezi Mungu?…Enyi watu wa kitabu (yaani Wayahudi au Wakristo) msiivuke mipaka ya dini yenu wala kumsingizia Allah kitu chochote zaidi ya ukweli. Kristo Yesu, mwana wa Mariamu, hakuwa zaidi ya mtume (mtumishi) wa Allah, na Neno Lake ambalo alimjalia juu ya Mariamu na Roho Mtakatifu aliyetoka kwake … Msitamke Utatu. Jiepusheni! Itakuwa vyema kwenu, kwani Allah, Bwana wangu ni mmoja. Utukufu na uwe juu yake (kwa kuwa Yeye ndiye aliyeinuliwa) Hawezi kuwa na mwana.” (Suah 5:116)*
>
> *Wanakufuru, wale wasemao: ‘Allah ni Kristo mwana wa Mariamu’ Oh, Enyi wana wa Israel. Muabuduni Allah Bwana wangu na Bwana wenu”. Yeyote anayemuunganisha Allah na miungu wengine – Allah atamkatalia kuingia ile bustani – paradiso, na makao yake yatakuwa motoni…Wanakufuru …. wale wasemao ‘Allah ni mmoja wa wale watatu katika Utatu …” Surah (5:75-76).*
>
> *“Hakuzaa wala Hakuzaliwa, na wala hakuna kiumbe kinacho fanana na Yeye.” (Surah 112:3-4)*

Yusuf Ali anatoa maoni haya: Haya ni kwa jili ya kukanusha dhana ya Kikristo kichwa cha uungu, “Baba”, “mwanawe wa pekee aliyezaliwa”, na kadha wa kadha”.

Tunaweza kuona wazi kabisa kutokuelewa kwa Muhammad kuhusu Utatu. Yeye alifikiri utatu maana yake ni umoja wa Allah, Mariamu na Yesu, na inamaanishwa kwamba Kristo alizaliwa baada ya tendo la kukutana kimwili kati ya Allah na Mariamu. Siyo jambo la kushangaza sana, kwamba Muhammad aliikataa dhana hiyo. Na sisi vile vile tunaikataa.

Ni jambo la kusisimua, lakini katika Surah ya 19 inabainishwa kwa lugha isiyo wazi kwamba Allah ndiye mwanzilishi wa dhuria ya Mariamu, kwa hiyo kuthibitisha jukumu la “ubaba” wa Mungu, japokuwa ni kwa njia tofauti na tendo la ngono.

> *“Haiwi kwa mwenyezi Mungu kufanya motto; ametakasika. Anapolitaka jambo basi huliambia tu kuwa ; nalo likawa (Surah 19:35)*

**Je, tujibu vipi?**
Sisi tunaposema Mungu ni Utatu, maana yetu ni nini. Jambo hilo haliwezi kueleweka wala kuelezwa au kufikiriwa kama ndiyo maudhui ya umilele au wakati usio na mwisho. Tunaweza kumfahamu Mungu kwa kutambua kile alichofanya na bado anachoendelea kukifanya, na mafunuo juu yake mwenyewe katikaYesu Kristo.

> *“Yeyote aliyeniona mimi amemwona Baba (Yohana 14:9) “Mimi na Baba tu umoja” (Yohana 10:30). “….. mwisho wa siku hizi alisema na sisi katika Mwana ….”(Waebrania 1:2)*

Tunakiri kwamba uana wa Yesu na Utatu wa Mungu ni mambo yanayodokezwa katika Maandiko kuliko kufundishwa. Soma:
Jeremia 23:5- 6; 33:15-16; Isaya 7:14; 9:6; 63:7-10 (neno ‘mwokozi’ ni sawa na “Yeshua” na ni sawa na Yesu!) Tafasiri ya Kumbukumbu ya Torati 6: 4 inasomeka hivi: *Bwana Mungu wetu na Bwana ni wamoja (katika umoja).* Jina lenyewe la Mungu – ‘*Elohim*’ ni la wingi. Kadhalika yanathibitishwa katika Zaburi 110:1 na 2:1-7. Katika Agano Jipya huthibitishwa pia katika mistari kama Mathayo 28:18-19; 2Wakorintho 13:14. na katika aya kadha wa kadha kama kwenye (Ubatizo wa Yesu na Kung’aa kwa Bwana). Kwa hakika Mungu ni mkuu mno, tofauti mno na sisi, kiasi kwamba siyo rahisi kwetu kumwelewa kwa ukamilifu. Lakini inatupasa tuamini yale anayosema juu yake mwenyewe.

### *7.3 “Msimfane Yesu Awe Zaidi ya vile Alivyodai Mwenyewe. Hakuna Popote Alipodai kuwa ni Mwana wa Mungu.”*

Tunasoma hivi katika Kurani:

> *“Wayahudi wanasema Uzeri ni mwana wa mwenyezi Mungu, na Wakristo wansema Masihi ni Mwana wa mwenyezi Mungu. Hayo ndiyo wasemavyo pasi na kuyapima. Wanaiga maneno ya wale waliokufuru kabla yao, mwenyezi Mungu awaangamize. Wanageuzwa namna gano hawa! (Sura 9:30)*

Tunalazimika kutamka hapa, kwamba upembuzi wa Kurani na Waislamu dhidi ya msingi huu wa mafunzo ya Biblia ni dhaifu kabisa.
Kwa upande mwingine, hatunabudi kutilia maanani heshima ya hali ya juu ambayo Yesu (Nabii Isa) aliyopewa ndani ya Kurani.
Kama tulivyoona, Kurani na Waislamu hubeza asili ya uungu wa Kristo. Lakini Biblia inathibitisha jambo hilo kwa maneno ya uhakika kabisa na kutoa ushahidi wote unaohitajika. Kwa kweli litakuwa jambo zuri sana endapo tutasoma

na kuzingatia aya zifuatazo za Kurani:

| | |
|---|---|
| **Alizaliwa na Bikira** | **Surah 19: 20** |
| **Alikuja na ishara zilizotabiriwa** | **Surah 43:63** |
| **Alikuwa mtakatifu asiye na dhambi** | **Surah 19:19** |
| **Alikuwa mfano kwa binadamu wote** | **Surah 19:21; 21:91** |
| **Alikuwa Masihi** | **Surah 4:171** |
| **Aling'ara katika ulimwengu huu na baada ya kuutoka** | **Surah 3:45** |
| **Yeye ni Neno la Mungu (!)** | **Surah 4:171** |
| **Ni roho kutoka kwa Mungu** | **Surah 4:171** |
| **Aliinuliwa kwenda juu mbinguni (ambako ndiko aliko hivi sasa)** | **Surah 4:158** |
| **Aliumba uhai** | **Sura 5:113** |
| **Aliponya wagonjwa** | **Surah 5:113** |
| **Atarudi tena kuhukumu** | **Surah 43:61** |
| **Alifufua wafu** | **Surah 5:113** |

***Haya ni matamko 13 ya kweli kuhusu Yesu Kristo. Je, tunaweza kumfikiria mtu yeyote, aliyewahi kuishi, isipokuwa Eliya, ambaye angeweza kudai kwa kweli kwamba anazo japo sifa 3 kati ya hizo zilizotajwa?***
***Ushahidi huu kutoka Kurani peke yake unathibitisha kuwa Yesu alikuwa zaidi ya nabii, lakini vile vile unampa wazi wazi sifa ya uungu.***

Siyo tu kuwa Agano Jipya hufundisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na ni Mungu, lakini imeandikwa wazi wazi hata katika Agano la Kale katika unabii wa kuja kwake Masihi:

> *"Bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanaume naye atamwita jina lake 'Mungu pamoja nasi" (Isaya 7:14).*
> *"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanaume … naye ataitwa Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani (Isaya 9:6).*

Bwana Yesu alikuwa na asili zote, za Baba yake na Mama yake ndani yake. Sura yake ilikuwa ya binadamu kamili. Alikuwa hanabudi kula, kunywa na

kulala. Alisikia maumivu, aliona huzuni na furaha. Kadhalika alisikia haja ya kuabudu. Lakini ni uungu wake uliomwezesha kuwalisha watu 5000 kwa mikate mitano na samaki wawili, kuponya wagonjwa wa ukoma, vilema, waliopooza na vipofu, kufufua wafu, kutuliza tufani, kusamehe dhambi, kutembea juu ya maji na kufufuka kutoka kwa wafuYeye mwenyewe.

| | | |
|---|---|---|
| **Yohana 14:6** | **Yohana 10:25-33** | **Luka 7:48-50** |
| **Mathayo 14:32-33** | **Yohana 5:21-27** | **2 Wakorintho 4:4** |
| **Wakolosai 1:15-20** | **Mathayo 26:63-64** | **Tito 2:11** |
| **Danieli 7:13-14** | **Tito 2:11** | **Matendo 20:27-28** |
| **Yohana 20:26-29** | **Yohana 1:10-12/** | **Warumi 9:4 -5** |
| **Waebrania 1:1-4.** | | |

***Kutokana na msingi wa aya hizo, jaribu kujibu maswali yafuatayo:***

Jina la ‘Mwana wa Mungu linaonyesha maana gani? Jina hilo linaambatana na mamlaka ya namna gani? Ni lini Bwana Yesu alipoanza kuwa Mwana wa Mungu? Je, jina hili ‘Mwana wa Mungu’ lina maana ya kwamba Yesu ni Mungu? Inaposemwa Yesu ana sura ya mwanadamu, maana yake nini?

## *7.4 “Kitabu chetu Kinatuambia kwambaYesu hakusulibishwa*

Huenda upinzani wenye nguvu kutoka kwa Waislamu ni dhidi ya suala la kifo cha kusulibishwa cha Bwana wetu:

*“Na (kwa ajili) ya kusema kwao: Sisi tumemuua masihi Isa, mwana wa Maryamu, mtume wa Mungu, bali hawakumwua wala hawakumsulubu, bali walibabaishiwa (mtu mwingine wakamdhani nabii Isa). Na kwa hakika wale waliokhitilifiana katika (hakika) hiyo ya kumwua nabii Isa wamo katika shaka nalo (jambo) hili (la kuwa kweli wamemwua nabii Isa), isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumwua.!” (Surah 4:157)*



*“Masihi bin Maryamu si chochote ila ni mtume (tu). Je! Mnaabudu-badala ya mwenyezi Mungu (peke yake) wale ambao kukudhuruni wala kukunufaisheni? (Surah 5:75-76)*

Katika vitabu vingi vya Kiislamu, vipeperushi, majarida, kaseti za video, za zamani na mpya zenye madai kama hayo hutetewa kwa kunukuu aya za Biblia yetu. Waislamu wengine wanasema Yesu aliangikwa tu msalabani lakini hakufa pale, kwa hiyo hakusulibishwa. Alizimia, akateremshwa pale msalabani akiwa amezirai, akahudumiwa na akina mama ndani ya kaburi hata akapata fahamu. Hata wengine husema aliyesulibishwa ni Yuda lakini watu walikosea kumfananisha na Yesu (au Yuda alibadilishwa kufanana na Yesu).
Neno "kusulibiwa" mzizi wake ni neno la Kilatini 'crux' sawa na 'msalaba' na 'ficere'' maana yake ni 'kuning'inizwa' au 'kupigiliwa'. Matokeo yake ni Waislamu penginepo kusema kusulibishwa maana yake ni kwamba mtu aliangikwa tu msalabani, lakini siyo lazima kuangikwa kusababishe kifo cha mtu pale msalabani. Bila shaka, jambo hili ni upuuzi mtupu!

***Daima Msalaba wa Kristo umekuwa Kikwazo kikubwa, na chukizo!***

Tena tungeweza kuwauliza marafiki zetu Waislamu kuyafikiria baadhi ya maswali haya:

- ✝ Nani alisulibishwa – Kama siye Yesu, nani mwingine?
- ✝ Je, Mungu alianzisha (alitunga) uongo kuhusu Yesu?
- ✝ Ni nani wa kuaminika zaidi, mtu aliyeona kwa macho, au mtu anayezungumza miaka 600 baadaye?

*Hebu tujikumbushe:*

> *"Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima, bali sisi tunamhubiri Kristo, aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuuzi, bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu." (1Kor. 1:22-24).*

Katika Wagalatia 5:11 tunasoma juu ya habari ya "chukizo la msalaba". Msalaba ni chukizo lililoje?
Kafara la Yesu Kristo pale msalabani laonyesha kwamba mwanadamu hawezi kabisa kuingia kwenye ufalme wa Mungu kwa wema na nguvu zake tu. Yesu aliliweka hivi: *"Pasipo mimi ninyi hamuwezi kufanya lolote" (Yohana 15:5).*
Paulo naye alikiri: *"Najua ya kuwa ndani yangu … halikai neno jema."* (Warumi 7:18) Kila mtu anamhitaji Yesu ambaye alikuwa dhabihu yetu, ambaye alikufa badala yetu ili kuifungua njia ya kutufikisha mbinguni. Kiburi cha mwanadamu humfanya muasi dhidi ya uamuzi wa Mungu. Binadamu anakwazwa kwamba Mungu hawezi kukubali jitahada anazofanya mwenyewe!

### *7.5 “Siyo Haki kwamba Mtu Mwingine Ateswe kwa Ajili Yangu. Kila Mtu Awajibike kwa Makosa Yake Mwenyewe.”*

Tunasoma hivi katika Waebrania 9:22: *“Pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi.”*
Mstari huu, bila shaka, unamaanisha damu ya kafara. Agano la Kale linafundisha hilo tangu mwanzo hadi mwisho: *“……. Ni hiyo damu iletayo upatanisho…”* (Mambo ya Walawi 17:10) Upatanisho maana yake ni usuluhishi, kurejeshwa kwa mawasiliano yaliyovunjika.
Ili Shetani aweze kubatilisha kabisa wokovu, ni lazima akatae kabisa dhabihu ya Yesu msalabani au aifanye ionekane haikuwa na ulazima. Na hivyo ndivyo Kurani inavyofanya. Kwa kuwa jambo hili ni muhimu sana, hatunabudi tuwaeleze marafiki zetu Waislamu kwa uvumilivu mkubwa juu ya ukweli wa kusulibishwa na kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo.

*Hoja zifuatazo zingeweza kusaidia:*

- ❒ Karibu theluthi nzima ya Injili husimulia habari za juma la mwisho katika maisha ya Yesu na kifo chake! Hakikisha hilo wewe mwenyewe.
- ❒ Dhabihu yaYesu ni jibu la kimantiki kabisa kwa mafundisho ya Agano la Kale. *(Tazama Luka 24:26, 44)*
- ❒ Agano la Kale lilitabiri kifo cha Kristo msalabani katika mistari mingi inayoeleza matukio hayo kinaganaga kabisa.
- ❒ Tuna ushuhuda wa watu walioona kwa macho yao. Kungekuwa na haja gani kwa watu kama hao kutunga hadithi kama hiyo ?
- ❒ Katika wakati wa uhai wake hapa duniani, Kristo alitabiri kifo chake mwenyewe mara nyingi (soma taarifa za Biblia. Kwa hivyo kifo cha Yesu hakikuwa ajali iliyotokea kwa ‘mungu kilema’. Alisema: *“Ndiposa Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu – ili niutwae tena. Hakuna mtu aniondoleaye, bali mimi nautoa mwenyewe.” (Yohana 10:17-18)*
- ❒ Upo ushahidi mwingi wa kihistoria unaokubalika wa kusulibishwa na kifo cha Yesu. (Soma 1Wakorintho 15:12-20)

### *7.6 Hoja nyingine za pingamizi zinazotolewa na Waislamu*

Daima Waislamu watatafuta - tafuta mapungufu haya na yale na kujaribu kuyaweka katika njia yetu, lakini kitakachotusaidia sisi ni kama tunafahamu ni wapi mapungufu yapo, basi tutaweza kupata njia ya kukabiliana na hawa *‘madowah’* (wamisionari wa Kiislamu).

| PINGAMIZI | BUSARA | JIBU |
|---|---|---|
| **1.Yesu hakuwa nabii wa ulimwengu, bali ali-tumwa kwa Wayahudi tu** | Yesu alisema: *"Nilitumwa tu kwa kondoo wa ali-opotea wa Israeli."* **(Mathayo 15:24)** | Yesu alifundisha wazi *"Mimi ni nuru ya ulim-wengu .."***Yoh. 8:12**<br>Ni dhahiri 'ulimwengu ni mkubwa zaidi ya 'Israeli!' 1 Yoh 2:2 |
| **2.Muhammad alitabiriwa ndani ya Biblia** | Katika Kurani Yesu anas-ingiziwa alisema: *"Kweli mimi ni mtumishi wenu .. anayewapa habari njema za mtumishi atakayekuja baada yangu ambaye jina lake ataitwa Ahmad"* **(S. 61:6)** Waislamu hushikilia hili linathibitisha **Nya. 18:15** na **Yoh 14:16-17** *"Nitamwomba Baba ,naye atawapeni Mshauri mwingine mtakayekuwa naye milele."* | Wanaposema nabii aliyeta-jwa ni Muhammad, Waislamu ni lazima Waku-bali kwamba:<br>-Yesu ni Mungu.<br>*"Kama nisipoondoka huyo Mshauri hatakuja kwenu, lakini nikiondoka (Yesu) nitamtuma kwenu"* **(Yohana 14:17).**<br>-Muhammad ni mzima hajafa. Hii imaanisha:Mtu aliyekufa anawezaje kukaa na waumini siku zote? **(Yoh. 14:16).**<br>Hatuna budi kuzingatia, kwamba wanafunzi walishamfahamu mshauri mwenyewe, wakati Muhammad alikuja miaka 600 baadaye. |
| **3. Sisi Waislamu ni Wakristo bora zaidi ya wengi wenu, kwa sababu sote tumetahiriwa** | Waislamu hudai kwamba mtu hawezi kukubaliwa mbele za Mungu mpaka awe ametahiriwa kama Abraham na wazawa wake wote baada yake. | Biblia inajitetea vizuri: *"Kutahiriwa si kitu na kutokutahiriwa si kitu."* **(1Wakorintho 6:19)**, soma pia **Wagalatia 6:15.** |
| **4. Kwa nini Wakristo wanakosa heshima kwa Mungu Mwenyezi wa-napo kataa kuvua viatu wanaposali ?** | Tangu siku ile Mungu al-ipomuamrisha Musa kuvua viatu vyake **(Kut. 3:4-5)** waabuduo ni lazima wavue viatu popote wanaposali. | Amri hii ilimhusu Musa peke yake kwa wakati ule maalum. Tungetii, kama ingekuwa amri iliyotolewa kwa wote. |

| | | |
|---|---|---|
| **Au …hamtawadhi...**<br><br>**Au hamuinami kichwa chini.......** | Wanakuja mahali patakatifu | Ni vema kutembea bila viatu wakati wote kwa kuwa pia inasema: *"Ulimwengu wote umejaa utukufu wake."* **(Isaya 6:3). Soma pia Zab. 51:10; 22:29, Waefeso 3:14 Mathayo 26:39)** |
| **5. Kanisa halikujengwa juu ya Petro, bali lilijengwa juu ya Shetani** | *"Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda Yesu aligeuka na kumwambia Petro, 'Nenda nyuma yangu Shetani!* (Matt. 16:23) | Petro aliitwa Shetani kwa sababu alikataa kukubali kifo cha Yesu msalabani (Mat 16:22) na, licha ya hayo, Yesu mwenyewe ndiye msingi wa Kanisa kama ilivyo katika **(1Korintho 3:11).** |
| **6. Paulo asingeweza kuwa Mtumishi wa Mungu; kwa kweli ni yeye aliyeanzisha Ukristo.** | Waislamu wanashindwa kumkubali Paulo kama mtumishi wa Mungu.<br>Je, hakuwa Paulo aliyeibua fikra ya Utatu, Imani ya Upatanisho na uheresi mwingi mwingine …?<br>Watauliza maswali kama haya ili kuonyesha wanayosema ni ukweli. | Biblia inasema:<br>*"Paulo Mtume – ambaye hakutumwa kutoka kwa watu wala na mtu bali na Yesu Kristo, na Mungu Baba"* **(Gal.1:1)**<br>Na, Paulo anasisitiza:<br>*"Injili hiyo niliyowahubiri nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu …. Bali naliipokea kwa mafunuo kutoka kwa Yesu Kristo."* **(Wagalatia 1:11- 12)** |
| **7. Ukristo haustahili kuitwa dini hivi leo kwa sababu ninyi hamutendi tena kabisa.** | Kitabu chenu wenyewe kinasema: *"Dini ambayo Mungu Baba anaikubali kama ni safi isiyo taka ni hii: kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao na kujilinda usichafuliwe na dunia."* **(Yakobo 1:27)** | Matendo mema hayawezi kutupatia wokovu, bali kumwamini Yesu pekee kwa ajili ya kupata masamaha ya dhambi zetu. Hapo ndipo tutakapoweza kuishi maisha ya kumtii Yesu kama Wakristo. **(Yohana 1:12; Mako 9:41)** |

## 7.7 Ushuhuda wa Watu Walioona Unathibitisha Kusulibishwa na Kufufuka kwa Yesu

Mtume Paulo anawataja watu wengi walioona:

> *"Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyopokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko, na ya kuwa … aliwatokea ndugu zaidi ya mia tano pamoja; katika hao wengi wanaishi mpaka sasa". (1Wakorintho, 15:3-6)*

Mtume Paulo anachosema hapa ni kuwa kama hamniamini, pandeni boti kutoka Korintho hadi Joppa, tembeeni kidogo hadi mfike Yerusalemu na kuwauliza ninyi wenyewe.

Petro anatoa ushahidi wake binafsi: Jaribu kufikiria kungetokea nini, baada ya Petro kumaliza mahubiri yake siku ya Pentekoste, kama hili lisingekuwa kweli!

> *"Watu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamuuwa …" (Matendo 2:22-23).*

Tukumbuke kwamba maneno hayo yalitamkwa majuma saba tu baada ya siku ile ya kusulibishwa kwake Yesu! Watu waliokuwa wanamsikiliza wangeza kusema: "Mpendwa wetu Petro haikosi ulikuwa unaota ndoto! Ni nani alisulibishwa na kuuawa?

Na hata wakati ule Injili ilipokuwa inaanza kuhubiriwa, watu wa Yerusalemu wangeweza kupinga hadithi hiyo kwa kupiga kelele – kama ingekuwa siyo kweli. Hebu soma kwa uangalifu Kitabu chote cha 'Matendo ya Mitume' ukiwa unalikumbuka hili kichwani mwako.


## 7.8 Wana Historia wanathibitisha Kusulibishwa kwa Yesu

Mwandishi maarufu sana wa historia wa karne ya kwanza, Tacitus aliandika hivi: *"Jina la 'Wakristo' wanalipata kutokana na Kristo aliyehukumiwa kifo zama za Mfalme Tiberio kwa mashitaka ya Pontio Pilato"*

Tafadhali, zingatia kwamba huyo Tacitus alikuwa mpembuzi mkali wa imani ya Kikristo. Lakini hata yeye alikiri kwamba kusulibishwa kwa Kristo Yesu na mtawala wa Kirumi ni ukweli unaojulikana.

Takriban wakati huo huo, mwana historia wa Kiyahudi, Flavius Josephus aliandika:

*“Wakati huo alikuwapo Yesu, mtu mwenye hekima, kama kweli ni haki kumwita mtu, kwa sababu alitenda miujiza ya ajabu, pia alifundisha watu waliopenda kupokea ukweli. Aliwavuta kwake Wayahudi wengi na hata watu wengi wa mataifa. Yeye alikuwa Masihi. Na wakati Pilato, kwa kushinikizwa na watu mashuhuri wa taifa letu, alimhukumu kifo msalabani; na wale wapenzi wake tangu awali hakuwaacha, kwani aliwatokea akiwa hai tena siku ya tatu, kama ilivyotabiriwa na manabii watakatifu hapo kabla … (Antiquitates Jueacum, Kitabu cha Josephus Vol. 2, uk. 412); Katika kitabu “Majibu ya Wakristo kwa Waislamu” kur. 98-102.*



*Tuzingatie:*

**Wayahudi** wanakubali kusulibiwa kwa Yesu: Lakini hawakubali kwamba yeye ndiye Masihi (ingawa walikuwapo).

**Waislamu** kwa dhati kabisa wanamwita Yesu ‘Masihi’ Lakini wanakataa kuwa hakusulibishwa! na msingi wa dai lao ni sauti iliyosikika miaka 600 baada ya tukio la Yesu kusulibishwa!

***Kutimia kwa unabii kuhusu Yesu ndani ya Agano la Kale ni ushuhuda wa kutosha wa ukweli wa Biblia.***

Tayari tumekwisha kuangalia kwa ufupi manabii wa siku za zamani walitabiri nini kuhusu Yesu, Masihi. Hebu sasa tuangalie unabii huo kwa undani zaidi.

| | **Unabii wa Agano la Kale** | **Kutimia katika Agano Jipya** |
|---|---|---|
| Alitazamiwa atokee miaka 483 baada ya amri ya kujenga Mji wa Yerusalemu uliobomolewa na Nebkadneza | Dan. 9:24-26<br>445 KK | |
| Atazaliwa mjini Bethelehem | Mika 5:2 | Luka 2:42ff |
| Atazaliwa na Bikira | Isaya 7:14 | Matt 1:18ff |
| Atakuwa Mungu Mwenyewe (haimaanishi Mungu hatakuwapo mahali pengine vile vile) | Isaya 7:14; 9:6 | Matt 1:18ff |

| | | |
|---|---|---|
| Jina lake ni Mwokozi (=Yesu) | Isaya 49:1-8; 63:8 | Matt 1:21 |
| Atakuja kuokoa na kuponya | Isaya 35:4-5 | Matt 1:21<br>Luka 19:10 |
| Ataingia Yerusalemu akiwa amepanda punda | Zech 9:9 | Matt 21:1-9 |
| Atasalitiwa na rafiki | Zaburi 41:9 | Mako 14:10; 21:43-44<br>Matt 27:3-8 |
| Atauzwa kwa vipande 30 vya fedha<br>Atashitakiwa na kuhukumiwa kifo | Zech 11:12-13<br>Isaya 50:6; | Mathayo 26:15<br>Yohana 18 + 19 |
| lakini si kwa makosa aliyofanya | 53:1-12 | |
| Mikono na miguu yake itatobolewa<br>Mavazi yake yatagawanywa na | Zab 22:1, 7-17<br>Zaburi 22:18 | Yohana 18 + 19<br>Yohana 18 + 19 |
| kanzu yake itapigiwa kura | | |
| Lakini aliye mtakatifu hataonja uharibifu | Zaburi 16:10 | Luka 24:1-11 |
| Atainuliwa mbinguni na kuketi mkono wa kuume wa Mungu | Zaburi 110:1 | Matt 26:64<br>Waebrania 1:13. |
| Atarudi, na wakazi wote wa Yerusalemu watamwona yeye aliye-chomwa kwamkuki | Zekaria 12:10 | **Unasubiriwa ku-timizwa** |

Mambo hayo yalitabiriwa kati ya miaka 1000 na 500 KK (kabla ya Kristo). Yote yanaeleza kwa ukamilifu mkubwa - mambo ambayo yasingeweza kabisa kubuniwa – ambayo yametimia kila moja kama ilivyotabiriwa.

***Hitimisho:***

Kwa sababu ya ishara hizo za kiungu, tunaweza moja kwa moja kutegemea juu ya ukweli wa Biblia. Kwa upande mwingine, Kurani haiwezi kutoa utabiri wala kuonyesha kitu kingine chochote kuthibitisha madai yake ya kuwa kitabu kitakatifu. Hoja zinazotajwa na Waislamu, kama vile sura yake ya kupendeza katika maandiko ya Kiarabu, na ugumu unaoonekana dhahiri wa mtu asiyejua kusoma na kuandika kama Muhammad kuweza kuandika Kurani, pamoja na madai yake ya usahihi wa maandiko ni vijasababu vya kibinadamu ambavyo havina usahihi wowote.

***Kumbuka kusoma na kuyajibu maswali yaliyotolewa katika kurasa za nyongeza. Endapo utahitaji msaada, usisite kuwasiliana nasi!***

# 8. Kuwashuhudia Waislamu

## *8.1 Hali Kama Ilivyo hivi Sasa*

Hakuna wakati wowote Kanisa limelichukulia suala la uinjilisti kwa Waislamu uzito unaositahili. Vikundi vidogo vidogo au watu binafsi ndio ambao mara chache wamejaribu kuwashuhudia, lakini matendo hayo hayakuwa na mfululizo wala hayakuwa na mkono wa Kanisa.

*Sababu moja kubwa ya kuwapo mapungufu katika kuwashuhudia Waislamu ni woga na ujinga*

Ni muhimu kutambua kwamba woga msingi wake ni ujinga. Kila mtu anaogopa nyoka. Lakini, endapo nitafahamu wana tabia gani wanapochokozwa, na nini la kufanya kama mtu ameumwa na nyoka, basi woga wangu utapotea. Ujuzi na uzoefu hupunguza sana woga.

Mfano huo unahusiana na uinjilisti wetu kwa Waislamu. Mkristo asiyejua, ambaye hafahamu Uislamu na Waislamu, wakati anapokabiliwa na propaganda ya kawaida ya kupinga Ukristo, atakuwa hajui kabisa afanye nini katika hali hiyo. Ujinga husababisha woga, pia hukandamiza uinjilisti.

Kwa hivyo, ili tuweze kulifikia suala lenyewe la jinsi ya kuwahubiria Waislamu, inatupasa kwanza tuchukue njia ndefu ya kuchunguza imani ya Uislamu na madai yake, na wakati huo huo tukizingatia fikra za Waislamu kuhusu Biblia. Yatupasa tuwe na uzoefu kuhusu mambo hayo ili tuweze kufafanua wazi wazi maana ya Injili kwa Mwislamu. Ni dhahiri kwamba Mungu anaweza na huamua juu ya masuala fulani kama apendavyo, na tunamshukuru sana kwa ajili ya hilo. Hata hivyo sisi wenyewe tujizatiti sawa sawa tunapoamua kuwahubiria majirani zetu Waislamu na marafiki.


## *8.2 Je, kuna kitu kinachoweza kuitwa hali ya kawaida?*

Ndiyo na hapana. Hapana kwa sababu vitendo vya dini, tuseme, vya Mwarabu Mwislamu, vina sura mbali mbali na vitu mbali mbali vinavyotofautiana na Mwislamu nchini Uturuki, Malaysia au Tanzania. Hata ndani ya nchi fulani inayojulikana, wapo Waislamu wa kawaida, na wale wenye 'Uislamu wa kienyeji', ambao pengine unajumuisha mapokeo mengi ya dini za asili, hofu ya mizimu na vitendo vya ushirikina. Kisha wapo wale ambao ni Waislamu wa jina. Kuna matajiri na fukara, wasomi na wenye elimu kidogo tu, watu wa vijijini na watu wa mijini. Watu wakimya na wenye maneno mengi. Kumbe, hata sisi wenyewe, vile vile tuko watu tofauti-tofauti.

Lakini basi, tunaweza kusema “Ndio, kuna kitu kinachoweza kuitwa hali ya kawaida.” Kutokana na maendeleo ya ufundi na fasihi, elimu na ujuzi wa kawaida huweza kupatikana zaidi na zaidi kwa hali inayolingana. Mwislamu wa Bara Hindi, Uturuki na Tanzania wanaweza kuwa wanafanana katika njia za kujadiliana na kuwa na misingi ya imani na maamuzi yanayofanana. Waislamu wanaoishi katika nchi yenye misingi imara ya Ukristo inayofahamika watakuwa wamepata mafunzo mazuri ya kujihami dhidi ya Ukristo, lakini kwa kiasi fulani tu.

### *8.3 Tunaposema Uinjilisti tuna maana gani?*

Kwanza kabisa, Uinjilisti maana yake ni kumpatia mtu mwingine habari kuhusu:
**Mungu ➢ Mwanadamu ➢ Sheria ya Mungu ➢ Dhambi ya mwanadamu ➢ Upatanisho na Mungu.**




Pindi habari zote hizi zinapokuwa zimeeleweka – na hapa hatujafikia kusemea juu ya uelewa wa kiroho, hapo ndipo panapofaa mtu kupewa mwaliko wa kukubali ahadi ya Mungu: msamaha kamili ya dhambi kutokana na kutubu. Mungu katika Kristo alipata mateso msalabani na kwa njia hiyo, alilipa deni lote la dhambi. Kadiri Mungu anavyohusika, tatizo letu la dhambi huisha, mara tu tunapokubali msamaha Wake, na kuamua kuishi kwa kujitenga mbali na dhambi siku zote, na kuishi maisha ya umoja pamoja Naye. Kupokea maisha mapya kwa neema kwa njia ya imani kunamaanisha kwamba Roho Mtakatifu, ambaye ameyafumbua macho yetu kuona sura mbaya ya dhambi na hukumu inayofuatana nayo, sasa anamwongoza muumini mpya katika ukweli wote, bila shaka, kama alikuwa amemaanisha katika azima yake. Lakini hata hivyo, ni lazima tukubali kwamba hatutaweza kuishi maisha yasiyo na dhambi! Bado tunaendelea kuishi chini ya neema (Warumi 5-8).
Labda tunaufikiria uinjilisti mara nyingi zaidi tu kama mwaliko wa kumpokea Kristo kama Mwokozi. Hiyo hakika itakuwa na maana ya kufuja sura ya Injili. Kwa hakika Injili ni zaidi ya hilo!

### *(1) Ukweli wa Injili*

Mungu anaupenda ulimwengu, au tuseme hasa kwamba Yeye anapenda watu wanaoishi ndani ya ulimwengu Wake. Anachukizwa na dhambi zao, lakini anaangalia kwa masikitiko na huruma katika hali yao ya kuwa maskini. Hali yao ya kutokujitambua wao ni nani, kusudi lao ni nini na thamani ya utu wao ni ipi, ndiyo iliyomfanya Mungu aandae mpango wa kuwapatanisha binadamu ili wamrudie Yeye. Kwa hivyo, sasa watu wanaishi maisha ya juujuu ambayo lengo lao ni kujipatia starehe kubwa, mamlaka ya kutawala watu wengine, au kupata bidhaa na kujilimbikizia fedha. Hayo hayakuwa makusudio ya Mungu kabisa.

Mungu aliwapatanisha, kama Nabii Isaya alivyosema, kwa kuwa Yesu wao, au, kama tukilitafasiri jina hili – Mwokozi wao (Isaya 63:8). Katika "mateso yao yote, yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa. Kwa mapenzi yake na huruma zake, akawakomboa" akawainua, akawachukua siku zote za kale na kutuangalia (Isaya msitari wa 9). Lakini watu wengi wakaasi na kumhuzunisha Roho wake Mtakatifu' (Isaya msitari wa 10). Licha ya hayo, tunasoma katika kitabu cha mwisho cha Biblia kwamba Yesu alisema: "Tazama, nasimama mlangoni, nabisha, mtu akiisikia sauti yangu na kufungua mlango nitaingi!" (Ufunuo 3:20)

Mungu alikuwa Yesu wetu, alikuwa mwanadamu na kufa, kitu ambacho Mungu kama kiumbe wa kiroho tu asingeweza kukifanya. "Aliutoa" uhai Wake kwa ajili ya kondoo zake (Yohana 10:15), akalipa kwa damu yake gharama ya kosa letu, dhambi na aibu yetu, ili atununue na kuturudisha Kwake. (Mathayo 20:28; 1Timotheo 2:6; Waebrania 9:15) Alikuja, ili kwamba wote "waliokuwa wamekufa ndani ya dhambi" wainuliwe na kupelekwa kwenye maisha mapya – maisha ya milele mbele zake (Waefeso 2:1-2,6-10; Warumi 6:4; Yuda ms 24-25; 1Wathesalonike 3:9). Nani anafahamu kwa nini Mungu alichagua njia hii, na hakuchagua njia nyingine yoyote? Hakuna anayefahamu. Lakini kitu kikubwa ni kile kwamba sisi tunaweza kumwamini Yeye kwa ukamilifu.

### *(2) Ushuhuda wa Injili*

Kwa njia yake mwenyewe, Mungu anatuhakikishia kwamba tunaweza kumwamini Yeye na kukubaliwa na Yeye: *"Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu." (Warumi 8:16)*

Bila shaka, huo ni ufahamu wa hali ya mtu binafsi. Je, hakuna uhakika wenye uzito zaidi wa kuridhisha zaidi? Bila shaka upo. Kama tulivyochunguza kwa karibu hivi punde. Kuna utabiri mwingi sana na usio tarajiwa, ambao Mungu aliupa uvuvio ili uandikwe na Manabii wa Agano la Kale, ambao umetimia.

Historia nzima ya Israeli, pamoja na kutawanyika kwa Wayahudi na hata kuanzishwa upya kwa Israel baada ya miaka 1900, jambo ambalo ni la pekee kabisa katika historia ya ulimwengu, lilisha tabiriwa. *(Habari zaidi zinaweza kupatikana kama mtu ataomba).*

Lakini, unabii wa ajabu zaidi ni ule unaomhusu Kristo mwenyewe. Je, unafahamu kwamba, katika Injili ya Mathayo peke yake, kuna sentensi 24 zisemazo, 'Kama ilivyo tabiriwa na manabii', 'ili kutimiza maneno yaliyosemwa na ….. na kadhalika ?

Jambo zuri ni kwamba tunaweza kuonyesha ushahidi huu wa ndani kuthibitisha ukweli wa Injili. Nakushauri uchukue orodha hii ya unabii na kutimia kwake katika Biblia.

Kadhalika mhubiri mwenye uzoefu anaweza kuongezea ushahidi mwingine kutoka matokeo ya utafiti wa mambo ya kale, historia na shuhuda za watu walioona kwa macho yao. Hakuna yeyote ambaye baada ya kuonyeshwa ushahidi kamili kama huo, anayeweza kuendelea kushikilia kwamba Biblia ni kitabu kama vilivyo vitabu vingine vilivyotungwa na binadamu.

Lakini yatupasa tuongeze hili pia:

### *(3) Ahadi za Injili*

Mwislamu alitusimulia kisa kimoja ambacho alisema kilimbabaisha sana sheikh wake alipomuuliza swali: Hivi sisi Waislamu tunazo ahadi zipi hasa? Aliongeza kutuambia, nafahamu ya kwamba kitabu chenu kina ahadi nyingi sana kuliko Kurani yetu. Naam! Tunaweza kufurahi pamoja na mtunga Zaburi:

> *"Mausia yako ni matamu sana kwangu, kupita asali kinywani mwangu" (Zaburi 119:103).*

Je, tunayafahamu (mausia) hayo na kuyathamini? Hebu tuangalie machache tu.

Mungu aliwaahidi watu wake rehema zake (Zaburi 103:7), Msamaha (Zaburi 103:12; Isaya 59:3; 43:25, 44:22; Yeremia 31:34, n.k.), Uzima wa milele (Yohana 10:22-28; Mathayo 25:34; 46 b n.k.)

Maisha mapya (2Kor. 5:17), Kupumzika (Matt.11:28; Ufunuo 14:13), Kuwapo kwake katika maisha yetu (Matt.28:20b). Yeye anataka kutupatia yale yanayo tumainiwa na dunia nzima pasipo kuyapata, ambayo ni upendo, amani na furaha (Yn. 14:27; 15:9-11; Wagalatia 5 :22). Na zaidi ya yote, Yeye anatuahidi sisi wafuasi wake, maisha ya mbinguni: (Yohana 14:3l; Ufunuo 5:10), Anatupatia vipawa vinavyotusaidia kufanya kazi Yake hapa duniani (1Kor.12:8-10; Waefeso 4:1; Warumi 12:6-8 na hasa Matendo 2:38b).

*La mwisho, lakini si kwa udogo, inatupasa pia kufahamu:*

***(4) Masharti ya Injili***

> *"Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni." (Mathayo 7:21)*

Kabla mtu yeyote hajakaribishwa amjie Bwana Yesu ili kuomba msamaha, ni lazima kama ni mume au mke, yampasa kukaa chini na kuhesabu gharama yake (Luka 14:28)! Kutubu na kuungama ni masharti ya kusamehewa, na maana yake ni kuamua kuacha dhambi yenyewe (Luka 13:3). Tunajua kwamba hatuna uwezo wa kuacha dhambi.
Lakini Mungu ameshughulikia hali hiyo pia:*"Nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. na, kama mtu akitenda dhambi tunaye Mwokozi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki …" (1 Yohana 2:1)* Kuwa tayari kutii (Waebrania 5:9), kunathibitisha kwamba tunamwamini Mungu, kwa sababu yeye anajua kuliko sisi. Ustahimilivu na uaminifu pia ni masharti ya wokovu, kwa kuwa: *"Mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakayeokoka."* (Waebrania 3:6; Ufunuo 2:4; Mathayo 24:13) Imani na 'uaminifu' hutembea pamoja. Hayo yaonyesha kwamba uamuzi wa kumpokea Kristo usikosewe na kuwa ni sawa na kuongoka (kubadili nia). Muumini ameteuliwa na kuwekwa kwa ajili ya Mungu kwa kusudi Lake maalum. Biblia huita kitendo hicho 'utakaso'. *"Bila ya utakatifu hakuna mtu atakayeweza kumwona Bwana" (Waebrania 12:14; 1Petro 1:13-19).*
Kutomfundisha habari hizi mtu mwenye nia ya kuongoka ni kumwambia tu upande mmoja wa Injili. Ni lazima tuhakikishe hatufanyi kosa hilo. Lakini vile vile tuzingatie jambo hili; Mungu ndiye mwanzishaji na mmaliziaji wa imani yetu (Wafilipi 1:6). Maisha ya Mkristo ni ya ki-miujiza! Kama isingekuwa kwa msaada wa Mungu na busara yake ya uvumbuzi, hakuna ambaye angeweza kumjia Kristo, sembuse kuvumilia hata mwisho!


***8. 4 Kabla ya Uinjilisti***

Waislamu wengi tunaokutana nao wameshaamua vibaya dhidi ya imani ya Kikristo. Hili linawafanya kuielewa vibaya kabisa imani yetu. Lengo la kutayarisha mazingira kabla ya uinjilisti ni kusafisha njia ya kuendea kwenye uinjilisti. Kile 'kifusi' kinachoziba njia ya kumjua Kristo hakinabudi kuondolewa kwanza. Huenda jambo hilo likachukua muda, lakini ni lazima lifanyike kabla mtu hajamuuliza mtu amkubali Kristo kama Bwana na Mwokozi wake binafsi.

Hebu tulitazame suala hilo kwa njia hii: Kwa nini Mwislamu apende kumjia Kristo, madhali yeye fikra iliyomjenga ni kwamba Yesu ni nabii aliyeletwa kwa Wayahudi tu na ameleta ujumbe ambao sasa umechafuliwa na kubadilishwa na hatimaye ikawa hapanabudi uondolewe na kuletwa toleo la kitabu kipya cha Muhammad ambacho hakikubadilishwa? Mwislamu anavyotuona sisi ni sawa na sisi tunavyowaona wafuasi wa madhehebu ya Mermon au Mashahidi wa Jehovah wakitujia kwa dhamiri ya kutushawishi tukubaliane nao juu ya maoni ya dini yao. Kazi ya kuanzisha mazingira mazuri ya Uinjilisti hainabudi kuwa ni kufafanua maudhui na kusahihisha fikra zenye makosa.

### *8.5 "Uinjilisti wa Kirafiki"*

Kwa kawaida ni vigumu sana kuwasiliana na Waislamu wakiwa katika kikundi au mkutano. Shahidi Mkristo akiwa mmoja au wakiwa wawili tu na Waislamu vile vile, wawili au mmoja tu, na wanapokuwa katika starehe ya kukaa nyumbani au mahali pengine walipozoea, hapo ndipo wanapaswa kuelekeza mazungumzo pole pole katika mambo ya kiroho.



**Uinjilisti kwa waislamu kwa kawaida ni wa kuwasiliana mtu mmoja mmoja**

Jambo hili huwa rahisi zaidi kwa Waislamu kuliko ilivyo kwa makundi mengineyo. Kwa jumla, Waislamu ni watu wanaoipenda dini yao. Hupenda sana kuzungumzia kwa hiyari dini yao. Wanapenda sana kutushawishi na pengine wanatazamia kwamba tunataka kufanya hivyo kwao. Kwa hivyo, hebu tulenge kujenga uhusiano pamoja nao hata kama Kurani inaonya Waislamu kuhusu jambo hilo kama hivi:

> *"Enyi mlioamini!, msiwafanye marafiki wale walioifanyia mzaha na mchezo dini yenu miongoni mwa wale waliopewa kitabu kabla yenu na miongoni mwa makafiri (wengine).. (Surah 5:57)*
> *Hawatakuwa radhi juu yako mayahudi wala Wakristo mpaka ufuate mila yao.' (Surah 2:120)*
> *Ninyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishwa watu ulimwenguni-mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwa-*

*mini mwenyezi Mungu. (Surah 3:110)*
*Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Mnataka awe nayo (mtume wa) mwenyezi Mungu hoja dhahiri juu yenu (ya kuwa nyinyi dhahiri). (Surah 4:144)*

Kwa upande mwingine Kurani vile vile inatoa matamko yenye maana. Surah 5:82 ni ya kwanza miongoni mwa hizo Surah zenye tamko la maana:

*"Hakika utawakuta walio maadui zaidi kuliko watu wengine kwa Waislamu ni Mayahudi na wale mushirikina (wasiokuwa na kitabu), na utawaona walio karibu kwa urafiki na Waislamu ni wale wanaosema, sisi ni Wakristo.(Hayo) ni kwa sababu miongoni mwao wanavyuoni na wamchao Mungu, na kwa sababu wao (Wakristo)hawatakabari."*

Je, tufiche sura ya kweli ya madhumuni yetu, tujidai kuwa hatuna haja ya kuwahubiria Injili ? Jitahada kama zile za 'kuhubiri kiataalam' kwa kujitangaza kuwa sisi ni 'Waislamu wa Yesu' ambao tumekumbatia mapokeo ya Kiislamu kama vile kufunga wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, tunasali kuelekea Maka, na mengineyo, ni dhahiri kutatafasiriwa na Waislamu kukubaliana na mistari yao ya kutumia uongo ili kuficha malengo yao ya kweli. Jambo hilo linajulikana kama "taqiyya" (= ufundi wa kudanganya) ambao msingi wake ni Surah 16:106!

Biblia inatoa jibu lililo wazi kabisa:

*"..... lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya neno la Mungu na uwongo bali kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu..." (2Wakorintho, 4:2).*

Kwa hili, Waislamu hawana lugha 'ya kuzunguka'. Wanasema wazi wazi, na mara nyingi kwa msisitizo wanapotangaza msimamo wao. Sisi nasi tufanye yayo hayo! Tukumbuke tu, kuna tofauti kubwa sana kati ya kushirikisha mtu mwingine kwa upole, upendo na heshima na mahubiri ya kuwaburuza watu yasiyo na mpangilio wowote. Wale wanaojidai ni "mashahidi' wa kuburuza watu, wanafunga milango yasiwepo mahubiri ya busara na yenye maana. Kwa hivyo, hatunabudi kufanya lile tu lililo sahihi, kwa kuzingatia yote mawili, tuwe wajasiri na wenye heshima.

## *8.6 Kukabiliana au kuridhiana?*

Tumezungumzia tu juu ya uinjilisti wa kirafiki. Mimi napenda kubadilisha neno 'urafiki' kwa kutumia neno 'uhusiano', kwa sababu, mtu asiyempenda Mungu na wala hajaokolewa na Kristo hawezi kuwa rafiki yangu kwa maana halisi ya neno hilo. Biblia ina mengi ya kusimulia juu ya kuwa na urafiki na ulimwengu

au kufungiwa nira pamoja na watu wasioamini. (2Wakorintho 6:4). Kuwa na urafiki mkubwa na watu wasio mwamini Yesu, ni jambo lisilopendekezwa. Lakini, ili tuweze kuhubiri Injili vizuri, uhusiano wa binafsi ni mzuri sana. Katika hali hiyo, kuaminiana na kuheshimiana kunaweza kusitawi, na kwa kweli ndio msingi mzuri wa uinjilist.



Hata hivyo, mahubiri ya moja kwa moja au mahubiri kwa njia nyingine, tunayo taka kutumia kutangaza Ukweli yanaweza kuleta matokeo ya kukataliwa. Hakuna anayetaka kukataliwa. Kukataliwa kunauma! Na, vile vile kunaleta kumalizika bila mafanikio kwa mahubiri ya Injili. Kwa hiyo, inatupasa kuweka uwiano sahihi. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunahubiri tu na yale ambayo tumeyapata kwa uangalifu na upendo kutoka Neno la Mungu.

Kwa upande mwingine, kuridhiana kuna maana ya kwamba tuko tayari kukubaliana. Hili lina uwezekano wa kuendeleza mahusiano yetu, ikiwezekana, bila kikomo, kwa sababu tunajizuia kusema neno lolote linalowaudhi wenzetu kuhusu Biblia – bali tunasema yale tu anayopenda kusikia juu ya Uislamu. Tunapojaribu kuchukua sehemu fulani ya Uislamu (au dini yoyote) na kuichanganya na ujumbe wa Kikristo ili kufanya mahubiri yetu yawe ya kuvutia zaidi wasilikilizaji, tunateleza na kuingia upande wa kutokubaliana na upande wowote katika imani ya dini. Kuliepuka hilo nalo, kunaweza kupelekea kuleta makabiliano na hata pengine kukataliwa. Tayari Biblia imeshatuonya juu ya jambo hilo kama ifuatavyo:

> *“Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. Lakini kama mnavyo shiriki mateso ya Kristo, furahini: ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe. Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia.” (1Petro 4:12-14)*
>
> *“Mtumwa si mkubwa kuliko bwana wake. Ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi … lakini haya yote watawatendea kwa ajili ya jina langu, kwa kuwa hawamjui yeye aliye nipeleka.” (Yohana 15:20)*
>
> *“Heri ninyi watakapo washutumu na kuwaudhi na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili yangu.” (Mathayo 5:11)*

➔ ***Tafadhali yatafakarini mambo hayo kwa kutumia maswali ya ukurasa wa** ……….*

# 9. Mawasliano yenye nguvu za Mungu

## *9. 1 Ukweli na mamlaka katika Uinjilisti*

Baada ya mkutano mkubwa wa Injili katika jiji fulani la Afrika, ilidaiwa kwamba mamia ya Waislamu waliponywa na kuokoka. Lakini tathmini iliyofanywa baada ya mwaka mmoja ilionyesha matokeo ya kusikitisha sana. Hapakuwa na Mwislamu hata mmoja aliyejiunga na kanisa lolote katika mji huo wala hapakuwa na uthibitisho kwamba mtu yeyote alipata uponyaji! 'Uinjilisti wa nguvu' mara nyingi huonekana kama nguvu ya kisaikolojia au ushawishi wa mawazo tu kuliko 'uweza wa Mungu uletao wokovu." (Warumi 1:16)

## *9. 2 Mamlaka ya Mungu - au mamlaka ya nafsi ya mwanadamu?*

Hapana shaka yoyote kwamba daima mamlaka ya kweli ya Mungu huwa imevaa unyenyekevu wa mhubiri. Mhubiri anapojaribu kukuza umbile lake kwa kupaza sauti au kufanya maigizo kwenye jukwaa, mara nyingi sana ni maonyesho ya nguvu yake binafsi. Inasikitisha kwamba watu mara nyingi hudanganyika na kutishika, na pengine wamezoea kuona 'maonyesho' hayo kiasi cha kushindwa kutofautisha kati ya uweza wa kweli wa Mungu unaopitia kwa mhubiri, na nguvu ya nafsi ya yule mhubiri mwenyewe.

## *9.3 Mamlaka ndani ya udhaifu*

Tunasoma habari za Paulo kwamba 'aliwajia Wakorintho …. 'katika udhaifu na hofu huku ameshikwa na tetemeko." (2Wakorintho 12:9). Lakini Paulo alikiri pia, kwamba Mungu amemwambia ya kuwa neema yake ilikuwa inamtosha kwani mamlaka yake hutimilizwa katika udhaifu (1Wakorintho2:3). *Lakini ujumbe wake (yaani mfumo wa jinsi ujumbe huo ulivyohubiriwa) haukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu…" Kadhalika tunasoma "... ya kwamba Injili yetu haikuwafikia katika maneno tu, bali katika nguvu na katika Roho Mtakatifu, na uthibitivu mwingi…" (1Wathesalonike 1:5). Na tena tunasoma: "…kwani ufalme wa Mungu hauwi katika maneno, bali katika nguvu." (1Wakorintho 4:20)*

Tunafahamu kwamba uweza huo haukuwa katika kipaza sauti. Kadhalika tunafahamu ya kwamba Paulo hakuwa msemaji hodari. Kwa hiyo, uweza huo ni upi? Hapa tunagundua kutokana na maandiko, kwamba hii maana yake ni kuvuta akili za watu kumfikiria Mungu badala ya mwanadamu anayehubiri. Roho Mtakatifu anamtumia mwanadamu kuwasha imani ili amwamini Mungu na kutegemea Neno lake. Yaani, 'uthibitivu mwingi'. Ni mawasiliano kutoka kwa Roho wa Mungu kupitia mhubiri kwenda kwa roho ya msikilizaji na kutoka

kwa mtu kwenda nafsi ya mtu mwingine au roho yake.
Je, tunawezaje kuzihamisha akili za watu kutoka kwetu kwenda kwa Mungu? Kwa kutambulisha mamlaka ya Mungu ni nini hasa? Biblia hueleza wazi kabisa.

*"Biblia ... ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye ... (Warumi 1:16).*
*"Neno la msalaba … ni nguvu ya Mungu." (1Wakorintho 1:18)*
*"Kristo aliyesulibiwa …. nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu." (1Wakorintho 1:23)*

**Ujumbe wa Msalaba = Kristo aliyesulibiwa = Injili**

Hili ni tamko la Mungu kuwa, mwanadamu hana njia yoyote ya kujiokoa mwenyewe kwa kufanya matendo mema isipokuwa kumtegemea Mungu tu na kile ambacho Mungu ameshamtendea.

**Injili hii ambayo ni ujumbe wa Msalaba peke yake, ndiyo yenye mamlaka ya Mungu yaletayo wokovu na maisha ya utakaso na uwezo wa kumtumikia Mungu.**

Kwa hivyo, Injili, kwanza kabisa, hainabudi kueleweka (na tutafanya jitihada kubwa kadiri tuwezavyo kutoa taarifa na kueleza), ndipo uamuzi ufuate kama mtu anapenda kumpokea Yesu Kristo kwa imani au kushika njia aitakayo.

Sisi tunaamini ya kwamba hii inamaanisha "udhihirisho wa nguvu ya Roho."

*"Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu, hata kuangusha ngome); tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukitekanyara kila fikra ipate kumtii Kristo." (2Wakorintho 10:3-5)*

## *9. 4 Nguvu za Shetani*

*Sangoma, mchawi,* mpiga ramli wa dini zote pamoja na dini ya Kihindu, mashehe au mganga wa kienyeji ambaye hutumia sehemu ya Kurani au vitu vingine kama "dawa" au vifaa vya uganga kwa ajili ya kumroga mtu fulani, wote hawa wanatumia nguvu za kiroho. Lakini nguvu yao ni "nguvu ya ulimwengu huu" (Waefeso 6:12). Tunasoma juu ya habari za mtu aliyekuwa chini ya mamlaka ya Shetani (Matendo 10:38). Mtu huyo anafananishwa na simba, ambaye ni alama halisi ya nguvu. (1Petro 5:8)

### *9. 5 Mashindano ya Nguvu*


Muhammad alitumia aina hii ya nguvu pia. Ujumbe fulani wa Wakristo kutoka Najran, Arabia Kusini, ulimtembelea na kukaa naye kwa siku chache wakijadili masuala ya dini. Wakristo walipokataa kusilimu, Muhammad aliwapa changamoto mbele ya mkutano wa hadhara. Surah ya 3: 61 inatusimulia juu ya tukio hilo:

> *"Semeni: Njooni! Sisi sote na tukusanye waana wetu, na ninyi kusanyeni waana wenu, wanawake wa kwetu na wanawake wa kwenu, sisi wenyewe na ninyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu; laana ya Allah ishuke juu ya wale wasemao uongo!".*

Alichokuwa anataka Muhammad ni kuwalaani Wakristo wale kwa jina la Allah, na Wakristo nao waombe laana kwa jina la Yesu ili wapate kuona kati ya (Allaha na Yesu) nani mwenye nguvu zaidi. Hayo ndiyo yanayoitwa "Mashindano ya nguvu" katika lugha ya kitheologia ya siku hizi. Wale Wakristo walikataa, kwa sababu hawakuitwa na Mungu kuwalaani watu, bali kuwabariki! Hata mimi, nimewahi kujikuta katika hali kama hiyo, ambapo Mwislamu fulani alinilaani, akinihakikishia kwamba ningekufa katika kipindi cha miezi miwili hivi. Hilo lilitukia miaka mingi iliyopita.
Wapagani watataka kujua ni roho wa nani aliye na nguvu; kwani wanachotaka wao ni kujisalimisha chini ya sangoma au mchawi mwenye nguvu sana. Waislamu wengi wa jina na Wakristo wa jina vile vile wanafanya hivyo, na kwa kufanya hivyo wanathibitisha kuwa wao ni wapagani wa kweli kwa mioyo yao. Bila ya shaka Yesu alimshinda Shetani. Na, sisi bila ya shaka, tumeokolewa chini ya nguvu na ulinzi Wake! Sisi, kwa kweli, tumepewa mamlaka na Yesu juu ya kundi lote la maadui na hakuna chochote kitakachoweza kutudhuru (Luka 10:19). Kuna haja gani tena kurudi kwenye hofu na imani za kipagani?

### *9. 6 Mawasiliano Halisi*

Kuhubiri Injili kunategemea mambo mawili. Naweza kuyafananisha mambo hayo na misingi miwili ya daraja ambayo inashikilia daraja kila upande wa mto. Kwa upande mmoja, ufanisi wote unategemea uwezo wa mhubiri kuweka ukweli wote wazi ili ueleweke kwa ukamilifu, akizingatia uzoefu na nafasi ya msikilizaji; na kwa upande wa pili, inategemea kama msikilizaji



anamsikia Roho Mtakatifu anavyomshauri ili apate kumwokoa.
Kwa hivyo, daima tamko haliwezi kutenganishwa na:

1. Ujumbe ulio wazi, unaoeleweka na unaozingatia kwa upole hali ya msikilizaji, na
2. Maombi yetu kwamba ufahamu wa kibinadamu uelezwe na Roho Mtakatifu ili kufikia imani na uamuzi wa kujitoa.

Mtu fulani amesema kwamba inatupasa kufanya bidii katika kueleza Injili, kuongoza na kufundisha kana kwamba ufanisi wote unatutegemea sisi tu. Na pia inatupasa kumwomba Mungu, kana kwamba kazi zetu zote ni bure kabisa na ufanisi wote unamtegemea anayofanya Yeye tu. Kwa hiyo, tunafanya kazi yetu 100 %, lakini pia tunamwachia Mungu matokeo yake.
Bwana Yesu mwenyewe alisema wazi: "*Pasipo mimi, ninyi hamuwezi kufanya neno lote." (Yohana 15:5)*

## *9. 7 Vita vya Kiroho*

*"... ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikra zao wasioamini, isiwazukie nuru ya Injili ya utukufu wake Kristo ..." (2Wakorintho 4:5).*

> Vita vya kiroho msingi wake uko juu ya ukweli kwamba kuna vita kati ya Mungu na Shetani. (Ufunuo 12:7)
> Ni jitahada za kuvunja athari za kishetani ambazo ndizo hupofusha na kuwafunga wanadamu.

Mtu anaitwa kipofu kwa sababu hawezi kuona. Hata tukijaribu vipi kueleza uzuri wa bahari ya bluu yenye kina kirefu, au jinsi ua jekundu linavyopendeza ni kupoteza muda tu. Mtu kipofu hawezi kuelewa bluu au nyekundu, hata kama tungekuwa hodari kueleza kwa kiasi gani! Ni mtu anayeona tu ndiye anayeweza kuelewa uzuri unaoonekana.
Mwisilamu, kama mtu mwingine yeyote yule, ni kipofu asiyeweza kuona ukweli wa kiroho, haoni kabisa haja ya Mwokozi, kwa sababu ya hali yake ya dhambi. Je, tunawezaje kumsaidia ili apate kuona? Kwa kupiga vita vya kiroho dhidi ya nguvu zinazompofusha na kumfunga.
Hili haliwezi kufanyika kwa sala peke yake. Hatumwombi Shetani au mapepo yake waondoke. Tunawaamrisha waondoke kwa ina la Bwana Yesu, wamwache yule mtu! Tuwaamuru waondoke! "Katika Jina la Yesu" tuna mamlaka ya kufanya hivyo. Si maneno yetu yanayofanya kama uganga dhidi ya Shetani. Bali tunamwamuru kwa niaba ya Bwana Yesu Kristo (na utamke kila mara kwa

ukamilifu: "Bwana Yesu Kristo", kwa sababu mapepo wengi hujiita "Yesu"). Tunaamuru kwa mamlaka Yake:

> *"Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…" (Mathayo 28:18-19).*
> *"Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru." (Luka 10:19)*

Serikali yoyote, ikiwa imekwisha kumpa afisa wake wa polisi mamlaka, ndipoanaweza kumkamata jambazi. Serikali inamsimamia afisa wake. Mihimili yote ya mamlaka ya Serikali inamlinda anapotimiza majukumu yake. Anatenda kwa niaba ya Serikali yake. Hakuna lazima kwa Rais au Waziri Mkuu kufanya hayo mwenyewe.

Vile vile nasi tumepewa nguvu, mamlaka ya kuwa watendaji wa haki ya Mungu, ni wajibu wetu kuwakamata 'majambazi' wa kiroho.

Lakini Shetani naye ana kiasi fulani cha mamlaka.

> *"Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho." (Waefeso 6:12)*

Lakini, majeshi ya Shetani yamekwisha kunyang'anywa silaha zao:

> *"Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo"(Wakolosai 2:14-15). "Yesu Kristo amekwenda zake mbinguni naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, akiwa na malaika, enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini Yake." (1Petro 3: 21-22)*

Ingawa hayo yote yamekamilika, lakini Shetani na mapepo yake bado wana nguvu na mamlaka kiasi, ingawa mamlaka na nguvu tulizopewa sisi ndizo zenye uwezo mkubwa zaidi.
"Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu." (1Wakorintho 15:24)
Lakini, daima kunakuwako na fursa ndogo, ingawa siyo sheria, kwamba wale 'majambazi' (tunavyosema sisi, mapepo walio katika huduma ya Shetani) wanakataa mamlaka yetu. Tukio moja la kusisimua sana limeelezwa katika Matendo 19:13-16), nasi tutafanya vyema kama tutasoma na kutafakari kisa hicho.
Muumini wa Yesu Kristo amepewa mamlaka juu ya mapepo "katika Jina la Bwana wetu Yesu Kristo". Tunatumia mamlaka hiyo kwa imani. Maana yake

ni kwamba tusipoona matokeo mara moja, tusikate tamaa! Shetani daima atajaribu kutubabaisha mawazo, kutupuuza ili tusiendelee kupingana naye. Kwa imani tujione sisi ni washindi.

Hata hivyo, haina maana kwamba tunaweza kumwingiza kila asiye muumini katika ufalme wa Mungu. Mwanadamu amepewa hiyari ya kuchagua. (Kumb. 30:19; Yoshua 24:14, n.k.). Tunaweza kumshuhudia mtu. Katika hali ya kufungwa kiroho, kupagawa, au kulemewa. Tunaweza, kwa jina la Yesu Kristo kuamrisha nguvu zile zilizo mfunga ziondoke – na hatunabudi kulifanya hilo kwa mfululizo, lakini hiyo haina maana kwamba mtu anayeombewa atakata shauri mara moja kumpokea Kristo kama Mwokozi na Bwana. Tunasoma habari za Stefano, mfiadini wa kwanza, kwamba alikuwa amejawa na Roho Mtakatifu. Lakini, alipomhubiri Kristo, wasikilizaji wake walikasirika na ‘kusaga meno yao’, ‘waliziba masikio yao na kupaaza sauti ya juu kabisa iliyoweza kutoka vinywani mwao.” (Matendo 7:55-57). Walikataa ujumbe wake. Je, tumlaumu Stefano kwa sababu walifanya hivyo?

Katika Uislamu, upofu na ufungwa pengine una nguvu zaidi kuliko ilivyo katika dini nyingine zote. Hii kwa sehemu, inatokana na mfumo ambao Mwislamu anaishi ndani yake. Hapana shaka pia, kwamba Mwislamu amefungwa na ‘Roho ya Uislamu’ ‘bwana wa nyumba hii’ (ile Ka’aba kule Maka). Kwa hiyo, huduma yetu haianzii wala kuishia kushuhudia Injili, bali ni kumwomba Mungu ayafumbue macho ya hawa vipofu.

Kwa kanuni, hiki kitakuwa kipindi cha maombezi (pengine kikiambatana na kufunga. (Mathayo 17:21), na kukemea kwa nguvu roho chafu ziondoke, na hii inaweza kuchukua muda mrefu.

> *“Muwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi kama simba angurumaye, huzunguka zunguka akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani.” (1Petro 5:8- 9)*



Simba atashambulia kwa nyuma wakati mtu anapokimbia. “Mpingeni huyo! Simama imara!” Simba ni mwoga anapokutana na mtu uso kwa uso, hawezi kusimama na kumshambulia. Vivyo hivyo, hatunabudi kupinga nguvu za uovu zinazowapofusha na kuwafunga watu tunaowashuhudia. Tusikubali kabisa kumwacha Shetani abaki na

mawindo yake, bali tushambulie kwa ujasiri.
Yesu aliuliza: *"Atawezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu na kuviteka vyombo vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu?" (Mathayo 12:29).*

Yule "mtu mwenye nguvu" ni Shetani, pamoja na mapepo yake. "nyara zake' ni watu wasio mwamini Yesu. Hawawezi kukombolewa, hawawezi kuona, hadi yule 'mtu mwenye nguvu' kwanza atakapokuwa amefungwa. Hilo ndilo alilofanya Bwana Yesu Kristo. Lakini vile vile alimwambia Petro: *"Lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lolote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni." (Mathayo 16:19).*

Baadaye aliwaambia wanafunzi wake wote neno hilo hilo. (Mathayo 18:19)
Je, tumewahi kulifanya hilo hata mara moja? Ni sehemu ya "Utume Mkuu", sehemu ya kuhubiri Injili yenyewe.

Roho Mtakatifu wa Mungu alikuwa akiwafunulia watu ubaya wa dhambi na kuwafanya waridhike na ukweli wa Neno Lake na kuwaongoza ili waelewe ujumbe uliomo ndani yake. Roho waovu wa Shetani ni waigizaji tu wanaojaribu kuzuia kazi hiyo isifaulu. Kwa hivyo, hebu daima tuwe katika mchakato wa kuwapinga na kuwafunga ili kwamba wasiweze kuzuia kazi ya ushuhuda wa Mungu.

***Hebu tufanye muhtasari***

a. Shetani ameshindwa kwenye msalaba wa Kristo.

b. Lakini ana nguvu kiasi juu ya watu wasioamini, ambao yeye kwa kutumia mapepo yake maovu, huwapofusha na kuwafunga wawe watumwa wake.

c. Ili wawekwe huru, lazima kwanza "yule mwenye nguvu" afungwe. Yesu amekwisha kufanya hivyo. Lakini tunapaswa tufunge na kufukuza uovu kwa njia ya maombi na kukemea.

d. Kristo ametupa mamlaka ya kiroho juu ya mapepo na majini (soma Marko 3:15).

e. Lakini hata hivyo, mtu ana uhuru wa kuchagua kukataa kupokea msamaha ya Mungu ndani ya Kristo.

f. Vita vya kiroho si badala ya mawasiliano mazuri ya Injili na yenye uaminifu, wala si kinyume chake.

g. Tunatambua kwamba sisi hatuna nguvu wala mamlaka ya kwetu wenyewe. Ukweli huo utuongezee unyenyekevu. Kwa hiyo, maombi ni kukiri kwamba sisi hatuna uwezo na kwamba Mungu anatosha kwa yote.

h. Sala yetu iwe kwamba Uislamu ukiwa kama ndio mfumo mkuu wa kupinga Ukristo uvunjikilie mbali, na kwamba Waislamu, kama tunavyowafahamu, waokolewe kutoka vifungo vyao.

➔ ***Maswali yaliyoko katika nyongeza ya kitabu hiki yatakusaidia sana kama utayafanyia kazi maswali yanayopatikana kwenye (ukurasa wa……….) Tafadhali chukua nafasi kuyajibu jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza.***

# 10. Maudhui ya Injili kwa Waislamu

Inapendekezwa kwa nguvu kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya ibada, lakini kama maandalizi hayo hayaleti matokeo ya kugusa maisha ya Mwislamu, basi yanakuwa zoezi lisilo na maana.
***"Maisha yaliyoguswa na Mungu lakini hayagusi maisha ya watu wengine yana maana gani"*** Yatupasa tujiulize wenyewe (Dr. E. Chandran).

Unaweza kustaajabu, kumbe kuna ukweli fulani katika Biblia ambao ni wa kuvutia zaidi kwa Waislamu kuliko watu wengine. Hii ni hoja nzuri sana. Kwani hata Bwana wetu hakuhubiri ujumbe ule ule unaofanana kwa kila mtu aliyekutana naye. Tukipitia kwa haraka Injili ya Yohana tutaridhika mara moja kwamba huyo mwalimu mkuu mara nyingi alitumia muda kufundisha mada ambazo zilitolewa na mtu aliyekuwa akizungumza naye. Mathalan, Nikodemo – Surah 3; Mwanamke pale kisimani huko Samaria – Surah 4, au mafundisho yaliyokuwa yanahusika na mazingira na mahitaji ya watu aliokuwa akiwafundisha: Mimi ni …. mkate, nuru, kweli, mchungaji mwema, ufufuo na maisha.

*Kuna mada nyingi zenye malengo maalum kwa marafiki zetu Waislamu*

Hapa tunazo mada chache zinazoendana na ukweli wa Maandiko; haikosi utapenda kujifunza kila moja ya mada hizi kwa wakati wako.

### *10.1 Maudhui ya Kiislamu – Yakilinganishwa na mapokeo ya Kikristo*

- **Hajj:** Je, Wakristo nao pia wanakwenda kuhiji? Soma Waebrania 11:9-10; 13-16; 1Petro 1:1.
- **Kibla:** Sisi tunaangalia upande gani wakati wa kuabudu? Soma Yohana 11:41-42; Waebrania 12:2.
- **Shahada:** Wewe tamko lako la imani ni nini? Je, Wakristo wanayo imani? > Soma Mambo ya Nyakati 6:4; Yohana 17:3; 1Timotheo 2:4-5.
- **Shariyah:** Je, wewe unafuata mfumo upi wa sheria? > Soma Warumi 6:14; Yohana 13:34.
- **Wudu:** Je, mnazo ibada maalum za maungamo? > Soma Waefeso 5:25-27; Zaburi 51:10; 32: 1-4.
- **Zaka:** Wakristo wanatazamiwa kutoa kiasi gani cha fedha kama sadaka kuwapa maskini na wenye uhitaji? > Soma 2 Wakorintho 9:7 + 15.
- **Zamzam:** Kuna hadithi gani juu ya kisima hiki maalum? > Mwanzo 21:19; Yohana 4:13-14.

### *10. 2 Manabii – Tunajifunza nini kutoka kwao?*

Kumbuka ya kwamba Waislamu “wanaamini” manabii wote waliotumwa na Mungu. Lakini wengi wao hawafahamu zaidi ya majina yao tu! Hii inatupa sisi mwanya mzuri ajabu wa kueleza kutokana na maandiko ya Biblia wanaume hawa na wanawake walikuwa nani. Tafuta muda wa kukaa pamoja na Waislamu ili mjifunze pamoja juu ya maisha na masomo tuliyofundishwa sisi kutokana na Maandiko kuhusu:

- ✧ **Adam na Kristo:** - Je, ungependa, kama uwezekano ungekuwako, kuanza maisha yako upya? > Soma Mwanzo 3; Warumi 5:19-21; 1Wakorintho 15:2.
- ✧ **Abraham – Rafiki wa Mungu** - Je, wewe pia ungependa kuwa na urafiki wa karibu kama hivi na Mungu? (Soma maelezo maalum katika sehemu ya nyongeza ya kitabu hiki).
- ✧ **Isaka na Ishmael** - Ni nani aliyekuwa mwana wa kweli wa ahadi? > Soma Mwanzo 17:19; Surah ya 19 – 21; Waebrania 11:17-18; Wagalatia 4:28-31.
- ✧ **Yakobo: Mwanaume aliyekamatana mwereka na Mungu** - Je, tunaweza kutazamia Mungu kuyaangalia maisha yetu? > Soma Mwanzo 27-32; 32: 22-32.
- ✧ **Yusufu – aliyeinuliwa kutoka kuwa mtumwa hadi mtawala** - Tunawezaje kujifunza kuwasamehe wanaotuumiza kwa makusudi? Soma Mwanzo 37-50; 50:20 -21.
- ✧ **Musa: mwanadamu aliyetembea pamoja na Mungu** – Je, tunaweza kutembea tukifuatana na Mungu bega – kwa – bega kama kiongozi wa maisha yetu? > Soma Kutoka 2- 3; 14:19 -20; 33:7-23; 2Wakorintho 3:7-18.

### *10. 3 Matukio ya maisha, karamu na masuala ya mifumo ya maisha*

Hivi ni vyanzo vya kawaida vya hoja za kuingilia mahali tunapokutana na Waislamu kwenye sherehe mbali mbali au kuzungumza nao juu ya maisha na vifo. Matukio hayo ni pamoja na:

☯ ***Uzazi, kutoa jina (kwa mtoto aliyezaliwa) Tohara, Harusi, Maziko*** – Ni vyema kuuliza maswali kuhusu mambo hayo wakati watu wanapo jumuika kijamii na katika sherehe. Onyesha jinsi unavyoweza kushirikisha fikra kutoka Biblia ambazo zinaweza kuwa na msaada kwa rafiki yako Mwislamu. Labda ungependa waanze kufikiri kwa kuuliza: Kama mtoto huzaliwa akiwa na moyo safi, mweupe, kuna haja gani ya kuleta kafara kwenye sherehe ya mtoto kupewa jina? – Kwa nini (baadhi) ya Wakristo hawana kawaida ya kuwatahiri watoto wao; wanakosa nini? Soma > Wagalatia 6:15 – Siri ya ndoa ya Kikristo ya mume na mke kuwa na furaha ni nini? – Utamjibu nini Mungu, siku moja utakaposimama mbele Yake? Je, kuna njia yo yote tunayoweza kuitumia kufahamu kuwa hatutakwenda jehanam? Je, una uhakika kuwa wewe ni bararaba, unaweza

kungoja hadi Siku ya Hukumu ili uweze kufahamu hatima yako itakuwa nini?
☯ ***Sikukuu za waislamu na Wakristo* -** Sikukuu zenu kubwa, Eid-ul-Adha (qorban) na Eid-ul-Fitr (mwisho wa mfungo wa Ramadhan) zina maana gani? Je, ninyi mnafahamu kwa nini sisi tunaadhimisha Sikukuu ya Pasaka, Krismas, Kupaa …? Kuna masomo mengi, ya kiroho tunayoweza kujifunza katika sikukuu hizi.
☯ ***Masuala ya maisha*** Kama maisha ya familia, malezi ya watoto wetu, ndoa za wake wengi, usafi na mazingira, athari za ushirikina, laana, uchawi wa vikope, na kadhalika. Mada zote hizi zinaweza kuwa mahali pazuri pa kuanzishia mazungumzo juu ya maudhui ya kanuni za Biblia na mifano inayotawala maisha yetu sisi kama Wakristo.

### *10. 4 Mahitaji na matamanio ya pamoja kama binadamu*

Mara nyingi unapo sikiliza Mwislamu akiuliza maswali utagundua kuwa sisi na wao tuna mahitaji ya pamoja katika kutafuta:

| | | |
|---|---|---|
| a. Amani | b. Furaha | c. Upendo |
| d. Msamaha | e. Uthibitisho | f. Ukweli |

g. Mamlaka juu ya dhambi, athari ya mambo mabaya na nguvu za giza

Haya ni mahitaji ya ndani kabisa ambayo huanzisha uwazi ndani ya roho ya binadamu, uwazi ambao anayeweza kuujaza ni muumba wetu mwenyewe tu. *(Tunayo maandiko mengi yaliyotayarishwa maalum juu ya mada nyingi zilizotajwa ambayo yanapatikana kutoka kwetu).*

### *10. 5 Hadithi zenye ujumbe maalum*

Kila mtu anapenda sana kusikia hadithi yenye kisa kizuri, hasa iwapo ataweza kujifananisha na mmojawapo wa mtu aliyetajwa katika hadithi hiyo. Mbali na vielelezo vifupi - fupi, mifano na methali iliyoandikwa katika sehemu ya nyongeza, tunazo hadithi nyingi maarufu katika vipeperushi ambavyo tungeweza kukupatia ili ushirikishe au uhadithie kwa vikundi mbali mbali vya Waislamu. (Agiza ‘Vipeperushi vya Mtumishi wa Kweli’ kutoka kwetu). Tunavyo vitabu/vipeperushi vya mada zifuatazo:
✍ *Deni la Rashid Davids* > Ni bora kukubali msamaha kuliko mtu kujitahidi kulipa mwenyewe deni lake.
✍ *Barua Iliyotoka Nchi ya Mbali* > Safari ya kijasiri ya kwenda kupokea zawadi ya ajabu kutoka kwa Mungu.
✍ *Hekima ya Shehe* > Bahati ya kupata masamaha kutoka mafuriko ya dhambi.
✍ *Sarafu ya dhahabu Isiyotoa Mlio wa Kweli* > Hatari ya kutumainia usalama na utajiri wa uongo.

- *Mauaji ya Kikatili ya El-Honouchi* > Nguvu ya chuki na furaha ya maisha yaliyo salama.
- *Kuwa Mwaminifu hadi Kifo* > Ushuhuda wa kweli wa mtu aliyehukumiwa kifo.
- *Mkusanyiko wa Hatima* > Mapitio juu ya Yerusalemu, amani na Masihi.

### *10. 6 Jinsi ya kuanzisha mazungumzo mazuri ya Kiroho*

Ø *Unafikiri nini kuhusu masihi?* Hupatikana pia katika vipeperushi. Sote twahitaji mwongozo wa kiungu ili tuweze kuvuka salama katika safari ya maisha.
Ø Tunawezaje kupata uhakika kuwa tutafika salama mwisho wa safari mahali panapotakiwa, ambapo ndipo kila mtu analilia kufika?
Ø Tofauti ni nini kati ya jamii ya Kanisa ikilinganishwa na *ummah* katika jamii ya Kiislamu?
Ø Msamaha wa kweli ni nini? Tunawezaje kuhakikisha tumesamehewa?
Ø Unawaleaje watoto wako katika jamii yenye muelekeo mkubwa wa kutokuwa na dini?
Ø Rangi na ukabila, vitu hivi vina athari gani juu ya matendo na imani zetu za dini?

Baadhi ya mada hizi, zinatoa fursa nzuri ya "kukaa mezani na kuzungumza" kwa mazungumzo ya kuzama zaidi katika mazingira ya nyumbani au mikutano iliyoandaliwa. Siyo tu kwamba vikao kama hivyo huleta mazingira mazuri ya kutoa ushuhuda katika mazungumzo, lakini vile vile kuleta mazingira ya kuelewana zaidi, na kila mmoja kueleza hadithi ya maisha yake vile vile (Soma 1Wathesalonike 2:8).




**➔*Pata muda upitie baadhi ya mada zilizopendekezwa halafu uandae mafundisho yako mwenyewe utakayotumia kushuhudia. Kadhalika kuna maswali mengine mwishoni mwa kitabu hiki kwa ajili ya matafakari ya ndani.***

# 11. Utendaji wa Uinjilisti kwa Waislamu


## *11.1 Maandalizi na Uzoefu*

Uinjilisti kwa Waislamu una kanuni tatu. Napenda kuzifananisha kanuni hizo na kigoda (kiti cha kienyeji chenye miguu mitatu). Mguu mmoja ukikosekana, kiti kinamwangusha yule aliyekikalia. Miguu hiyo ni:

***Maisha ya kiroho***

***Maarifa***

***Uzoefu***



Hakuna mguu ulio badala ya mwingine!
Tumekwisha chunguza masuala ya maarifa, ufahamu na maombi. Sasa hebu tuangalie juu ya uzoefu.
Mtu yeyote anayeanza kufanya kazi mpya hajawa mzoefu. Uzoefu hupatikana kwa vitendo. Kila mtu aliye shahidi wa Kristo alianza bila ya kuwa na uzoefu. Kwa hiyo hatunabudi kuanza mahali fulani ili tupate uzoefu.

Maandalizi, kwa upande mwingine, ni ya lazima. Bila ya kujiandaa vizuri, tunaweza kusababisha hasara badala ya faida. Maandalizi ni kujipatia maarifa kuhusu uinjilisti huo maalum. Unaposoma na kutafakari kwa makini maelezo ya kitabu hiki, na pia unapohudhuria semina ya mafunzo, unajiandaa kwa huduma hiyo.

Je, nahitaji kuwa na maarifa kiasi gani, kabla sijaweza kuwashuhdia Waislamu? Kama umesoma mwongozo ulioandikwa katika kitabu hiki na kuelewa vizuri, kwa kweli umekwisha jiandaa, laukama huwezi kuyakumbuka yote uliyosoma. Unajua ni wapi unapopaswa kutafuta majibu ya maswali utakapoulizwa. Kumbuka, unaweza kutuandikia kuhusu tatizo lolote litakalokukabili! Hivyo, uwe tayari, kisha lenga akili yako kwenda kazini.
Lakini pengine bado unauliza, “MIMI NI NANI, BWANA?” Je, ninazo sifa zinazohitajika? Kila mtumishi wa Mungu aliye mnyenyekevu ni dhahiri atauliza maswali kama hayo.
Musa aliuliza swali hilo (Kutoka 3:11), na Isaya pia (Isaya 6:5). Wote wawili

walipata kuwa watumishi waadilifu *(soma mistari inayo fuata ile iliyotajwa!).* Yeremia pia alionea mashaka uwezo wake, hadi Mungu aliopomjibu kwa uwazi (Yeremia 1:60). Hata Paulo aliuliza: "Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?" (2Wakorintho 2: 16). Na jibu lake ni:

> *"Si kwamba twatosha sisi wenyewe kufikiri neno lo lote kwamba ni letu wenyewe, bali utoshelevu wetu watoka kwa Mungu." (2Wakorintho 3:5)*


Hakuna mtu yeyote aliyekuwa na akili, uzoefu, au maisha bora ya kiroho kiasi cha kumfanya awe mwenza wa Mungu katika kazi Yake! Inanipasa nikiri kwamba hata baada ya miaka mingi ya kuwatembelea Waislamu nyumbani kwao, bado ninatetemeka ninaposimama nje ya mlango na kubisha hodi. "Je, watanipokeaje? Nitawezaje kuwashawishi wanisikilize? Watakubali kusikia?" Ni Mungu peke yake tu ndiye anayeweza kufungua mioyo ya watu. Maana "utoshelevu wetu watoka kwa Mungu."

## *11.2 Kuanzisha majadiliano*

Kabla ya kuanzisha majadiliano na Mwislamu ili tumshirikishe Injili, yatupasa kwanza tufikirie msimamo wetu kuhusu maeneo ambayo yanaweza kuleta hatari.

***Je, ni vyema kunukuu Kurani wakati tunazungumza na Waislamu?***

Kusema kweli kwa jumla, hapana! Kunukuu Kurani kutaonekana mara moja kuwa ni tishio kwa Waislamu wengi, na huenda watatuelekeza kwa "mtaalam" wao, akiwa *Shehe* au *Imamu*. Unapoonekana umebeba kitabu cha Kurani, utapokelewa kwa mashaka, kama siyo kwa uhasama. Pia kuna uwezekano mkubwa wa kutopoteza nafasi nzuri ya mazungumzo ya wazi na ya kirafiki. Katika hali fulani, hasa kwa mtu ambaye anaijua vizuri Kurani, anaweza kufaidika kwa kutumia ujuzi wake. Lakini, endapo tunafanya hilo, kwa kweli, ni lazima tuhakikishe kwamba Mwislamu hatafikiria kwamba tunaitambua Kurani kuwa nayo ni Neno la Mungu. Tunaweza kuzuia mawazo kama hayo kwa kusema: "Wewe ukiwa Mwislamu, unaamini kwamba ….."




Majadiliano yakiendelea sana wakati utafika, ambapo itakubidi uonyeshe wazi tofauti kati ya Biblia na Kurani, na upungufu uliopo katika Kurani. Maelezo

hayo yamfanya yule Mwislamu aionee mashaka imani yake mwenyewe, hali inayohitajika kabla hajaamua kukubali imani bora na iliyothibitishwa vizuri zaidi.

### *Je, ni Vyema Kuishambulia Kurani?*

Kushambulia kilicho kitakatifu, kwa Mwislamu, kusema kwa maneno yaliyopoa, ni jambo ambalo halina ladha nzuri. Lakini hanabudi afahamishwe kwamba Uislamu ni dini isiyompa wokovu wa Mungu. Ni lazima aelewe, kwamba yale anayoamini ni mambo yaliyofunuliwa, yanapingana na Biblia; pia Kurani ina matatizo mengi kuliko yale anayofikiria kwamba Biblia inayo, tena aelewe kwamba hakuna uthibitisho unaokubalika kwamba Kurani ilitoka kwa Mungu. Tunapowasilisha ukweli wa Biblia, tunasema moja kwa moja au kwa namna fulani kwamba Kurani haina uvuvio wa Mungu wa Abraham, Isaka na Yakobo, na kwamba mafundisho yake ni makosa. Tunamaanisha kwamba Muhammad siye nabii wa Mungu na Uislamu ni udanganyifu. Haya yote ni maudhi ya kukasirisha sana kwa Mwislamu, na yanaweza kabisa kufunga mlango wa ushuhuda zaidi, lakini ni kiini muhimu sana kwa uinjilisti kwa Waislamu. Hekima, mbinu na upendo katika kupangilia muda na msamiati wa kuyashuhudia hayo ni mambo muhimu sana.

Sitasahau kamwe majadiliano yangu na Mwislamu mmoja ambaye namheshimu sana. Tulipofikia mahali pa kugongana, nilimwambia kwamba yale niliyokusudia niyaseme haikosi yatamuumiza. Hata hivyo alijibu kwamba, niyaseme, kama nimeyaona kuwa ni muhimu. Kabla ya kuendelea, nilimgusa na kusema: "Nataka ufahamu, kwamba inaniumiza mimi pia ninapokuumiza wewe. Nitafanya hivyo kwa sababu tu ukweli hauna budi udhihirishwe." Nina uhakika kweli nilimuumiza, lakini kwa sababu ya maelezo yangu ya awali aliweza kunisikiliza kwa makini, na 'ukweli' huo haukuvunja uhusiano wetu.

### *Jibu kuhusu Swali: Je, Unamwonaje Muhammad?*

Je, tunalijibu namna gani swali la moja kwa moja kama: "Unaufikiria vipi Uislamu au Muhammad?"

Sijapata tatizo hata kidogo nilipojibu swali hilo kama hivi: "Mimi ni Mkristo mwenye imani thabiti. Kama mtu yeyote angeniridhisha, kwamba Uislamu ndiyo njia sahihi – na hilo ni lazima lithibitishwe na Mungu – kwa hakika nisingekuwa na sababu ya kuwa Mkristo, bali kuwa Mwislamu. Hadi leo, hakuna mtu aliyeniridhisha juu ya hilo. Unaona! Sisi tunaiamini Biblia, na katika Biblia tunaonywa tusikubali ujumbe wowote ambao hauna dhamana ya Biblia ya kuaminika, ambao ni unabii uliotimia (Soma katika Kumb. 18:21-22; Zekaria

4:9; Isaya 41:21; 44:7, 26; Amos 3:7; Yeremia 28:9; Kumb. 13:1-4, na kadhalia). Niruhusu nikupe mfano!"

Kuanzia hapo unaweza kumwonyesha Mwislamu unabii wa Agano la Kale kuhusu Yesu, kazi ambazo angefanya na jinsi ambavyo angekufa. Tunaweza kuendelea kuonyesha kwamba Kurani inakataa kusudi lenyewe la Kristo, la kuja duniani, yaani kifo chake msalabani kwa ajili ya kutupatanisha na Mungu Baba. Je, unafikiri nitakubali lipi – lile lililotabiriwa na manabii wengi wa Biblia kwa muda wa karne nyingi, walioeleza hata mambo madogo madogo yaliyo tendeka na kushuhudiwa katika maandiko ya watu wanne, pamoja na wengine walioyaona kwa macho yao na ambao maisha yao ya milele yalitegemea ukweli wa ushuhuda wao, yaliyothibitishwa pia kwa utaalam wa kihistoria na utafiti wa mambo ya kale – au lile lililoandikwa na mtu mmoja tu, karne sita baadaye, katika kitabu kisicho na unabii wo wote?" Inawezekana kutoka hapo utapata nafasi yenye faida ya kulinganisha imani zetu zilivyo, pamoja na sababu zake.

***Kutamka "Bwana Yesu" na "Nabii Muhammad"***

Je, tunayatamkaje majina hayo? Je, Yesu Kristo ni Bwana wa Mwislamu? Na, je, Muhammad ni nabii wako? Tayari maswali haya yanatoa majibu. Ninapozungumza na Bwana wangu katika sala, na tunapo zungumza habari zake kati yetu sisi Wakristo, tunatamka jina hilo: "Bwana Yesu". Lakini ninapo ongea na watu wasio Wakristo, napenda kumwita "Yesu Kristo" au "Yesu Masihi". Vile vile, simwiti Muhammad 'nabii" kwa sababu siamini ya kuwa yeye ni nabii kwa mujibu wa maelezo ya Biblia kuhusu nabii.

***Mkristo ni Mtu kutoka Nchi za Magharibi?***

Kwa kawaida, Waislamu wanapima imani ya Kikristo kufuatana na maisha ya "Wakristo", yaani wote wasio Wayahudi, Waislamu au wapagani. Wanafikiri kwamba maisha ya watu wa Magharibi, wenye kukosa maadili, walevi wa pombe, wanaotaka kutawala nchi nyingine, kuharibika kwa maisha ya familia, na kadhalika, ni matokeo ya Ukristo. **Ni muhimu sana kueleza wazi kwamba Mkristo ni mtu anayemfuata Kristo**, na kwamba mambo yaliyo mengi katika filamu za ki-Marekani si ya ki-kimaadili wala ya ki-Kristo.

Lakini pia inatupasa kueleza kwamba imani yetu haina orodha ndefu ya mambo tunayo ruhusiwa na orodha ndefu ya mambo tunayokatazwa kufanya. Kwa Mwislamu, kitabu kiitwacho *"Mambo ya Kutenda na Kutotenda katika Uislamu"* kina umuhimu mkubwa, kwa sababu anakitegemea kitamsaidia afike mbinguni. Wakristo hawana haja ya kujipatia wokovu wao, bali hutenda mema kwa sababu wanampenda Mungu na mapenzi yake, na kumshukuru Kristo kwa

kifo chake msalabani kwa ajili ya dhambi zao. Tunatakiwa tufikie maamuzi yetu ya ki-maadili sisi wenyewe. Wakristo tofauti wanaweza kufikia maamuzi tofauti. Wala hatulazimiki kufuata utaratibu ule ule wa maisha na ibada, kwa sababu kila mtu anaishi kwa upekee wake mbele za Mungu, kwa hiyo hatuwezi kufanana kabisa – na tofauti zetu za maumbile zina makusudi yake.

***Je, ni Lazima Tujiepushe na Mahojiano Kuhusu Dini?***

Wakristo wengi hutuonya kila mara kwamba haifai kufanya mahojiano kuhusu masuala ya kiroho.

Paulo hakufikiri hivyo.

> *"Alinena na kuhojiana na Wayahudi na Wayunani (Matendo 9:29).*
>
> *"Akahojiana nao kwa maneno ya maandiko sabato tatu, akiyafunua na kuyaeleza …" (Matendo 17:2)*
>
> *"Akayojiana na Wayahudi na waliomcha Mungu, na wale waliokutana naye sokoni kila siku." (Matendo 17:17)*
>
> *"Akatoa hoja zake katika sinagogi kila sabato, akajaribu kuwavuta …" (Matendo 18:4). "Akaingia katika sinagogi, akahojiana na Wayahudi." (Matendo 18:19)*
>
> *"Akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu." (Matendo 19:8).*

Neno hilo 'kuhojiana' kwa Kiyunani ni 'dialegomai', maana yake kujadiliana, kusikiliza maoni ya wengine na kuyafafanua. Hayo ni mazuri. Lakini haifai kubishana na Waislamu kuhusu Mungu wala Biblia, kama lengo la mabishana ni mashindano.

## *11. 3 Kushuhudia Wanawake na Watoto wa Kiislamu*

Waafrika wana methali isemayo: "Mwanamke hana dini." Methali hii ina maana ya kwamba lazima mwanamke atafuata dini ya mume wake kama ilivyo imani na mapokeo yake. Kama anatambua au la. Lakini fikra hizi zimewapotosha wamisionari na viongozi wa makanisa, vile vile. Ziliwafanya kulenga juhudi zao kubwa kwa wanaume tu wakiwa kama vichwa wa nyumba, na viongozi wa jamii. Kwa kufanya hivyo, walianzisha "umisionari-kipofu-kijinsia" na kufanya kosa baya la kushindwa kukamata mapigo ya moyo wa jamii ya Kiislamu.

Wanawake wa Kiislamu, haidhuru wawe wamesoma au hawakusoma, wawe huru au wameokoka, hawatafuata waume zao bila kufikiria, kama kwa kufanya hivyo wataingia Ukristo.

**Kupima Mahitaji ya Ndani ya Mwanamke wa Kiislamu**

**Hitaji la kwanza** bila shaka, ni mapenzi ya mume wake, ambayo anataka ayapate peke yake, na kwa ajili ya manufaa yake mwenyewe tu. Kwa hivyo, ni jambo muhimu sana kwamba anampatia mume wake watoto kama anaopenda (hasa watoto wa kiume). Mke wa Kiislamu anajaribu kujitoa kwa ukamilfu ili kuona kwamba mume wake anatosheka naye, lakini ni kwa nadra sana kufanikiwa.



Mume – ambaye anapewa uhuru wa kiroho usio na mipaka katika Uislamu – mara nyingi anashawishika kufikiria kwa mapana zaidi kuhusu ndoa ya mke mmoja; kutosheka na mke mmoja tu litakuwa kichekesho kwa "wanaume halisi" wengi katika ulimwengu wa Kiislamu. Hamu kubwa ya mke kudhibiti mapenzi ya mume wake kwa gharama yoyote mara nyingi huleta matokeo kinyume. ('Hata usithubutu ikuingie akilini mwako ya kwamba utakuwa ni wewe peke yako').

**Hitaji jingine la ndani** ni utashi wake wa **kutaka kutambuliwa kijamii**.
Mara nyingi sura ya nje ndiyo hushika jukumu la kulazimisha: mavazi/mapambo, vidani, mitindo ya nywele, na kadhalika. Kwani hayo ndio dalili zinazoonyesha kwa kila mtu wa karibu naye ni jinsi gani mume wake "anavyompenda" na kumjali. Lakini dalili hizi si aghalabu kulingana na ukweli wenyewe, kwa hivyo baadhi ya akina mama wanaingia madeni ili waonekane wanapendeza wakati wote. Lakini, ndani ya nyumba yake, ukweli hauwezi kuepukwa; na pindi mume anapochukua mke mwingine, mke wa kwanza amepata jeraha kubwa moyoni. Heshima yake binafsi imepata mtikisiko mkubwa, na atafanya kila jitahada ya kujaribu kulificha jambo hilo kwa majirani na marafiki zake.
Lakini hofu kubwa kushinda vyote ya mama wa Kiislamu ni ile ya kupewa talaka. Kwani, endapo hilo likitokea, atanyang'anywa watoto wake, nyumba yake na heshima yake katika jamii; na atajiona hata paradiso imesukumwa mbali naye. Kwa sababu amekuwa akiambiwa neno lile lile mara kwa mara: *"Ni utii kamili kwa mume wako tu ndio hukupa uhakika wa kuingia paradiso" (soma Vikwazo Katika Uinjilisti kwa Waislamu).*
Furaha ya mwanamke yeyote wa Kiislamu (mwenye elimu au asiyesoma) inategemea sana juu ya kutimilizwa kwa mahitaji hayo, na mwanamke wa Kiislamu atakwenda mapana na marefu ili kuyapata mahitaji hayo.

***Mawe ya Vianzio au Madaraja ya Kuhubiria Wanawake wa Kiislamu***


Kwa kawaida wanawake wa Kiislamu hawajishughulishi sana kufuata “imani sahihi”, za maandiko ya dini yao. Hujishughulisha zaidi na jinsi gani watakavyopata mafanikio katika mapambano yao ya kumudu maisha ya kila siku.

Wanawake wa Kiislamu:

- ☐ Haja yao kubwa ni kupendwa, kutambuliwa na kukubaliwa.
- ☐ Wanapenda kuwa na waume waaminifu, na watiifu, au vyema zaidi, watoto waliopata mafanikio.
- ☐ Hawapendi kabisa kupewa talaka, au kulazimishwa kumvumilia mke mwenza.
- ☐ Wanaogopa kupoteza vyeo vyao, heshima na haiba.
- ☐ Wanaogopa sana nguvu ya ‘uchawi wa mapenzi’, ‘uchawi wa vikope’ wa majirani zao au ndugu.
- ☐ Wanaogopa sana tabia ya utetaji katika jamii na aibu inayoweza kuletwa ndani ya familia na tabia hiyo.
- ☐ Wanaogopa magonjwa, vifo au ulemavu wa watoto au ndugu.
- ☐ Wanaomba Mungu awe karibu nao, awaguse, awapatie uponyaji katika maumivu yao, na wasafishwe.
- ☐ Wanapenda sana kuelewa mambo mengi kuhusu dini yao, maisha au Vitabu Vitakatifu.
- ☐ Wangependa kusikiliza mara nyingi Neno la Mungu, Biblia na hadithi zake za kweli za maisha – lakini hawapendi jambo hili lijulikane.

Wanawake Wakristo wana nafasi nzuri sana ya kushirikiana maisha yao na wanawake wa Kiislamu katika sehemu zile ambazo Wakristo na Waislamu wanaishi pamoja. Ikiwa kama wanawake wa Kikristo watawaangalia hawa “Mabinti wa Abraham” kwa macho ya upendo, kujenga uhusiano pamoja nao halitakuwa jambo gumu, mara tu litazaa matunda, na wanawake wa Kiislamu wataanza kuwauliza wanawake wa Kikristo maswali kama haya:

- ❁ Mke wa Kikristo anatumia uchawi gani wa kumweka mume wake daima kuwa mwaminifu kwak ?
- ❁ Kwa nini mwanamke Mkristo hana hofu ya mambo kama haya ya “uchawi wa wivu” au “uchawi wa vikope’ wa majirani zao?
- ❁ Ni jinsi gani unavyoweza kuwa na uhakika wa kupata masamaha na kwenda mbinguni unapofariki?




***(Vikwazo: vya kiuchumi, kisaikolojia, kidini na kijamii).***

***Kutumia hadithi kama njia ya upole ya kufikia Mioyo ya Wanawake***

Wanapokuwa katika mazingira ya mapokeo ya asili, wanawake wa Kiislamu hupenda sana kusikiliza hadithi zilizorithiwa kutoka kizazi hadi kizazi kutoka kwa wakuu wao wa dini, haidhuru wawe wanawake au wanaume. Hasa wanapenda hadithi zenye matumaini. Kwa hivyo hakikisha umejizatiti kwa hadithi nzuri zilizosheheni ukweli na maana kwa maisha ya majirani zako Waislamu na marafiki.

Hunabudi kukumbuka, kila mara kwamba Waislamu wanasikiliza kwa hiyari hadithi za Maandiko yaliyofunuliwa. Kinacho hitajiwa ni kuwa jasiri katika kushirikiana nao Hadithi ya Mungu.

***Mawasiliano kwa kutumia Hadithi za Biblia***

Biblia ina hadithi nzuri ajabu ambazo wanawake (Waislamu) wanaweza kuzielewa kwa urahisi kama:

- ⌘ Magomvi na migogoro katika nyumba zenye wake wawili: Lea na Rahel (Mwanzo 29), Hannah na Peninah (1Sam. 1 + 2).
- ⌘ Hisia ya kuona ni hasara kubwa kukosa watoto – Rebeka na Hannah.
- ⌘ Kukosa usalama na wasiwasi katika maisha ya ukimbizi – Hagai (Mwanzo 16).
- ⌘ Mama anayejikaza baada ya kupoteza watoto – Kaini na Habil (Mwanzo 4).
- ⌘ Matatizo kati ya mume na mke yaliyosababishwa na upendeleo katika familia – Esau na Yakobo, Yakobo na Yusufu.
- ⌘ Kujiweka sawa katika maisha ukiwa na mlemavu au mtoto mwenye matatizo – Mefibosheth (2 Sam 9).

Haya ni miongoni mwa matatizo yale yaliyozoeleka kwa akina mama wengi wa Kiislamu, lakini ni nadra sana kwao kupata msaada wowote wa majibu kwa vitendawili hivi vya maisha. Mara nyingi huwa hawafahamu njia yoyote nyingine isipokuwa kuzuru makaburi ya (Waislamu) watakatifu, kwenda kuomba msada kutoka kwa wachawi, sangoma au vyanzo vyeusi vinginevyo. Je, kwa nini sisi tukose mengi ya kuwasaidia!

**Kuhubiria Watoto wa Kiislamu**

Jamii za Kiislamu zinawalinda sana watoto wao. Kinababa, wajomba, kaka wakubwa huangalia kwa makini tabia za watoto wao wadogo na hasa wasichana. Katika nchi za Afrika kusini ya Sahara hatuna shule nyingi za Kiislamu. Shule nyingi ni za mchanganyiko, watoto wa Kiislamu na watoto wa Kikristo wana uhuru wa kushirikiana katika mambo mbali mbali. Baadhi ya shule zina mfumo wa mikondo miwili ya EDK – Elimu ya Dini ya Kikristo na Elimu

ya Dini ya Kiislamu. Lakini katika sehemu nyingi kuna waalimu wachache tu wa Kiislamu na wa Kikristo ndio wanaofundisha wanafunzi wa Kiislamu katika vipindi vya dini. Wazazi (Waislamu) wako radhi kukubaliana na hilo kwa sababu haja yao ni watoto wao wapate elimu nzuri. Kwa hivyo hawana haja ya kujali kama kuna athari za Ukristo.

***Waumini watu wazima wengi waliokuwa Waislamu wametoa shuhuda kwamba hamu yao ya kupata ukweli ilianzia wakati wa miaka ile walipokuwa shuleni.***

Tangu wanapokuwa na umri mdogo wa miaka minne hivi watoto wanapelekwa kwenye madrassa, ambako wanafundishwa Uislamu na elimu ya msingi ya Kiarabu. Katika elimu hiyo mkazo mkubwa unawekwa juu ya uhodari wa kusoma vizuri, na kila mtoto wa Kiislamu anatazamiwa awe anajua kukariri Kurani, hata kama Kiarabu si lugha yao ya asili. Kupitia elimu wanayopata kwenye madarasa hayo wanajengewa mazowea ya itikadi za Kiislamu, desturi, ibada na jinsi ya kuishi kama Waislamu. Lakini vile vile mara nyingi, watoto wa Kiislamu hujazwa propaganda ya kupinga Ukristo tangu utoto wao na kuendelea, ili kuwalinda wasiambukizwe imani ya Kikristo hata kidogo.

Lakini hayo yote yasituvunje moyo tukaacha kutafuta uwezekano wa kushiriki Injili na watoto kutoka nyumba za Waislamu kila inapowezekana. Waalimu wa Kikristo wana nafasi nzuri wakati wanapofundisha vipindi vya elimu ya dini kuwashirikisha watoto wa Kiislamu ukweli wa Biblia. Kama watakuwa ni mahodari wa kufundisha hadithi za Biblia kwa namna ya kuvutia, basi wanafunzi wataaza kuwaamini waalimu wao na kuanza kupenda Biblia, upenzi ambao watakuwa nao maisha yao yote.

Pengine, watoto huruhusiwa kujiunga na Shule za Jumapili au Vilabu vya Biblia vilivyo karibu na nyumbani kwao. Wanayoyaona huko yanaweza pia kujenga mapenzi ya kupenda nyimbo za Kikristo, kupenda hadithi za Biblia na hivyo kutayarisha medani ya kukua kwa uwazi wa kupenda Injili katika siku za usoni wanapokutana na Wakristo.

Lingekuwa jambo zuri sana kama Kanisa lingekuwa linasaidia viongozi wa vikundi hivyo, kule ambako watoto wa Kiislamu wanashirikiana na watoto wa Kikristo, kuwaombea, kuwa tayari kutoa ushauri na mafunzo, au kusaidia kutayarisha mashindano ya michezo au burudani za aina mbambali. Wakati huo huo, ni jambo muhimu kuhamasisha watoto wa Kikristo kuonyesha upendo kwa marafiki zao wa Kiislamu, wawakaribishe kucheza nao pamoja na kuwakaribisha


kutembelea nyumbani kwao. Kule tu kuangalia maisha ya familia ya Kikristo na kulinganisha maisha yao na maisha yalivyo nyumbani kwao kunaweza kuwa ni ushuhuda mkubwa kwa watoto wa Kiislamu na msaada mkubwa kwao kujenga itikadi zao zitakazowasaidia kufanya uchaguzi wa busara siku za usoni.

Nafasi za kuwahubiria watoto wa Kiislamu ni nyingi mno, kama vile:

a. ***Vilabu vya Biblia vya Wakati wa Likizo*** inaweza kuwa njia maalum kabisa kutumika kwa mahubiri. Hutokea mara nyingi kwamba wazazi wote wawili ni wafanyakazi, hivyo wataona furaha endapo watoto wao watapata 'malezi ya mchana' ya aina fulani.

b. ***Kuimba*** kuna mvuto wa ajabu sana kwa watoto. Kuimba kunafaa kufanywa ndiyo sehemu nzuri ya program ya kuingiza ukweli wa Biblia katika akili za watoto, wakati wanapoimba nyimbo za Yesu nyumbani kwao tayari watakuwa wanahubiri.

c. ***Hadithi za Biblia*** hazinabudi kusimuliwa kwa lugha nyepesi inayoeleweka kwa urahisi, na 'msamiati wa kiroho' haunabudi kuepukwa. Kama hadithi za Biblia zinatofautiana na hadihi za Kiislamu, usiwe na haja ya kuingia katika majadiliano makubwa juu yake … tafuta jibu la swali mtoto alilouliza, kisha baadaye mjibu katika mazungumzo ya binafsi ya ana kwa ana.



d. ***Maigizo hadithi*** ziwekwe katika mfumo wa maigizo yanayowajumuisha watoto ili waone jinsi wanavyohusika. Tumia vielelezo vya picha na vielelezo vingine vya kuyafanya masomo hayo yawe rahisi kukumbukwa.

e. Wafundishe kukariri ***aya za Biblia*** kwa kichwa. Watoto wa Kiislamu wamezoezwa kukariri, kwa njia hiyo, hazina itakuwa imehifadhiwa katika mioyo yao.

f. ***Unaposali*** pamoja na watoto sema na Mungu kama "Baba yetu" na baadaye kabisa ndipo uwatamkie "Yesu" katika sala zenu. Unaposali, siyo lazima ufumbe macho huku umesimama, na inawezekana kusali hata bila ya kufumba mikono.

g. ***Beba Biblia kwa Uangalifu***: ili watoto waweze kuona jinsi gani unavyoki-

heshimu kitabu hicho: lakini pia kitendo hicho kiwe tabia yako na mtindo wako wa maisha. Usithubutu kuweka chini Biblia kwa dharau.

h. ***Usiweke shinikizo lolote:*** kwa watoto kumkubali Yesu kama Mwokozi wao, wape muda na uhuru wa kuchagua kama watapenda kuwa Wakristo. Wanapokuwa watu wazima, hasa wakati ule wa kubalehe au kuvunja ungo, mara nyingi huwa hawaruhusiwi tena kwenda kwenye Shule za Jumapili au Vilabu vya Biblia. Kwa hivyo ule wakati wanapokuwa watoto ndio wakati mzuri wa kuwafunulia ujumbe wa Injili.

*Kama mtoto atapenda kumfuata Kristo* uhakikishe ameelewa kuwa Mkristo maana yake nini, na ile inayoitwa "njia iliyonyooka" pamoja na Kristo ina sura gani. (Kusoma Neno la Mungu, kuabudu, kushirikiana na waumini kufanya maombezi).
Lakini pia wanahitaji kufahamishwa, kuwa ni lazima watakabiliwa na magumu, majaribu na upinzani katika njia yao.
Hakikisha unampatia mtoto tafsiri sanifu ya Biblia ambayo inaeleweka kwa urahisi (siyo ile ya "thee" na "thou") na shuleni usisitize wahudhurie kipindi cha ibada au vikao vingine kama Umoja wa Maandiko Scripture Union au matukio mengineyo, ambapo mtoto anaweza kukua na kupanua ufahamu wake wa Neno la Mungu.

## *11.4 Jinsi ya Kumuongoza Mwislamu Muongofu*

***Ushuhda na kuongoka***

> *"Hakuna awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba aliyenipeleka." Yohana 6:44).*

Tunaweza kushuhudia Injili, lakini hatuwezi kumwongoa mtu! Hata hivyo, ushuhuda wetu hakika unalenga kumsaidia na kumkaribisha mtu ampe Mungu maisha yake – kwa njia ya ki-Biblia.
Kumsukuma au kumlazimisha mtu aongoke ni kazi ya ki-kibinadamu au ya kimwili, lakini mtu akiwa amejifunza na kuelewa Injili kiasi cha kutosha, lazima afahamishwe haja ya kujitoa, na kukaribishwa afanye hivyo.

***Kuongoka na Kumfuata Kristo***

Tunatazamia uamuzi wa kumfuata Kristo hata Waislamu. Lakini huweza kutokea pole pole si ghafla kama unavyotazamiwa katika mikutano ya Injili. Uamuzi unafikiwa pale ambapo Mwislamu amekubali madai ya Kristo kwamba yeye kweli ndiye Mwana wa Mungu, aliyekufa kwa ajili ya dhambi zake binafsi. Hapo ndipo anapokubali kupokea karama ya Mungu, yaani masamaha na

maisha mapya kutokana na kifo cha Kristo msalabani. Ingawa kukubali kwake pengine kutatofautiana na vile 'tulivyozoea' lakini ukweli wa imani lazima ubaki kama ulivyo katika Biblia. Haikosi kutakuwapo na maswali machache ya wazi.

Lakini, maswali hayo siyo ya msingi, hakuna haja ya kuyahangaikia bali tuombe kwamba Neno la Mungu litoe jibu linalo takiwa. Roho Mtakatifu atamwongoza.

Hata hivyo, kadiri vile tunapo sikiliza shuhuda kadhaa za waongofu waliokuwa Waislamu, na kuzielewa njia za Mungu jinsi anavyowavuta kwake watu, tunaweza kubaini masharti kadhaa ya kuongoka.

**MASHARTI 5 YA WOKOVU YENYE NGUVU**

1. **Mtu aitwaye Yesu** - ***anapendeza!***
2. **Kukutana na Ukweli** - ***Nimepata ukweli ninaoweza kuuamini.***
3. **Jamii ya Kanisa** - ***Hawa ni watu ninaoweza kuwaamini.***
4. **Haja ya kupata msamaha** - ***Nimejaribu katika maisha yangu yote; sasa nafahamu.***
5. **Kukutana binafsi na Mungu** - ***Nataka Mungu aliye karibu; Mungu anayenisikiliza ninapoabudu.***

*Chanzo: Called from Islamu to Christiaity Kitabu kilichotungwa na Jean-Marie Gaudeul*

Mara Mwislamu akiisha kukiri imani yake na kujitoa kwa Mungu kwa kumpokea Kristo kama Mwokozi na Bwana wake, baba/mama huyu anahitaji kufundishwa jinsi ya kuwa mwanafunzi wa Yesu. Kwanza kabisa, hii maana yake atayarishiwe ratiba ya masomo ya kimsingi kuhusu imani ya Kikristo na itekelezwe. Kwa mujibu wa kanuni, tunapendekeza kwa nguvu hilo lifanyike katika 'kanisa la nyumbani' au kwa mafunzo mengineyo yoyote yasiyo rasmi. Hapa huyo mwongofu atajifunza juu ya imani na kazi yake, na kadhalika. Atazoezwa pia juu ya taratibu za Kikristo za kuabudu ambazo zinatofautiana sana na zile za Kiislamu. Atafundishwa kwa mara ya kwanza jinsi ya kuabudu kwa kuimba. Mwalimu mwenye hekima atafanya kwa uangalifu mkubwa kueleza na kuelekeza kila kitu kipya, na vile vile atahakikisha anamwonyesha asili yake ya ki-Biblia.

Maana ya ubatizo hainabudi kuelezwa kinaganaga bila ya kumshinikiza muumini huyu mchanga. Ubatizo ndiyo itakuwa hatua kubwa kwa mama au baba huyu!

### *Kujifunza Kutembea na Yesu Siku kwa Siku*

Baada ya uamuzi haina maana kwamba kazi imekwisha. Muumini huyu mchanga anahitaji marafiki Wakristo wa karibu kusimama sanjari pamoja naye, kumsaidia na kushauri. Afanyeje nyumbani kwao? Atawaambiaje ndugu zake kwamba sasa amempokea Mwokozi? Afanyeje pindi anapokataliwa na kuteswa? Je, sasa anaweza kuanza kula nyama ya nguruwe? Je, mfungo nao? Nazo ibada za kawaida? Ushauri wa kufaa ulio komaa haunabudi kutolewa pale maswali na matatizo yanapojiokeza. Muumini mpya anahitaji kuambatana na mtu mwenye uzoefu katika mwenendo mpya wa maisha yake pamoja na Kristo. Anahitaji kutegemezwa kwa maombi na pia kufundishwa Maandiko. Anahitaji sana msaada wa kuona ulimwengu mpya ambao ataishi ndani yake, kwani ule wa zamani na familia yake itakuwa imemkataa. Yote yamevunjika kabisa. Ufahamu, fadhili na utunzaji wake binafsi unahitajika kwa muda mrefu hadi atakapokuwa mtume mwaminifu.

### *Muumini Mpya na Kanisa*

*"Kanisa letu limekuwa nyumbani kwa Wakristo waliokuwa Waislamu"*……… ndiyo ingepaswa kuwa kauli mbiu ya kila jumuiya ya kanisa. Lakini kama ni kanuni ya jumla, tusifanye haraka kumkaribisha Mwislamu ahudhurie ibada au mikutano makanisani, kwa sababu Mwislamu aliyekuwa anafuata utaratibu wa dini yake anahitaji "mawe ya kuvukia" aweze kutoka kwenye mazoea ya msikiti na kuingia kanisani, na kufahamu yale yanayofanyika.

Je, umewahi kuhudhduria ibada ya Ijumaa msikitini? Huenda bado hujapata nafasi. Lakini kama umefanya hivyo, ni lazima umejiona huna usalama na umetoka ukiwa na maswali mengi. Siku moja nilipokuwa na zamu ya kutoa hotuba kanisani, ilinipasa nimwambie mgeni Mwislamu aliyetutembelea nyumbani kwetu kwamba nilikuwa natakiwa niondoke. Akiwa katika hali ya udadisi, aliniuliza kama ningeweza kwenda pamoja naye. Bila shaka nilikubali! Hivyo, tukafuatana. Lakini tulipofika Kanisani alijibana kwenye kiti nyuma kabisa karibu na mlango wa kutokea. Na, baadaye alikiri kwamba alikuwa anaogopa wakati wote na kujisikia haja ya kukimbia atoke nje ya Kanisa.




"Kanisa la nyumbani" au kikundi kidogo cha maombezi chenye watu wenye uzoefu na wenye huruma, vyema zaidi wak-

**Mawe ya Kuvukia**

Nyumbani
Maombezi
Masomo ya mtu mmoja mmoja

iwa wametoka kwenye Uislamu ingekuwa ndilo 'jiwe la kuvukia'. Ni hapa, yule anayetarajiwa kuwa mwongofu au mwongofu kijana angepitia misingi ya Biblia akisaidiwa na Wakristo waliokomaa. Anaweza kujifunza, hatua kwa hatua kwa kuangalia jinsi tunavyoabudu na kuimba na tunafanyaje katika ibada zetu. Lakini hili "kanisa la nyumbani" lisigeuzwe kuwa mkutano wa Injili! Bali iwe ni mahali pa kumshauri mwongofu mpya kwa njia isiyo rasmi ni kwa ajili ya nani na kwa faida ya nani angekata shauri.

### *Mwongofu Anayekabiliwa na Kukataliwa*

Takriban kila Mwislamu anayemgeukia Kristo kwa ajili ya kupata wokovu, anakabiliwa na kukataliwa na ndugu, marafiki, na bila shaka, na jamii nzima *(Umma)* ya Kiislamu. Kwa hiyo, inatupasa kama Kanisa, au kikundi cha waumini waliomwongoza hadi kufikia uamuzi wa kuongoka, kumpokea na kuwa jamii na ndugu zake wapya. Wala si kwa muda wa majuma machache tu, la! Anahitaji msaada wetu hadi hapo atakapokomaa katika imani na kutulia katika familia ya Mungu.

## *11.5 Kanuni Nyingine Zenye Msaada katika Mawasiliano Yetu na Waislamu*

NJIA BORA ZA KUWAFIKIA WAISLAMU ni kama zile za kawaida za kushirikiana na watu wengine, na nafasi zitakuwa nyingi mara tutakapozishinda hofu zetu za kuwafanya Waislamu kuwa marafiki zetu. Kwanza kabisa, tufahamu ya kwamba Waislamu pia ni watu wenye mahitaji sawa na watu wengine, na hayo yanajumuisha na matamanio ya kukubaliwa bila kuonewa mashaka na kupendwa. Urafiki wa kijuu juu hautoshi; ushirikiano wa kina ndio utakaoleta hiyari ya kufunguka pale ambapo panauma kweli.

Lakini kanisa linaweza (kutumaini) kuamua kuanzisha utaratibu mzuri wa mfululizo wa kutembelea nyumba zote za Waislamu katika eneo lake. Tungeweza kuita aina hii *"huduma ya maombi nyumba kwa nyumba."*. Hii si njia ya kawaida ya kuwaendea Waislamu, kwa hivyo mtu hanabudi kujitambulisha mwenyewe na kujieleza sababu ya ujio wake. Hapo chaguo ni kati ya kuwaendea kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia nyingine. *"Sisi tunafanya utafiti wa dini katika eneo hili na tunakuomba kwa ukarimu utupatie dakika chache kujibu "dodoso"*

*letu. Dodoso* lililoandaliwa kwa uangalifu linaweza kuamsha maswali mengine kwa upande wao na hata kutoa nafasi kwa ushuhuda uletao matunda. Lakini, mara nyingi inafaa kwanza kujenga uhusiano na jamii ya Kiislamu kwa muda kabla ya kuuliza maswali kama hayo, kwa sababu nyingi. *(Madodoso kama yaliyotajwa yaweza kupatikana kwa kuagizwa kutoka ofisi zetu).*



Wakristo wasio na uzoefu wanaweza kutumia *maandiko maalum* yaliyotayarishwa kwa ajili ya Waislamu, au kuwakaribisha kuona video ya Kikristo itakayo wafaa. Kwa wengine, ambao wana uzoefu kidogo, wanaweza kutembelea nyumba fulani kwa ajili ya kuanzisha *matafakari ya kila siku ya kifamilia.* Waislamu wataonyesha ya kwamba na wao pia wana utaratibu wa sala za kila siku. Kwa kweli tunastahili kuwapongeza kwa kitendo hicho cha matafakari, lakini jibu letu liwe kwamba kwa kweli hatuna maana ya kutimiza masharti ya *Salat*, lakini nia yetu sisi ni matafakari ambayo yana sehemu mbili – kwanza, kusikiliza Neno la Mungu, na pili ni majibu yetu juu ya hilo kwa kufanya sala ya binafsi na utii. Waislamu watajibu kwamba wao wanasoma Kurani. Tuulize: "Je, unasoma Kurani kila siku?" Jibu ni: "Hapana. Si kila siku". Tayari hapo sasa mtu atakuwa tayari yumo katika mazungumzo ya kiroho.

Njia nyingine ya moja kwa moja ni kuuliza: *"Je, unafahamu kutatokea nini kwako kama ungefariki leo?" au, "Mathalan kama umefikia wakati wa kufariki kwako na kusimama mbele za Mungu, je, unazo sababu gani za kumtazamia Yeye akuruhusu wewe kuingia mbingun ?"* Mkabala kama huu kwa upande wetu ni sawa na kufungua mlango kwa mazungumzo ya kiroho.

**Wakristo wenye mapenzi wataweza kufikiri njia nyingi nyingine za kunyoosha mikono**

KUULIZA MASWALI ni njia nzuri sana ya kuanzisha mazungumzo. Kwanza kabisa, watu wengi hujisikia vizuri wanapokaribishwa wajieleze, hisia zao, mazingira na imani zao. Kusikiliza kwa hakika ni sehemu muhimu sana ya mazungumzo. Kumshushia mtu mwingine mabomu ya ujumbe au hata kumsomea aya za Biblia kutawasukuma na kuwaweka katika nafasi ya kujihami, au, hilo ni sawa na kutoa mwaliko wa makabiliano ambayo hayahitajiki hapa. Lakini pia

kunyesha mvua ya maswali mara moja, nako hakusaidii sana, kwani ni rahisi watu kukufikiria kwamba wewe ni mrakibu wa polisi!

Maswali yanayoulizwa hayanabudi yawe yamelenga kuendeleza mazungumzo ya kiroho, kama maswali yafuatayo:

- *"Nasikia (au nimeona) kwamba unasali mara tano kwa siku. Kwa nini unafanya hivyo? Kwa nini kila mtu anafanya matendo hayo hayo? Je, ukisha sali maneno hayo mara 10,000 bado unaweza kuona maana ya kiroho ndani yake? Je, hayo si mazoea tu?"*
- *"Nasikia (au nimeona) kwamba mnatoa dhabihu. Je, mnafanya hivyo kwa njia zile zile na kwa makusudi yale yale jinsi Mungu alivyowaamuru Abraham na Musa? Je, huo utoaji wa dhabihu una malengo gani?*
- *Waislamu wanaamini kwamba Uislamu ni dini ya Abraham. Kwa njia gani?*
- *"Je, umeshakwenda Maka kuhiji (Hajj)? Je inaonekanaje kuwako huko katika mkusanyiko wa maelfu ya Waislamu wengine? Je, safari hii si gharama kubwa kifedha? Kwa nini mnabusu lile jiwe jeusi ndani ya Ka'aba? Sisi tungeliona hilo ni sawa na kitendo cha kuabudu sanamu. Ingawa Muhammad, alianzisha dini mpya katika Bara la Uarabu, kwa nini hakuondoa ibada zote za sanamu?*

Ni dhahiri yule anayeuliza maswali hanabudi mwenye awe anafahamu majibu yake ya ki-Biblia! Maswali yapo mengi, yasiyo na mwisho. Lakini kila swali halinabudi kuulizwa kwa kusudi maalum, kiasi cha kumfanya rafiki wa Kiislamu aanze kufikiri! Na vile vile, kulinganisha!

Bila shaka hakuna uchawi wowote katika kuhubiri! Waislamu pengine husema, tuacheni na mambo yetu, ingawa hii haitokei mara nyingi. Wanapojibu maswali yetu, *jibu moja huibua swali jingine. Biblia inatufundisha kwamba ....."* na sasa tumepata nafasi ya kuwashirikisha Neno la Mungu.

KUONGOZA MAZUNGUMZO mara nyingi ni lazima. Waislamu wana tabia ya kubadilisha hoja kila wanapoona wametingwa, na njia ya kujihami ni kushambulia Biblia. Wanapoanza kuuliza maswali yasiyohusika bila ya kuwa tayari kusikiliza majibu, inatubidi turudishe mazungumzo mahali penye mada, la sivyo yatageuka kuwa mabishano ya kipumbavu. (2Timotheo 2 : 23 – 26)

HISIA ni dhahiri zitalipuka mara Waislamu wanaposhambulia Maandiko Matakatifu au Yesu Kristo. Ni katika hali hiyo hasa, tunatakiwa tusihamaki. Mtu

hana sababu yoyote ya kukasirika. Hasira haitendi jambo jema. Hakuna faida yoyote wakati jazba zimepanda katika mabishano yasiyo na maana. Bila ya shaka baadhi ya hoja za Kiislamu zina lengo la kutukasirisha. Lakini tunapaswa kutawaliwa na Roho ili tuenende kama Kristo.

KUTUMIA VIELELEZO ni muhimu sana. Si watu wengi wanaoweza kuelewa fikra bila ya vielelezo. Katika tamaduni nyingine, lugha inayotumiwa ni ya ki-mifano au ki-ishara. Karibuni maelezo yote ya fikra na maelezo ya kiroho ndivyo yalivyo – yanahitaji kuimarishwa kwa kutumia methali, mifano na mafumbo. Bwana wetu Yesu alitumia mifano, methali kama sheria kila alipofundisha. Jambo hili halinabudi kututia moyo sisi vile vile kufanya kama alivyofanya Yeye, lakini tujifunze kutumia vielelezo, methali na hadithi kufuatana na mazingira ya maisha ya wasikilizaji wetu. (*Mifano mingi imeandikwa katika nyongeza. Haikosi unafahamu mifano mingine. Tafadhali, hebu pata muda wa kukaa chini na kutuletea ili nasi tuweze kuwafikishia wengine. )*


**Mkulima alitoka ……**


MBINU NA UFAHAMU na njia za busara hazina haja ya kusisitizwa zaidi. Tunapoingia nyumbani kwa watu, sisi ni wageni wao, tutende kama inavyotupasa. Wakati tunapo tumia Biblia au kuongoza mazungumzo ya kiroho, kama watu wengine, ndugu au marafiki wanaingia, tusimtilie mashaka mwenyeji wetu. Turudishe Biblia mfukoni na kubadilisha mazungumzo kwa muda. Waislamu wana kawaida ya kuwaogopa Waislamu wenzao; kwa hiyo wanafurahia adabu njema kama hiyo.

VITABU VITAKATIFU lazima vitumiwe kwa heshima. Kitabu cha Kurani huwekwa wakati wote kwenye dawati iliyo juu kabisa chumbani. Mara nyingi ikiwa imefungwa ndani ya kitambaa safi. Ni kufuru kuweka kitabu kitakatifu chini. Tufuate mfano huo pia katika kushika na kuweka Biblia zetu.

UWE TAYARI KUTHIBITISHA maelezo yako wakati wote! Maoni yetu binafsi hayata thaminiwa sana. Tunapotamka hoja, haidhuru iwe ya ki-Biblia, ki-historia au inayotokana na Uislamu, tuhakikishe kwamba tunaweza kuithibitisha kwa kunukuu mstari unaohusika au maelezo ya kitabu kinachoaminika. Pengine haitawezekana kufanya hivyo papo kwa papo lakini tunaweza kuahidi

kuleta uthibitisho tutakapokutana tena. Tuweke malengo ya kuthibitisha hoja zote, pia tutazamie uthibitisho kama huo kutoka kwa rafiki zetu Waislamu, ingawa mara nyingi hawataweza kuthibitisha mengi kati ya yale wanayodai ni imani yao, hasa kama sisi tumejifunza kiasi cha kutosha kuhusu Uislamu.

UHUSIANO KATI YA WANAUME NA WANAWAKE katika jamii ya Kiislamu huwa na masharti mengi kuliko katika jamii ya Kikristo. Kumbuka, Mungu anatutaka tufuate maadili mema katika uhusiano wetu wote. Katika Uislamu kila jambo, kubwa au dogo, hutawaliwa na sheria zake, ikiwamo uhusiano wowote, hasa kati ya watu wa jinsia tofauti. Kwa hiyo inashauriwa kwamba kusiwe na mawasiliano yoyote hata ya kiroho kati ya mwanaume na mwanamke, bila ya kuwapo watu wengine. Katika nchi nyingi za Kiislamu wanawake hawaruhusiwi kutokea hadharani bila ya kujifunika shela (kufunika uso). Jambo hilo linahusu desturi za mavazi pia.



MAVAZI. Waislamu hudhania kuwa nguo zetu za mitindo ya magharibi, hasa za wanawake, kuwa za kihuni, kama si za umalaya. Maoni hayo pia yanasababishwa na tofauti zetu kuhusu maadili na adabu njema za ndani na nje. Hata hivyo, inapasa mwanamke anayetaka kuwashuhudia Waislamu, avae nguo zinazokubaliwa kuwa ni zenye adabu katika utamaduni wa Kiislamu, kwa mfano, kuvaa kiremba wakati wa kuwatembelea nyumbani kwao. Ni dhahiri mavazi yanayofikiriwa kuwa yanastahili yanatofautiana sana katika nchi mbali mbali na matumizi yake (kwa mfano katika maeneo ya chuo, kazini au nyumbani), na kujilundikia nguo mwilini, nako pia hakusaidii kwamba ndio kuvaa vizuri.

ADABU hutofautiana sana katika tamaduni mbali mbali. Katika utamaduni wa Kiislamu, mkono wa kulia hutumiwa kwa "matendo safi" kama kula chakula. Mkono wa kushoto hutumiwa kwa "matendo machafu." Ni muhimu tusiwakwaze wenyeji wetu katika hilo. Katika tamaduni nyingine si adabu njema kutekenya miguu. Mbwa kwa Waislamu ni mnyama mchafu na haifai kumgusa. Shahidi mwenye busara, anaweza labda kuuliza uliza ni adabu gani zinazoonekana kuwa hazifai.

UKARIMU ni sehemu muhimu sana ya utamaduni wa Mashariki. Kukataa ukarimu wa Mwislamu kunaweza kumkwaza sana. Kwa upande mwingine,



tuelewe kwamba Waislamu wanasita kukubali ukarimu wetu. Wana sababu ya kufanya hivyo. Wanaogopa kulishwa *"haraam"*.(kitu kisicho safi ki-dini au kilichokatazwa) Waislamu wanatakiwa kuwa waangalifu kula vyakula vilivyo *"halali"* tu. Katika nchi zilizostaarabika, vyakula vyote madukani huwekwa maneno yaliyoandikwa "halali" kuonyesha usafi wake ki-dini.
Lakini, kama sheria, inayohusika zaidi ni nyama ndiyo ambayo inahitajika kuwa "safi", ni lazima iwe imetoka kwa mnyama aliye "safi"; Mwislamu haruhusiwi kula nyama ya nguruwe. Nyama ya mnyama anayokula Mwislamu ni lazima awe amechinjwa, na mchinjaji awe amesema dua maalum wakati wa kukata shingo yake kwa mujibu wa taratibu za Kiislamu. Unapokaribisha wageni Waislamu, litakuwa ni jambo la kustahika kuandaa tu chakula halali, na wageni waalikwa wafahamishwe hilo wazi wazi.

## *Muhtasari*

- Waislamu wana njia tofauti za kujiheshimu. Jiepushe kumkwaza rafiki yako kutokana na mavazi na tabia zako. Tumia busara yako. Pia umwombe akueleze wazi kama umefanya jambo lisilokubalika kwake.
- Uwe mnyenyekevu na upende kusikiliza na kujifunza. Yako mambo mengi ya kujifunza kuhusu Waislamu na imani yao kutoka kwao wenyewe.
- Wathamini sana marafiki zako Waislamu. Heshima ya pande mbili, licha ya tofauti zenu, inasaidia sana.
- Uwe mkarimu. Ufahamu kwamba Waislamu ni lazima watii sheria ya 'halali', yaani, hawaruhusiwi kula kila aina ya chakula (hasa nyama) na wanaweza kuogopa kula nyumbani kwako. Uzungumze nao wazi kuhusu jambo hilo na kutafuta njia itakayo kubalika kwao.
- Jaribu kueleza zaidi 'mambo yalivyo' kwao kuliko 'mambo yasiyo'.

Usianzishe wala kukubali kuingizwa katika mjadala wa maneno yenye lengo la kumnyamazisha kabisa mmoja wenu! Ufafanue Injili kwa upendo na uelewano. Hakikisha kwamba umeeleweka kwa ukamilifu. Eleza maana ya mawazo na maneno yote ya dini na uulize maswali yanayoweza kuonyesha kama kweli mwenzako ameelewa vizuri.

- Usimridhishe kupita kiasi. Inatupasa mara na mara, kumtia moyo Mwislamu kuonja Ukweli.
- Usikubali kusukumwa na mawazo yake. Waislamu mara nyingi wanataka kutuweka katika nafasi ya kujihami. Wanabisha juu ya kila hoja. Tunahitaji kubuni njia nzuri zaidi ya kuwasiliana nao. Tuongoze majadiliano sisi wenyewe.
- Usianzishe majadiliano kwa nia ya kuadhiri Uislamu, Muhammad, Kurani wala Allah! Hayo yote ni ya thamani na utukufu kwa Mwislamu, nasi tukiyadharau, tunaweza kufunga milango ya mawasilano daima.

  Ingawa "inaruhusiwa" lakini jiepushe kutumia mifumo iliyokwishatayarishwa kama njia ya mkato ya kulazimisha uamuzi. Mtu yeyote asitazamiwe akate shauri pasipo kukubali kwamba Biblia inaeleza ukweli inaokataa dhambi, kwamba mwanadamu si 'mwenye dhambi' (kuna tofauti kubwa kati ya hayo mawili!); na kwamba amepotea milele kama Mungu asipomsaidia. Naye Mungu amekwisha kumwokoa katika Yesu, Mwokozi ambaye aliteswa akafa kwa ajili yetu ili atulete kwa Mungu tukiwa tumetakaswa.
- Kwa kawaida tusijaribu kueleza Injili nzima katika muda mfupi. Mwislamu anahitaji kuelezwa kwa ukamilifu, mawazo na maneno ya dini lazima yafafanuliwe. Pia inatubidi Mwislamu afikirie kwa upya mambo mengi muhimu. Hali hii inafanya "uinjilisti" wa kawaida kuwa njia isiyo wafaa Waislamu! (Ingawa pengine mtu 'atakata shauri' mara nyingi, uamuzi wake hautadumu).
- Ukumbuke wakati wote, kwamba hayo ni mapambano ya kiroho kati ya uhai na mauti, nuru na giza, Mungu na Shetani. Hoja zetu, hata zikiwa za ki-akili sana haziwezi kumhakikishia Mwislamu kwamba anamhitaji Mwokozi, bali ni Roho Mtakatifu tu atakayemhakikishia. Kwa hiyo, silaha yako kuu iwe ni maombi, wala si akili yako, au utaalam wako wa mawasiliano.

# 12. Utendaji

## *12.1 Tutawezaje kuwafikia Waislamu?*

Tukiuliza kwa dhati swali hili mbele za Mungu, na kuahidi kwamba tutamtii na kuwa waaminifu kwa Utume Mkuu kuhusu ulimwengu wa Waislamu, jibu kwa swali lako limepatikana.

Baada ya muda mfupi tu utagundua kwamba unafanya kazi katika sehemu ngumu kabisa ya 'bustani' ya Mungu. Lakini utakuwa na uhakika wa msaada wake, na utaweza kumwomba vipawa unavyohitaji kwa ajili ya kufanya vema kazi Yake. Tutawezaje kuwafikia Waislamu? Kwa kuwaendea pale walipo! Tumekwisha kuona hakuna sababu ya kutosha katika kujaribu kuwakaribisha Waislamu kwenye makanisa yetu. Kwanza, si rahisi kuwa watakubali kuja. Pili, hata kama watakuja, hawataelewa tunafanya nini wala hata tunaongea kuhusu mambo gani. Lakini inatupasa tuende kwao kwa sababu Bwana wetu Yesu alisema: "Enendeni ulimwenguni ….. na siyo "ngojeeni hadi watu wa ulimwengu watakapo kuja kwenye makanisa yenu".

## *12.2 Tuandae Mbinu*

Unapojenga nyumba, kwanza unaanza kuchora ramani. Unahesabu vyumba vinavyohitajika, ukubwa wake, vifaa vitakavyotumika, fedha itakayotosha na kadha wa kadha. Baada ya kila kitu kufahamika, unaamua, kama utamkabidhi fundi mwashi kufanya kazi ya kujenga au utaifanya kazi hiyo wewe na marafiki zako. Kwa njia hiyo hiyo, ndivyo unavyotakiwa kuandaa mpango wa uinjilisti. Matatizo yasitukatishe tamaa bali yatuwashe moto ili tutafute majawabu bora kabisa.




**KULIKABILI TATIZO**

**Ni kazi gani inayohitaji kufanyika?**
**Je, naweza kuifanya peke yangu?**
**Je, tunahitaji maarifa na mafunzo zaidi?**
**Je, kanisa langu litatuombea na kusimama nasi?**
**Je, kazi ni kubwa mno, hata kama washarika wenzangu watasaidia?**

**KAZI ZA KUTATUA TATIZO**

**Kama sivyo, naweza kumpata nani kufanya kazi pamoja nami? Tutawezaje ili hili lifanyike? Kama haliwezekani, nifanyeje kupata msaada wa Kanisa? Je, tunaweza kushirikiana na Kanisa lipi jingine katika kazi hiyo?**



Ingawa ni vyema kuwa na mwanzo mdogo, hatunabudi kuwa na mpango wa kumaliza kazi nzima. Na, ili hilo liwezekane, hatunabudi kuhamasisha Wakristo wengine kadiri inavyowezekana. Pengine maana yake pia itakuwa hapanabudi kushirikisha makanisa au madhehebu mengine ambayo yanaamini Biblia kwa ukamilifu. Kila Mkristo anapaswa kuwaombea Waislamu!

***Uinjilisti kwa Waislamu usipopanuliwa na kuwa lengo la Wakristo kwa jumla, haitawezekana kuwafikia Waislamu wengi.***

Pengine utapenda kumkaribisha Mwalimu wa Uinjilisti kwa Waislamu ili akusaidie kuanzisha kazi hii na kukufundisha wewe na wenzako. Ujaribu kumtafuta mwalimu, au tuandikie tukusaidie! Tunaweza pia kukupatia vitabu vingine vya mafunzo.
Utahitaji maandiko mengine yaliyoandaliwa kwa ajili ya Waislamu wenyewe. Uwe mwangalifu! Usitumie vipeperushi vile vya kawaida tu. Mara nyingi havifai sana kwa Waislamu.
Uanze kwa kuwashirikisha Wakristo wakereketwa walio tayari kushirikiana nawe katika maombi na kufanya kazi pamoja nawe. Kisha mkae na kupanga pamoja, mjifunze pamoja na kubuni mbinu zenu za kazi.

## *12. 3 Iko Mifano na Njia Nyingi*

❒ ***Kuwatembelea watu nyumba kwa nyumba.*** Haya hayanabudi kupangwa ili yaweze kufanyika kwa mfululizo kama utaratibu wa kawaida wa kila siku.
❒ ***Kujenga uhusiano:*** kwa ajili ya kuwashirikisha wengine imani yenu – rafiki, jirani, watu wanaofanya kazi pamoja nao, na kadhalika. Mtahitaji kuwa wengi kufanikisha mbinu hiyo (tuandikie tukupatie kitabu chetu maalum).
❒ ***Program za maandiko:*** Ikiwa Waislamu wa eneo lako wanaweza kusoma, tafuta maandiko yafaayo; pengine hata kuyaandaa mwenyewe. Unaweza kuyagawa nyumbani kwao, na/au kuwa na Maktaba ya kuanzimisha vitabu. Lakini muhimu: usisahau kuwa na mpango wa ufuatiliaji!
❒ Unaweza kubuni hata njia nzuri zaidi. Uwakaribishe Waislamu kwa ***Somo la Biblia nyumbani kwako*** au kwao. Kozi yetu *"Al-Kitab"* ni zana bora kabisa kwa ajili ya somo hilo. Upendo kila mara hubuni njia.
Uwe na maono makuu! Usisahau kamwe: "Pasipo Kristo hakuna Mwislamu aliye na matumaini ya uzima wa milele! Wewe unaweza kubadilisha hali yake hiyo. Usimsubiri mtu mwingine aanzishe kazi, isipokuwa ushirikiane na wote waliotayari kuifanya.
Kumbuka: Sisi tupo hapa ili kuwa *WASAIDIZI WAKO KATIKA KAZI YAKO YA UINJILISTI KWA WAISLAMU*

**Kumbuka ile orodha ndefu ya utajiri mkubwa wa vyanzo vilivyotajwa katika nyongeza**

### *12. 4 Unangoja Nini Sasa? Nyoosha Mikono!*

Je, mtu kama mimi, nikimbie? Aliuliza Nehemia alipokuwa katika hali ngumu (Nehemia 6:11) Hakika, hakukimbia! Na, wewe je? Ukimbie matazamio ya Mungu? La hasha!

Kama ni mapenzi ya Mungu, kwamba watu wote watubu, na hapana mtu yeyote anayetakiwa apotee (2Petro 3:9), kwamba Mungu hutaka watu wote waokolewe na kupata kujua yaliyo kweli (1Timotheo 2:4), na kwamba WEWE uwe shahidi Wake (Matedo 1:8), uenende ukawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi (Mathayo 16:15); basi utafanya nini?

Tukumbuke nafasi nyingi wanazoweza kuzipata watu wengine kusikia Injili – na uzilinganishe na nafasi chache sana wanazopata Waislamu. Kwa nini wewe sasa, usiseme kama Isaya alivyosema:

***"Mimi hapa, nitume mimi!" (Isaya 6:8)***

> ➔ ***Vyema sana. Kuna maswali machache tu ambayo yatakusaidia kutumia kwa vitendo yale uliyojifunza katika maisha yako na katika huduma yako.***
> ***Hakikisha unayafanyia kazi, mshirikishe rafiki au tuandikie sisi na kutuambia fikra zako***
> ***Mungu akubariki wewe na akufanye baraka ikuzunguke***

## Sehemu ya Nyongeza

1. Vielelezo kwa ajili ya ushuhuda wako kwa Waislamu.

2. Mifano kutoka Biblia.

3. Uhusiano wa Abraham na Injili.

4. Maswali kwa ajili ya matafakari zaidi.

5. Ushirika wa mabinti wa Abraham.

6. Vitabu vinavyopendekezwa kusomwa.

7. Masomo ya juu kwa ajili ya Uinjilisti kwa Waislamu.

8. Vyanzio – kama unavyohitaji.

## ❶ Vielelezo kwa Ajili ya Ushuhuda Wako

***Kuna haja gani ya kutumia vielelezo kama kueleza ukweli kunatosha ?***

Siku moja, zamani kidogo, Ukweli ambaye hakuvaa nguo alikuwa anatembea mitaani katika mji alikozaliwa. Lakini kila alikopita alikataliwa na kila mtu. Hakuna hata mtu mmoja aliyemkaribisha nyumbani mwake. Kila aliyemwona anakuja, alitoroka. Ukweli alifadhaika na kuhuzunika sana moyoni alipokutana kwa bahati na Methali.

Methali alikuwa amevalia nguo nadhifu zenye rangi nzuri ya kumeremeta, akitembea kwa madaha kutoka hapa kwenda pale. Alipoona uso wa kujiinamia wa rafiki yake alimuuliza Ukweli: "Hebu niambie, sahiba yangu, ni nini leo kinakufanya kuwa na huzuni hivyo? Ukweli alijibu kwa uchungu na masikitiko: "Ah, dada mpendwa, mambo ni mabaya sana. Nimeshayaona maisha katika hali yake yote, yakiwa juu na chini, hata sasa ni mzee, tena mzee sana, lakini yaonyesha hakuna anayenijali. Vibaya zaidi, hakuna hata ndugu mmoja anayetaka nishirikiane naye. Wote wananikwepa."

Wakati wote Methali alikuwa anasikiliza kwa makini, akasema: "Siyo kwamba watu wanakukimbia kwa sababu wewe ni ajuza. Mimi nina ujana gani kuliko wewe ! Lakini kadiri umri wangu unavyoongezeka, ndivyo jinsi watu wanavyozidi kunipenda. Nitakwambia siri ya kupendwa kwangu: Kila mmoja anapenda kuona mtu aliyevaa 'nguo kidogo' zilizo rembwa vizuri. Hebu nikuazimishe baadhi ya nguo zangu chache, zile nzuri na zenye thamani. Hapo ndipo utakapotambua, kwa nini wale waliokukataa hapo kabla, sasa watakukaribisha nyumbani mwao na kuomba ushirikianne nao kufanya maombezi."

Ukweli alikubali na kupokea ushauri huo wa rafiki yake Methali. Aliazima nguo za rafiki yake, akazivaa. Tangu wakati ule na kuendelea, Ukweli na Methali wakawa marafiki wa kutembea mkono kwa mkono, na kila mmoja alipenda kuwasikiliza.

*(Chanzo: Yiddish Folktales, Pantheon Books, New York).*

C.H. Spurgeon alidokeza:
**"Mahubiri yasiyo na kielelezo**
**ni kama chumba kisicho na dirisha."**

## SHAMUEL, MWANA WA MFALME WA MILIMA YA CAUCASIA - Mfano wa Kihistoria

Shamuel alikuwa Mfalme wa nchi iitwayo Caucasia kiasi cha karne mbili zilizopita. Watu wake walikuwa wakipigana vita na Waturuki kila wakati. Siku moja, yeye na jeshi lake walilizingira jiji fulani la Uturuki. Kama kawaida yao, mama yake alikuwa pamoja nao vitani. Usiku mmoja alipanga kufanya shambulio la kushitukiza, lakini kumbe maadui walikuwa wamejiandaa. Mipango yake ilikuwa imesalitiwa.

Kwa hasira, Shamuel alitangaza kwamba msaliti akipatikana, ataadhibiwa kwa kupigwa viboko mia moja. Shambulio jingine la kushitukiza likapangwa, safari hii, kwa siri kubwa. Lakini matokeo yake yalikuwa yale yale.

Lakini, safari hii, msaliti alifahamika. Alikuwa ni mama yake mwenyewe! Shamuel alijifungia ndani ya hema lake kwa siku tatu. Akiwaza, nini la kufanya. Akimwachia mama yake, watu watalalamika kwamba hakutenda haki. Akimwadhibu, wote watasema: "Huyu mtu hana huruma, hata kwa mama yake mzazi!" Hatimaye alitokea. Askari wake walikuwa wakimsubiri kwa hamu. Katika hali ya ukatili, aliwatangazia askari wake: "Tumeshindwa katika mapambano mawili kwa ajili ya uhaini. Baadhi ya askari wetu wameuawa. Hakuna kisingizio… kosa limetendeka na adhabu lazima itolewe kama nilivyoamuru – viboko mia moja. Haki na sheria lazima visimamiwe. Mama yake alitolewa mbele ya askari wote, huku anatetemeka kwa hofu. Mwenye kupiga viboko aliinua kiboko juu yake – lakini kabla hajampiga kiboko cha kwanza, Shamuel alipaza sauti akisema: "Ngoja! Huyu ni mama yangu. Mimi ni nyama yake na damu yake. Nitampokea adhabu yake!" Alivua joho lake na kusimama ndani ya mduara wa askari wote na kumwamrisha Mpigaji viboko: "Usithubutu kupiga kwa huruma kuliko ambavyo ungempiga msaliti mwenyewe. Fanya kazi yako!"

Alipigwa hadi akaanguka chini, na kupoteza fahamu. Hata hivyo, kinyume cha matazamio yote, alipona.

> *Tukio hilo, pengine kuliko lo lote jingine katika historia, linafuatana na tendo la Kristo. Yeye alikuwa Mungu katika mwili wa kibinadamu. Ilimbidi atoe hukumu ya haki, lakini katika upendo Wake kamili alijichukulia dhambi zetu; zangu, zako; na kustahimili adhabu ya Mungu pale msalabani.*

## MZAMIA-LULU – Hadithi ya ki-mila

Mpigambizi, mzee fulani aliyekuwa akiishi karibu na bahari upande wa mashariki wa Bara Hindi, aliamua kumalizIa sehemu iliyobaki ya maisha yake katika matendo ya kidini, akijiandaa kwa maisha yajayo. Wazo lake lilikuwa ni kutembea kwa magoti hadi jiji takatifu la dini ya Hindu, Varanasi, lililopo kwenye kingo za Mto Ganges.

Alikuwa na rafiki mmoja tu, Mkristo, ambaye yule mzee alimkaribisha kwa chakula cha kuagana. Tena mpiga mbizi huyo hakuwa na ndugu yeyote aliye karibu naye.Walipomaliza kula, yule mpigambizi alimweleza rafiki yake mpango wake. Yule Mkristo alijaribu kumshawishi abadili mawazo yake... “Magoti yako yatakatwa na mawe, yataoza, nawe utakufa,” alimuonya. “Hata nikifa,” mpigambizi alijibu, “kama niko njiani kwenda Varanasi kwenye mto mtakatifu, roho yangu itapata thawabu yake ya haki.”

Baadaye siku ile jioni, kabla rafiki yake hajaondoka, yule mzee alisogeza kabati lake na kukunja mkeka mdogo, akafunua tundu la siri lililojificha. Alitoa kifurushi kidogo akakifungua katika mwanga hafifu wa koroboi. Ndani yake kulikuwa na lulu kubwa na nzuri ajabu! Alisema: “Wewe ni peke yako mtu mpendwa wangu, nataka nikuzawadie lulu hii!”

“Lakini ina thamani kubwa!” yule rafiki alisema kwa mshangao. “Siwezi kupokea zawadi kubwa kama hiyo.” Machozi yalielekea kumlengalenga yule mpiga mbizi. Nilikuwa na mtoto wangu wa kiume. Alikuwa mpigambizi hodari kushinda wote katika pwani hii. Aliweza kuzama chini sana na kwa muda mrefu zaidi kuliko sisi sote. Siku moja tulikuwa tukipiga mbizi pamoja katika hali ya hewa nzuri kabisa. Mimi nilikuwa juu kwenye mashua nikipokea na kufungua kwa kisu zile chaza ambazo yeye alizitoa kwenye marijani.

“Basi, kulitokea nini! Aliona chaza kubwa sana iliyokuwa chini kabisa. Alijaribu kuitoa kwenye marijani lakini ilikuwa imebana sana. Aliendelea kujaribu kuing’oa hadi kumaliza muda ulio salama kwa kukaa chini ya maji. Hata hivyo hakuiachia. Kwangu, ilikuwa saa kadha mpaka alipoibuka kutoka majini huku damu ikitiririka kutoka mdomoni mwake. Alinifia mikononi mwangu… Nilipata lulu hii katika chaza ile. Nisingeweza kuiuza kamwe Naipenda kikomo!”

“Lakini, kweli thamani yake ni ya juu kabisa. Je, siwezi kuinunua kutoka kwako? Naomba nikupe angalau kitu kidogo. Kama pauni 100 elfu hivi! moja tu,” rafiki yake alijaribu kumbembeleza. Yule mzee alikasirika. “Yaani, unataka KUNILIPA fedha nyembamba kama pauni laki moja kwa kitu ambacho mwanangu alikifia? Hakuna mtu anayeweza kulipa thamani yake kwangu! Lakini nilitaka nikupe kama zawadi ”.

Yule Mkristo alimkumbatia rafiki yake mzee. "Kwa kweli, sikutaka kukuumiza. Lakini unajua wewe nawe unajaribu kumlipa Mungu kwa ajili ya ile iliyosababisha kifo cha Mwana Wake, yaani dhambi yako. Je, huoni kwamba unamkasirisha Mungu anapojaribu kulipia kitu chenye thamani isiyopimika?

*Ndipo yule mpigambizi alipofahamu mara moja, aliacha mpango wake wa kwenda Varanasi kwa magoti. Badala yake alipokea zawadi ya msamaha wa Mungu kwa ajili ya dhambi zake, uliotolewa bure kabisa!*

## MASHINDANO YA KUOGELEA -Hadithi ya kubuni

Je, umewahi kusikia habari ya mashindano makubwa ya kuogelea kutoka Mombasa hadi pwani ya India? Yalikuwa ya ajabu! Unaweza kubuni matokeo yake? Watu wengine walizama wakafa maji meta chache tu baada ya kufikia maji marefu. Wengine waliweza kufika kipwa cha marijani. Wachache walio mahodari sana walifaulu kuogelea kwa muda wa saa nyingi kidogo. Lakini mwishoni wote walikufa maji tu.

*Bila shaka hakuna mtu yeyote anayeweza kujaribu kuogelea mbali kiasi hicho. Lakini wengi wetu tunajaribu kufika mbinguni tukitarajia kwamba Mungu atakubali matendo yetu mema. Hakuna tumaini lo lote kwamba mwanadamu yeyote atafika mbinguni kutokana na bidii au nguvu yake mwenyewe. Tutakuwa salama pale tu ambapo tutajisalimisha kwa "chombo cha wokovu" cha Mungu na kukubali njia Yake ya wokovu.*

## KUJILIPIA CHAI - Mfano wa Matendo

Ukarimu umekuwa sifa moja ya Waislamu tangu awali hadi leo. Kwa hiyo, hata wewe utakaribishwa kwa chakula au angalau kikombe cha chai. Siku moja Mkristo fulani ambaye alikuwa amemtembelea Mwislam aliyekuwa rafiki yake wa muda mrefu, alitoa shilingi mia moja mfukoni mwake akamwambia mwenyeji wake, "Nimekunywa chai hapa kwako mara nyingi mno; leo nataka nilipe." Mwenyeji wake alishtuka, akashindwa hata kujibu kwanza. Ndipo aliposema, kwa kubabaika: "Huwezi kulipia chai!" "Kwa nini? Sitaki kuendelea kunywa bure tu. Acha leo niilipie!" Alisisitiza hilo, huku akiwa ameishika ile shilingi mia moja mkononi mwake. Kufikia hapo, yule Mwislamu alipandwa na hasira. Akajibu kwa ukali:"Sisi tumekukaribisha unywe chai kwa ukarimu wetu. Ni kama unatusukuma unapodai utulipe."

Ndipo mtumishi wake (yule Mwislamu) alipita pale, na yule Mkristo alimwita na kumpa ile shilingi mia moja. "Lo, asante sana bwana," kijana alisema, akipokea fedha bila kusita.

*Bila shaka unaweza kugundua maana ambayo yule Mkristo alikuwa nayo*

*katika kutenda vile. Alimwomba mwenyeji amsamehe kwa maudhi aliyomfanyia. Lakini alimweleza, kwamba alitaka tu kumwonyesha msimamo wetu mbele ya Mpaji wa mbinguni, ambaye pia anaweza kuchukia na kuhuzunika tunapojaribu kulipia dhambi zetu kwa matendo tunayoyaona ni mema.*

## KUKALIA KITI - Mfano wa Kutumia Chombo

Tumeutumia mfano huu mara nyingi tukisisitiza maana ya imani ya kweli. Kumwamini Mungu kwa ukweli si jamnbo la kumkubali ki-akili, bali ni kujitoa katika hali ya kutegemea kile tunachojidai kwamba tumekiamini.

Tunapotembelea nyumba ya Kiislamu na kukaribishwa ukae kwenye kiti, wakati unaofaa katika mazungumzo yenu, usimame na kushika kiti kile ulichokuwa umekikalia. Ndipo ueleze, "Nilipoingia hapa kwako, ulinikaribisha kwa ukarimu nikalie kiti hiki. Je, ungeonaje kama ningesema: "Asante" lakini hali nimeendelea kusimama? Nafikiri ungeniambia mara nyingine nikae chini, na baada ya muda ungeanza kuona kwamba niliogopa kukalia kiti hicho au kuna tatizo gani jingine. Na kweli, ningeweza kuwa na mashaka kama kiti hiki ni imara kumudu uzito wangu. Kuna viti vilivyovunjika na kuwaangusha watu walio vikalia. Lakini nilipokaa chini (na hapo urudie kukaa tena kwenye kiti), nimethibitisha kitendo kwamba ninaamini kiti hicho kinaweza kunibeba. Nina imani na kiti hicho na ndiyo sababu nimejisalimisha kwake.

Kama vile imani yangu kwa ajili ya kiti imethibitika hapo tu ambapo nimekubali kukikalia, ndivyo imani yetu kwa ajili ya Mungu inathibitika pale tu ambapo tunategemea ahadi yake ya wokovu katika Yesu Masihi. Nami ninaweza kukuhakikishia kabisa, kwamba Yeye ni thabiti na anaweza kutubeba na kutufikisha Kwake.

## RAFIKI WA MFUNGWA - Tukio la Kweli

Mke wangu alifikishwa mahakamani hivi karibuni kwa kosa la kuendesha gari kwa mwendo kinyume cha sheria. Alimwomba hakimu apunguze faini, akieleza mazingira yaliyomfanya azidishe mwendo wa kasi. Faini yake ilipunguzwa kiasi lakini bado ilimbidi alipe TShs 30,000/= hivi.

Alipoona haikupunguzwa zaidi, alitoa kitabu chake cha hundi apate kuandika kiasi hicho. Ndipo alishangaa, kuambiwa kwamba hundi yake haikubaliki, lazima alipe kwa fedha taslimu.

"Lakini, sina kiasi hicho cha fedha," alilalamika. "Huwezi kunipendelea (kunifanyia 'feva' ?)

"Haiwezekani !" alijibiwa.

“Ngoja basi, niende Benki, kuchukua fedha hizo.” Mke wangu alisema.
“Hapana, mama. Huwezi kutoka nje ya jengo hili.”
Aliambiwa: “Unaweza tu kumpigia simu mtu mmoja ambaye pengine atakubali kukulipia faini yako. Akikataa, basi utakwenda jela kwa muda wa siku tano.”
Ndipo mimi nilipokea simu kutoka kwa mke wangu, akiniomba nitafute shilingi elfu thelathini kwa haraka na kuzipeleka mahakamani, vinginevyo anikute gerezani. Bila ya shaka umekwisha kubaini kwamba nilikwenda haraka hadi mlango unaoitwa “Rafiki wa Mfungwa”. Nikamlipia mke wangu faini yake, naye hajasahau tendo hilo hadi leo.

*Mafunzo ya tukio hilo ni kwamba mwanadamu anaweza kujaribu kukubaliwa mbele ya Mungu kwa matendo yake mazuri na maisha yenye heshima. Lakini tunapovunja sheria ya Mungu hatuwezi kujilipia kwa njia ZETU, bali kwa njia ile moja tu iliyoandikwa katika Neno Lake (Matendo 4:12).*

**HABARI NJEMA AU MBAYA- Kutumia Nafasi Inayopatikana Nyumbani**

Mara nyingi tunapowatembelea watu nyumbani kwao, tunawakuta, au wanatazama televisheni au wanasikiliza habari ya jioni kwenye radio. Badala ya kupata kigugumizi na kushindwa kusema, tunasema: “Mtuwie radhi sana kwa kuwasumbua wakati wa taarifa ya habari. Je, leo kuna habari njema au mbaya inayotangazwa zaidi? Inaonekana siku hizi habari mbaya ndizo zinazotangazwa zaidi kuliko habari nzuri, au sivyo? Je, unaweza kutupatia dakika chache za kujibu dodoso letu linaloweza kutusaidia kutafakari hali hiyo?”
Wanapokubali, basi tunapata nafasi ya kutumia madodoso yaliyotayarshwa maalum.

**UFUNGUO WA UHURU - Hadithi ya Kubuni**

Marafiki watatu wa mfalme walipata matatizo katika nchi ya kigeni. Wakatupwa gerezani. Kwa masikitiko, mfalme aliamua kumtuma mwanawe kwenda kuwasaidia watoroke. Kijana huyo aliwashinda walinzi wa gereza na kuupitisha ufunguo wa mlango kwenye dirisha dogo sana la gereza hilo. Lakini wale wafungwa, badala ya kufungua mlango kwa haraka na kutoroka, walikaa chini na kuuchunguza ule ufunguo, huku wanabishana kama kweli ungeweza kufungua mlango wa lile gereza.
Ndipo walipoanza kuubadilisha ule ufunguo kwa kuvunja sehemu nyingine. Mwishoni walipokubaliana kuujaribu kwenye mlango, haukufanya kazi tena. Kwa aibu, walianza kumdhihaki mwama wa mfalme, wakisema kwamba ufunguo wenyewe usingeweza kufungua mlango ule hata pale ulipokuwa haujabadilishwa.

*Hadithi hii inafafanua ukweli kwamba watu wengi wanaosikia Ukweli wa*

*Mungu katika Injili ya Yesu Kristo, wanautumia vibaya, kuudhihaki na kuubadilisha mpaka usitambulike tena kama Ukweli. Mwishoni, badala ya kuutegemea, wanaukataa kabisa.*

## MKULIMA NA PAKA - Hadithi ya Kubuni

Hapo zamani za kale, kulikuwa na Chifu Mwislamu aliyependa sana wanyama, hasa paka wake aliyempa jina la Antari ambaye alikuwa amemfundisha kumhudumia yeye na wageni wake kwa kuwaletea chai katika sinia.

Siku moja mkulima fulani alimetembelea yule Chifu, kwa ajili ya kumtaka ushauri wake kutokana na kijana wake aliyekuwa akiishi maisha mabaya sana. Yule Chifu alimwonyesha mkulima vitendo vya uhodari wa Antari, kisha akamshauri kwamba endapo atajitahidi kumpa mwanawe elimu ya kutosha, mambo yote yatakuwa mema, kwa sababu ni elimu tu ndiyo iliyombadilisha tabia paka wake.

Yule mkulima alirudi kwake na kwa miaka kadha alihakikisha mwanawe anapata elimu iliyo bora kabisa kadiri iwezekanavyo. Mambo yote yalipo onekana kana kwamba yanakwenda vizuri, ghafla yule mkulima alitupwa katika mashaka makubwa kwa mara nyingine tena mwanawe alipoanza kurudia njia zake za awali. Kwa mara nyingine tena, yule mkulima alifunga safari kwenda kumtembelea yule Chifu, safari hii akiwa amechukua kifurushi kidogo ambacho amekitayarisha kwa njia maalum. Yule Chifu alisikiliza kwa uangalifu sana hadithi ya kusikitisha ya yule mkulima, lakini alikuwa hana maneno mengine ya faraja ya kumpa baba huyu mkulima.


Hatimaye Antari alipokuwa anawaletea chai Chifu na mkulima, yule mkulima alifungua kwa haraka kile kifurushi chake na kuachilia panya wadogo weupe watatu. Antari alibwaga chini sinia la chai na vikombe vikavunjika alipowarukia wale panya, jambo ambalo lilimlazimisha Chifu akubali kuwa kumbe tabia ya Antari ilikuwa haijabadilika hata kidogo.

Siku moja, muda mrefu baada ya kifo cha mkulima, kijana mvulana aliingia nyumbani kwa Chifu. Akajitambulisha mwenyewe, kwamba kama baba aliwahi kukwambia kuwa ana mtoto mwenye tabia mbaya, mtoto huyo ni mimi, ambaye sasa nimebadilika kabisa baada ya kusoma Neno la Mungu. Baada ya kumsikiliza kijana yule, Chifu kwa hiyari yake, aliomba apatiwe nakala moja ya Biblia; kwani alitambua ya kwamba ni Mungu peke yake ndiye mwenye uwezo wa kubadilisha tabia ya mwanadamu.

*Suala muhimu linalosimuliwa katika kisa hiki linahusu asili na tabia ya mwanadamu. Je, anaweza kubadilika asili yake ya uovu kwa elimu ya maadili akifuata kanuni za "Fanya hivi na Usifanye vile?" Je, sisi wanadamu ni dhaifu tu? Au, je, mwanadamu hana uwezo wowote wa kujibadilisha bali kutegemea kabisa msaada kutoka mahali pengine?*

**"HALALI" AU "HARAMU" - Swali la Kuhamasisha**

Muulize rafiki yako Mwislamu, angefanyaje kama angefika dukani na kukuta 'soseji' za aina nne: Aina ya kwanza 50 % nyama ya ng'ombe na 50 % nyama ya nguruwe. - Aina ya pili yenye 75 % nyama ya ng'ombe na 25 % nyama ya nguruwe. - Aina ya tatu yenye 90 % nyama ya ng'ombe na 10 % nyama ya nguruwe. - Aina ya nne yenye 100 % nyama ya ng'ombe, ila tu ngozi ya nje ni utando wa nyama ya nguruwe. Atachagua soseji ipi kati ya hizo?



*Asilimia kumi tu (10%) Nguruwe*

Mwislamu mwaminifu atajibu moja kwa moja kwmba aina zote ni 'haramu' kwake hawezi kula hata moja. Hazina tofauti kama asilimia kubwa au ndogo ni nyama ya nguruwe au hata ganda la juu tu. Hakuna aina yeyote inayokubaliwa chini ya sheria ya Kiislamu.

> *Ndipo unapoweza kumwonyesha, kwamba vivyo hivyo kwa dhambi! Hukumu ya Mungu ni ile ile kwa dhambi yoyote ile; dhambi zote zimekataliwa kabisa na Yeye. Je, kuna tofauti kati ya dhambi ya 80 %, 50 % au hata 10 % ? Sisi tnnapo wapima wenzetu tunajidai kwamba ipo tofauti, lakini Mungu anaweza kutukubali tu tukiwa 100 % takatifu, kama alivyo Yeye mwenyewe. (soma Walawi 19:2 na Mathayo 5:48).*

**WATU WAWILI WALIOKWENDA KUABUDU - Mfano wa kiBiblia (soma Luka 18:9-14).**

Wanaume wawili walikwenda kusali msikitini. Mmoja alikuwa Mwislamu mwaminifu aliyefahamu vizuri kabisa kufuata mapokeo yote ya *'salat',* Kiarabu chake, hakina kasoro hata ndogo na alikuwa hodari kweli wa kufanya vitendo vyote vya mwili vinavyotakiwa wakati wa *salat.* Ni hakika kabisa, alikuwa mzoefu sana katika kuyatii majukumu yote ya ibada kwa miaka mingi. Alitembea kifua mbele kwenda mbele katikati ya msikiti, akapiga magoti na kufuata utaratibu wote wa *salat.* Lakini alipokuwa akisali, mawazo yake yalimtorosha hadi nyumbani kwa msichana mrembo jirani yake ambaye alikuwa amemtamani kwa muda mrefu.


Yule mwanaume wa pili, alikuwa mtenda dhambi mkubwa aliyeishi maisha machafu wala hakusali kwa muda wa miaka mingi. Hata hakuweza kukumbuka jinsi ya kufanya 'salat'. Alijihisi kuwa hafai kabisa alipoingia pale msikitini. Hakupoteza muda kutawadha bali alisimama tu nyuma ya nguzo kubwa na

kunong'ona kwa lugha ya kabila lake, "Mungu unisamehe, nimeharibu maisha yangu yote, lakini ninatubu kweli. Nakuomba unisaidie nibadilike, nataka kukufuata na kukutumikia."
Je, unafikiri ni sala ipi iliyo kubaliwa na Mungu?

*Unaweza kutumia mfano huo kuonyesha kwamba ingawa sisi tunapenda kuwashawishi watu kwa matendo yetu yanayo onekana, Mungu anaangalia mioyo yetu na kutuhukumu (soma pia Mathayo 23:23-36 kwa mfano mwingine wa Yesu).*

## "MTOTO WA KUFULI" - Usemi Unaofafanuliwa

Katika lugha rasmi ya taifa la Malysia, kufuli huitwa 'kutshi', na ufunguo huitwa 'ana-kushi', ikiwa na maana ya 'mtoto-wa-kufuli'.
Bila ya shaka, watu wa Malysia sio wajinga kiasi cha kudhani kwamba 'kutshi' moja ilijuana na 'kutshi' jingine na kwa pamoja akazaliwa 'ana-kutshi' au ufunguo! Maneno hayo maana yake ni kwamba vitu hivyo vinahusiana kabisa na kuhitajiana. Huwezi kufungua kufuli pasipo ufunguo wake, wala si ufunguo mwingine. Kufuli isiyo na ufunguo haina kazi. Pengine itakubidi uvunje kufuli ili ufungue mlango, ikiwa umepoteza ufunguo wake. Ni vitu viwili vinavyopaswa kukaa na kufanya kazi pamoja.




Mfano mwingine ni katika lugha ya Kiarabu: msafiri anaitwa 'mtoto wa barabara'. Hakika hakuzaliwa na barabara ile. Usemi huo unaeleweka kabisa wala hauna utata.

*Ni kwa namna hii kwamba Wakristo wanafahamu Uana wa Yesu. Yeye ndiye 'ufunguo' unaofungua kufuli na kutuwezesha tuingie katika uhusiano wa binafsi na Mungu. Kumbuka maneno ya Yesu mwenyewe: "Mimi ndimi Njia, na Kweli, na Uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya Mimi." Yohana 14:6).*

## MJINGA MAARUFU KUPITA WOTE - Hadithi ya Kubuni

Hapo zamani kulikuwa na Mfalme aliyekuwa na Mchekeshaji wake, ambaye kwa lugha yao aliitwa 'Mjinga'. Yule Mfalme alimpenda sana Mjinga wake kwa sababu aliweza kumchekesha kila wakati. Siku moja Mfalme alimpa Mjinga zawadi ya fimbo maalum kama alama ya ubingwa wake katika fani yake: "Kwa sababu sijawahi kuwa na Mjinga kushinda wewe, nataka upokee fimbo hii," yule Mfalme alimwambia. "Ila siku yoyote utakapo kutana na Mjinga anaye kuzidi wewe, basi mpatie fimbo hii."

Miaka mingi ilipita, Mfalme na Mjinga waliendelea vyema katika ushirikano wao. Hatimaye Mfalme alishikwa na ugonjwa akawa mahututi. Kama watu wengine, yule Mjinga alikwenda kumuaga Mfalme. Alipofika kwa Mfalme, alikuwa wa kwanza kuongea. Alisema:
“Ee, Mfalme, nasikia unakwenda safari ndefu.”
Mfalme alijibu: “Ndiyo. Unaweza kusema hivyo.”
Mjinga aliendelea: “Bila shaka umefanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya safari hiyo, na haikosi unasubiriwa kwa hamu sana huko uendako.”
Mfalme alijibu: “Sivyo, Mjinga wangu. Nasikitika kusema kwamba sikufanya hivyo.”
Mjinga akamuuliza Mfalme: Kwani je, hukujua kwamba utakwenda safari hii, Mfalme wangu ?”
Mfalme alijibu: “La. Nilijua. Kila mtu anajua habari ya safari hiyo.”
Mjinga aliendelea kumsaili Mfalme: “Yaani unaniambia, kwamba ulijua utakwenda safari hiyo, lakini hukujiandaa hadi sasa?”



Mfalme alitikisa kichwa chake akionyesha kukubali.
Ndipo yule Mjinga alichukua fimbo yake na kuiweka kwenye kitanda cha Mfalme. Akamaliza mahojiano:
“Ee, Mfalme, imenipasa nikurudishie fimbo hii, kwa sababu sijawahi kukutana na mtu yeyote aliyefanya ujinga kushinda huu.”
*Mfano huu unakufanya ufikiri, au sivyo?*

## HAKIKA MALAIKA HAWEZI KUSEMA UONGO - Ukweli Usio na Ubishi

Marafiki zako Waislamu wanapokuchagiza juu ya Uana wa Bwana wetu Yesu Kristo, hebu jaribu kujibu kwa njia hii:
“Je, haikosi mnafahamu vyema, ya kwamba malaika ni watumishi waaminifu wa Mungu, au ninyi hamuamini hivyo? Hebu basi tuangalie Injili ya Luka 1:32, na tusome maneno ya malaika aliyemletea Bikira Mariamu ujumbe. Alisema kwamba: “Yesu ataitwa Mwana wa Aliye Juu.”

Sasa, tuangalie, huyo malaika ni nani? Sawa. Ni malaika Jibril au Gabriel (soma Luka 1:26). Huyu ni malaika yule yule ambaye ninyi mnamwamini, kwamba ndiye aliyeleta mafunuo ya Kurani kwa nabii wenu Muhammad. Je, mnathubutu kufikiri ya kwamba Gabriel anaweza kusema uongo? Hakika, hapana. Lakini hapa, hata Gabriel anamwita Yesu "Mwana wa Mungu", "Aliye Juu" sana. Ni kwa jinsi gani basi mnaona ni vigumu sana kuamini hata kile ambacho Gabriel alithibitisha miaka mia nyingi kabla ya hata Muhammad hajazaliwa?!"

*Rafiki aliyetushirikisha mfano huo, aliongeza kusema kwamba Waislamu wa mji wake wametokea kumheshimu kutokana na jibu hilo, na sasa kila mara wanapokutana, wanazungumza vizuri sana.*

## KISIMA KILICHOTIWA SUMU - Hadithi ya Kubuni

Mkulima tajiri siku moja alivumbua kisima katika shamba lake. Kisima hicho kilikuwa na maji mengi, nacho kilikuwa kimekaa mahali pazuri tu kando ya njia kuu ya usafirishaji. Mara moja jicho la mwenye shamba liliona uwezekano wa kuchuma fedha nyingi, kwa hivyo alikijengea vizuri kisima chake na kukiwekea bomba zuri la maji. Mambo yote yalipokamilika, mwenye kisima alifurahi sana jinsi maji ya kisima hicho yalivyo matamu. Kwa hivyo alifanya mpango wa kutengeneza bango kubwa na kuagiza liwekwe hapo kisimani. Bango linasema: "Hapa unapata uzima. Maji haya safi na ya kuburudisha hukuletea uzima. Yeyote anywaye maji kutoka kisima hiki hataona kiu tena. Yeyote apendaye, anaweza kufaidi kunywa maji haya bila malipo yoyote".

Mwaka mmoja, miaka miwili ilipita, lakini tena kisima chenyewe kilitiwa sumu na hakikuwa salama tena kunywa maji yake. Haijulikani, kama jambo hili lilisababishwa na tetemeko la ardhi au kwa sababu nyingine yoyote, hakuna anayefahamu kwa hakika. Lakini, baada ya hapo, kila aliyekunywa maji ya kisima hicho aliona cha mtema kuni, alifariki. Hakukuwa na tiba.

Ni jambo la kusikitisha kiasi gani, kwamba kisima hicho hakikufukiwa, wala lile bango la ahadi ya uhai halikuondolewa na badala yake kuwekwa tangazo la ilani kuonya watu wasinywe maji ya kisima hicho!

Tunamfikiriaje mkulima huyu?

## MWENYE NYUMBA ALIYEAMKA MWISHONI …. Hadithi ya Methali

Mkulima tajiri mkubwa, alikaa ndani ya nyumba yake yenye giza totoro! Mtu mmoja fukara mwenye tabia isiyoaminika, alipita karibu na nyumba hiyo, akaona jinsi ilivyokuwa gizani. Bila ya kutaka kupoteza nafasi hii, kwa kudhani kwamba hakukuwa na mtu yeyote ndani aliamua kuingia, na kujichukulia

chochote kilichomo. Baada ya kuingia nyumba hiyo kwa uangalifu mkubwa, aliwasha taa. Hapo hapo, alimwona mwenye nyumba ameketi kwenye kona fulani, anamtazama tu yule mgeni. Mwenye nyumba hakutoa sauti yoyote. Yule mwizi alishangaa sana mwanzoni, lakini, kwa vile mwenye nyumba hata hakujitingisha kumzuia yule mwizi asiingie ndani ya nyumba yake, ingawaje alikuwa mzima kabisa, alipata ujasiri na kuanza kuchukua chochote alichokitaka. Kwanza, alifanya hivyo kwa kuogopa-ogopa, kwa uangalifu, lakini mara alipoona hakuna haja ya kuogopa alikusanya bila kuogopa kitu. Alikusanya vitu vingi vya thamani kutoka chumbani hapo siku ile.

Jioni ya siku iliyofuata, alitokea kupitia tena karibu na nyumba hiyo, na kwa kuwa nyumba ilikuwa gizani aliamua kujaribu bahati yake kwa mara nyingine. Mara hii aliingia kwa kupitia dirishani. Alimkuta mwenye nyumba amekaa mahali pale pale alipokaa jana jioni, akiwa hana dalili yoyote kuonyesha wasiwasi wa kitu chochote. Kwa hivyo, yule mwizi aliamua kuingia chumba kingine na kuchukua kila kitu kilichokuwa ndani yake. Siku iliyofuata, mwizi alirudia kufanya vile vile, na matokeo yakawa yale yale. Jioni ya siku ya nne, mwizi aliingia kama ilivyokuwa kawaida ili kuokota hazina yake, ghafla, mwenye nyumba aliruka, na kupiga kelele kuitia ‘mwizi’ kwa sauti kubwa kama alivyoweza, na hata pia alianza kumshambulia mwizi. Mara polisi walifika. Wakamtia pingu mwizi na hatimaye wakamtupa gerezani.

Kwa nini ilimchukua yule mwenye nyumba muda mrefu wote huo kupata hekima kuchukua hatua ya kusalimisha mali yake?

Je, ni jambo la busara kudhani kwamba ni Mungu yule yule aliyesimama tu akiangalia kutoka mbali wakati ukweli wa vitabu vitano vya Musa, pamoja na Zaburi, na Agano Jipya ulipokuwa unabadilishwa kuandikwa uongo na kutiwa makosa? Lakini aliona vyema, “kuamka mara moja” wakati ulipowadia wa kulinda Kurani?

> *Ni hakika, kwamba daima Mungu amekuwa akililinda Neno lake tangu milele na milele hadi hivi sasa, ili kwamba sisi tuweze kuwa nalo mikononi mwetu, kama neno la Mungu, lenye mamlaka, ambalo halikubadilishwa. Tena ni ahadi yake, kuweka ulinzi juu ya neno Lake.*

# ❷ Methali katika Biblia

**Talanta 10:** (Luka 19:12-27)

- Thawabu yetu ni kubwa, endapo tutamuishia Mungu kupitia Yesu Kristo.

**Punje ya haradali:** (Mathayo 13:31-32).

- Punje ya haradali ni ndogo sana mwanzoni, hata ni vigumu kuonekana, lakini siku moja itaonekana ya maana na kuhesh imiwa na kila mtu: ukweli wa Yesu.

**Mtini:** (Luka 13:6-9).

- Mtunza bustani anauombea mtini muda wa mwaka mmoja zai di apate kuutunza. Muda wa kuomba msamaha una ukomo wake.

**Ngano na Magugu:** (Mathayo 13:24-30).

- Wema na wabaya wanaweza kuishi pamoja, lakini kila moja hatimaye atapata hukumu anayostahili.

**Mkulima anayepanda mbegu kwa kuzitawanya:** (Mathayo 13:3-9).

- Sikiliza kwa uangalifu usifanye makosa katika utekelezaji.

**Mzabibu usiozaa:** (Isaya 5:1-7)

- Matokeo ya maisha yasiyo na matunda na ubadhirifu yanatisha mno.

**Hadithi ya Yotham:** (Waamuzi 9:7-20). Siku ambapo miti ilitoka kwenda ku utia mafuta mti mmoja uwe mfalme wao.

- Uchaguzi wa kiongozi mbaya unaleta madhara kwa taifa zima.

**Vibarua katika bustani ya Mizabibu:** (Mathayo 2:33-42).

- Si manabii tu waliokataliwa, hata Mwana wa Mungu alikuja, naye akauawa.

**Kondoo wa maskini:** (2Samuel 12:1-9).

- Utekelezaji wa huruma na haki, na kukiri makosa.

**Ngamia na Tundu la Sindano:** (Mathayo 19:24).

- Ni vigumu kwa matajiri kuurithi Ufalme wa Mungu.

**Mlango mwembamba:** (Mathayo 7:13-14).

- Usiige maisha ya watu wengine. Chagua mwenyewe maisha unayomudu.

**Hazina iliyofichika:** (Mathayo 13:44-46).

- Hakuna kafara kubwa ihitajiwayo kwa ajili ya kupata uzima wa milele.

**Kondoo aliyepotea, shilingi iliyopotea, Mwana mpotevu:** (Luka 15).

- Kuna shangwe mbinguni, kwa mwenye dhambi mmoja atu buye na kumrudia Mungu.

**Wana wawili:** (Mathayo 21:28-31).

- "Ada ya mja kunena … muungwana ni kitendo" Fikiri kabla ya kutamka, timiza ahadi zako.

**Mfarisayo na Mtoza Ushuru:** (Luka 18:9-14).

- Mungu hatazami matendo ya nje ya dini. Mungu hutazama mi oyo yetu.

**Mwaliko kuhudhuria Karamu ya arusi:** (Mathayo 22:2-14).

- Kukataa ukweli kuna matokeo ya kusikitisha.Tii sheria za Mungu, kama umekubali mwaliko wake.
  Mungu peke yake, ndiye mwenye kuweka amri tunazotakiwa sisi tuzitii.

**Wanawali Kumi:** (Mathayo 25:1-13).

- Jiandae kwa ujio wa Kristo, madhali inawezekana. Jaza maisha yako na mafuta ya Mungu, kabla hujachelewa sana.

# ❸ Uhusiano wa Abrahamu na Injili

***Umuhimu wa Mada hii***

"Je, unamwamini Mungu wa Abaham" ni swali zito nililoulizwa siku fulani nilipotembelea nyumbani kwa Mwislamu hivi karibuni. Hapakuwa na sababu ya kupata kigugumizi katika kulijibu swali hili. "Naam! namwamini Mungu wa Abraham, Isaka na Yakobo; na vile vile, naamini ya kwamba Yeye ni Mungu wa wahai na siye Mungu wa wafu." Kwa kweli, Waislamu wanamthamini sana Abraham. (Angalia katika Kurani p.57)

***Kuanzisha mazungumzo kuhusu Abraham***

Ni kwa nini Waislamu, Wayahudi na Wakristo, wote wanamheshimu sana Abraham? Abraham alikuwa na sifa gani zilizokuwa maalum? Je, ni kutokana na matendo yake? Au ni msimamo wake na imani yake vilivyo muhimu zaidi?

> *Tumia kielelezo;* Ikiwa mtoto atachota fedha yote iliyokuwamo ndani ya kisanduku cha akiba kununua zawadi maalum kwa ajili ya mama na baba yake, ni kipi kilicho na maana zaidi: ni kiasi cha fedha mtoto alizotumia kwa ajili ya kununulia zawadi au ni hisia ya mapenzi, au uhusiano maalum, ulioonyeshwa kwa zawadi iliyonunuliwa?

**Kumwongoza Msikilizaji afahamu Injili**

(*Lengo:* tunapoanza kwa kutoa hoja mbali mbali za ukweli wa kawaida kwa wote, Waislamu na Wakristo, lengo letu ni kumwongoza msikilizaji wetu afahamu kwa undani umuhimu wa Abraham kwetu sisi hata leo).

**1. Jina alilopewa Abraham: Rafiki wa Mungu (Kiarabu: "Khalilullah").**

Biblia: 2 Nyakati 20:7; Isaya 41:8; Yakobo 2:23.

Kurani: Sura 4:125 (Tafasiri ya Al-Farsy ya Kiswahili = "Kipenzi chake").

*Uliza:* Kwa nini Abrahamu aliitwa Rafiki wa Mungu? Jina hilo linatufahamisha nini juu ya uhusiano wa Mungu na Abrahamu?

> *Jina hilo linatufahamisha mengi kuhusu Abraham wa Mungu*
> *na pia ni kuhusu Abraham mwenyewe!*

*Sisitiza:* Mungu anaweza kutegemewa. Anatimiza ahadi zake. Hana kigeugeu. Pia anapenda kuwashirikisha watumishi wake mipango Yake. (Soma Amos 3:7). Ni Mungu wa ajabu!

**2. Abraham ni Baba halisi wa wote ambao ni watu wa Mungu**
Yeye alipokea ahadi maalum ya Mungu iliyomfanya awe baraka kwa watu wote wa dunia: Mwanzo 12:3; 15:1-6; 17:5,19. Wayahudi walimtambua kama baba yao: Luka 3:8; Yohana 8:33,39 (Kama muda unatosha, endelea na hoja nzima hadi mstari wa 58!).
Kila Mkristo wa kweli ana haki ya kujitambua kuwa ni mtoto wa Abrahamu: Warumi 4:16; 9:8; Wagalatia 3:7-8.

*Angalizo:* Mistari ile ya Yohana 8:56 na Wagalatia 3:8 ni maelezo ya ajabu sana. Nani angeweza kubuni kwamba Abrahamu aliona siku ya Yesu na yeye ndiye aliyetangulia kupewa Injili kabla haijatokea! Hakikisha unatamka haya wazi wazi. Kurani inamwonyesha Abraham alikuwa kiongozi wa kupigiwa mfano kwa binadamu wote. Sura 2:124 ('Nitakufanya wewe kuwa Imam kwa mataifa yote') Sura 16:120 ('mfano'); Surah 3:67 ('Abrahamu hakuwa Myahudi wala alikuwa bado hajawa Mkristo; lakini alikuwa mkweli katika imani' – unatakiwa usiusahau mstari huu, lakini ikiwezekana usiutaje katika mazungumzo yenu).

**3. Abraham alimpendeza Mungu kutokana na imani yake tu**
Waislamu wanahamasishwa waige imani ya Abraham: Sura 3:95; 2:135; 6:161. Wakristo wanakumbushwa watafakari imani yake: Wagalatia 3:6- 9.

*Tumia kielelezo:* Haikosi umepata kumwona mbwa aliyefundishwa kutii amri kama 'kaa chini', naye anakaa. Anafanya kama anavyoamrishwa. Lakini hatuwezi kufikiri kwamba mbwa ana imani kwa yule anayemwamrisha. Ni kwamba amefundishwa kutii tu. Utii ni jambo zuri, lakini sio sawa na imani.
*Imani ya Abraham ilikuwa itikio kwa uaminifu wa Mungu (1Wakorintho 10:13; 2 Wathesalonike 3:3); nayo ndiyo Mungu aliyo mhesabia haki (Mwanzo 15:6).*

**4. Ahadi ya Mtoto kwa Abrahamu**
Ahadi hiyo imetajwa katika Biblia na katika Kurani pia:
Kuran: Surah 11:71 "Na mkewe (Abraham- Bibi Sarah) nasi tulimpa habari njema za Isaka…. zingatia Isaka ndiye mwana wa ahadi, siyo Ishmael: Sura 37:112.
Biblia: Mwanzo 17:15, 16,19.

*Angalizo:* Abraham aliamini, kwamba kama Mungu ametoa ahadi, ni hakika ataitimiza Warumi 4:18-22; Waebrania 11:11; Methali 30:5.

**5. Amri ya Mungu kwa Abraham amtoe mwanawe kama kafara**

Kurani: Sura 37: 102-113 hutofautiana sana na maelezo ya Biblia.

Bila shaka, Abraham alijiuliza: "Kama Mungu ni mwema na mtakatifu anawezaje kudai kafara kama hili?" Je, Anaweza kudai utii kwa Allah bila kuuliza? *Tofautisha* maelezo hayo na Mwanzo 22:1-13. Ingawa Abraham alikuwa ameshtuka na kuhuzunishwa, alimtii Mungu, kwa imani - na kugundua kwamba nia ya Mungu ilikuwa kudhihirisha utukufu wa wokovu Wake.

Kwa Abrahamu, ulikuwa mtihani wenye sehemu tatu:

i. Abraham athibitishe kwamba alimpenda Mungu.
ii. Abraham asimwonee Mungu wasiwasi.
iii. Abraham ashikamane na imani yake.

Mara nyingi Abrahamu alihoji Amri za Mungu. (linganisha Mwanzo 18:23-25), kwa hiyo angeweza kuelewa amri hii kwa njia moja kati ya nne:

i. Mungu amesahau ahadi Yake.
ii. Mungu amebadilisha Mpango wake.
iii. Mungu anataka nimtii tu bila kuuliza swali lolote.
iv. Mungu hata hivyo atatimiza ahadi yake kwa njia fulani.

Abraham alibakiwa na uamuzi huu: Kwamba Mungu angemfufua mwanawe Isaka kutoka kwa Wafu (Waebrania 11:17- l9; Linganisha na Kurani – Surah 2:260). Ndiyo imani ya Abraham.

*Angalizo:* Abraham alionyeshwa Injili yote kabla ya mtu mwingine yeyote. Mwanawe, ambaye tayari alimpenda:➔ aliyepewa kwa njia ya uzazi usio wa kawaida ➔ atolewe kama dhabihu kwa ajili ya dhambi ➔ afufuliwe ➔ awe baraka kwa wengine.

Kwa jinsi hiyo Isaka anakuwa lengo la somo la kazi ya upatanisho wa Mwana wa Mungu. (Hadi hapo ungeweza kupitia ukweli mkuu wa maudhui haya kwa mara nyingine tena au unaweza kuendelea kueleza umuhimu wake).

**Maswali ya kujikumbusha**

1. Mungu amefanya nini kuonyesha upendo Wake kwako?
2. Je, Mungu amewahi kuwatendea wanadamu lolote linalofikia tendo la upendo la Abraham alipokuwa tayari kumtolea Mungu mwana wake?
3. Ikiwa njia pekee ya mwanadamu kuthibitisha kwamba anampenda Mungu ilikuwa ni kuhiyari kumtolea mwana wake, je, ni kwa njia gani Mungu anaweza kuonyesha upendo wake mkuu kwetu sisi?

*Haiwezekani kabisa kufikiri kwamba Mungu angemdai mwanadamu tendo kuu kuliko lile ambalo Yeye yuko tayari kumtendea.*

## ABRAHAM KATIKA KURANI

| | | |
|---|---|---|
| 2: | 124 | - Abrahamu alitimiza amri ya Mungu |
| | 125ff | - Abrahamu na Ka'aba (Sura 3:96/7) |
| | 130/5 | - Kufuata dini ya Abraham |
| | 258 | - Abraham anahojiana na watu wasioamini |
| | 260 | - Abraham anaamini kwamba Mungu anawapa ndege waliokufa maisha mapya |
| 3: | 67 | - Hakuwa Myahudi wala Mkisto |
| | 95 | - Hakuwa mpagani |
| 6. | 74 | - Anapinga ibada za sanamu (Sura 19:41-50) |
| | 75 – 79 | -Anakataa kuabudu viumbe vya mbinguni |
| | 80 – 83 | -Anawahubiria watu wake |
| 9: | 113 – 4 | - Anamwombea baba yake (Sura 26:86) |
| 11: | 69 – 73 | - Anawatetea watu wa Lutu |
| 14: | 35-41 | - Sala yake (Sura 26:83- 87) |
| 16: | 120 – 123 | - Abraham ni Mfano |
| 21: | 51 – 71 | -Anabishana na watu wake dhidi ya sanamu Sura 26:70-82; 29:16-18; 37:83-98 |
| 21: | 69 | - Yuko salama ndani ya moto |
| 37: | 99-111 | - Anamtoa mtoto wake kuwa dhabihu |
| 53: | 37 | - Kitabu cha Abraham (Sura 87:19) |
| 60: | 4-6 | - Mfano wake katika kushughulika na watu wasioamini |

*(Mengi ya maudhui haya yame chukuliwa kutoka "Millat-a-Ibrahim: Imani ya kweli ya Abraham" kitabu kilichoandikwa na John Gilchrist).*

# ❹ Maswali: Kwa ajili ya kujifunza na Kutafakari

***Sura ya 1 na 2***

1. Kalenda ya Kiislamu ilianza lini?
   a) Muhammad alipozaliwa
   b) Muhammad alipopokea mafunuo ya kwanza
   c) Muhammad alipokimbilia Medina
2. Wakristo na Waislamu wanakubaliana kuhusu mambo kadha wanayoamini, lakini hawakubaliani kabisa kuhusu mengine. Taja mifano mbali mbali na kueleza jinsi yanavyofanya kazi ya kuwashuhudia Waislamu kuwa ngumu zaidi.
3. Katika nchi ya Arabia wakati wa dini za asili (za upagani) kabla ya Muhammad, watu walitumia uganga na ushirikina kwa wingi. Unaonaje uhusiano wa mambo hayo na imani ya Waislamu wa sasa?
4. Je, “Aya za Shetani” ni nini? Je, bado zipo katika Kurani?
5. Eleza habari za mabadiliko katika maisha ya Muhammad baada ya kifo cha mke wake wa kwanza, *Khadija*. Tukio hilo liligusa maisha yake katika njia gani?
6. Eleza maana ya *“Dhar-ul-Islam” na “Dhar-ul-Harb”*. Je, Waislamu wanaelezaje maana ya “Vita Vitakatifu” siku hizi?
7. Kwa nini ni muhimu sana kutofautisha kati ya utaratibu wa Uislamu na wafuasi wake, wanaume na wanawake walio Waislamu?
8. Fikiria tena imani na desturi za Waislamu. Eleza matokeo ya kila moja katika maisha ya jirani na rafiki zako Waislamu.
9. Je, unajua mambo gani kuhusu madhehebu mbalimbali ya Kiislamu? Wapo wafuasi wa madhehebu yapi katika eneo lako? Unafahamu mambo gani kuhusu watu hao? (Jibu la swali hili halipo katika kitabu hiki.)
10. Je, Uislamu ulieneaje baada ya kifo cha Muhammad? Je, ulifikia nchi yako au kabila lako kwa njia gani?

***Sura ya 3 na 4***

1. Linganisha Kurani na Biblia kuhusu yafuatayo:

| | Kurani | Biblia |
|---|---|---|
| a) Jumla ya Vitabu | --------- | ------- |
| b) Jumla ya Sura | --------- | ------- |
| c) Waandishi wangapi | --------- | ------- |
| d) Miaka mingapi iliyotumika kuandika | --------- | ------- |
| e) Utaratibu wa kupanga vitabu vyake | --------- | ------- |

2. Eleza yale unayoyafahamu kuhusu vyanzo vya Kurani.
3. Eleza maana ya "Sheria ya Kutangua". Kwa nini sheria hiyo inaleta matatizo katika kufahamu Kurani?
4. Ungemjibule Mwislamu anayekwambia kwamba Kurani haijabadilishwa kabisa tangu wakati wa Muhammad.
5. Kwa nini Waislamu wanahitaji vitabu vya "Hadith" pamoja na Kurani?
6. Taja majina ya watu wawili maarufu waliokusanya Hadithi. Je, watu hawa waliishi wakati gani?
7. Watu hao waliokusanya mapokeo hayo ya Hadith walitumia kanuni gani katika kukubali mengine na kukataa mengine?
8. Ni mambo gani yaliyomo katika Hadith hizo, na yanagusa maisha ya Mwislamu katika nini?

***Sura ya 5 na 6***

1. Linganisha kwa kifupi wazo la Kiislamu la "tawhid" na mafundisho ya Biblia kuhusu umoja wa Mungu.
2. Je, Waislamu wanawafahamu na kuwatambua manabii wote wa Biblia? Unaona tofauti gani kati ya kufahamu kwao na kwetu?
3. Je, umegundua nini katika kujifunza mawazo ya Kiislamu kuhusu "Kuchaguliwa" inavyo tofautiana na imani ya ki-Biblia kuhusu jambo hilo?
4. Je, Uislamu hufundisha nini kuhusu kuongoka? Kwa nini Wakristo wanaamini kwamba upo uwezekano wa maisha ya mtu kubadilishwa kabisa?
5. Eleza tofauti kati ya "kutenda dhambi" na "hali ya kuwa mwenye dhambi". Je, dhambi kuu kabisa tunayoweza kumtendea Mungu ni ipi?
6. Katika Uislamu maana ya "shirk" ni nini?
7. Unaweza kujifunza nini kutokana na mafundisho ya Uislamu kuhusu uhai na mauti?
8. Kwa nini ni muhimu sana kuwaelezee Waislamu kwa uwazi kabisa kuwa njia ya wokovu ni moja tu?

***Sura ya 7***

1. Waislamu wanaamini nini kuhusu Biblia?
2. Je, umewahi kuwahubiria Waislamu au kuwafikisha kwenye mkutano wa Kanisa? Kama ndiyo, ulionaje matokeo yake?
3. Je ungemhakikishiaje Mwislamu imani yako, kwamba Biblia inaaminika kabisa?
4. Waislamu wanaelewaje mafundisho ya Biblia kuhusu Utatu wa Mungu?
5. Umepata habari gani kuhusu "Injili ya Barnaba"?
6. Ungemwonyeshaje Mwislamu kwambaYesu ni zaidi ya Nabii?
7. Ungetumia mistari gani ya Agano la Kale kumthibitishia Mwislamu kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa?
8. Biblia hueleza "Kikwazo cha Msalaba". Maana yake ni nini?
9. Waislamu wanakataa imani ya upatanisho kwa sababu zipi?

***Sura ya 8***

1. Taja mambo matano au zaidi katika Injili yaliyothibitika.
2. Tunasoma "Mungu mwenyewe amekuwa Mwokozi wetu". Ungefafanuaje maana ya sentensi hiyo?
3. Soma kwa makini Injili nzima ya Mathayo, ukiweka alama kwa kila mstari unaoeleza kutimizwa kwa unabii fulani wa Agano la Kale. Orodhesha mistari hiyo kwenye karatasi, ukaibandike ndani ya jalada la Biblia yako, uweze kuishirikisha kwa wengine.
4. Ni mambo yapi matano yanayohitaji kutiliwa mkazo tunapowaeleza Waislamu Injili?
5. Eleza masharti yaliyo katika Injili kwa watu wanaofikiria kumfuata Kristo. Hakikisha unayataja kabla mtu unayezungumza naye hajakata shauri kufanya hivyo.
6. Je, unaweza kujifunza mambo gani katika 2 Wakorintho 4:2 kwa ajili ya kuwashuhudia Waislamu?

***Sura ya 9 na 10***

1. Je, tunawezaje kuwa watu wenye kushuhudia katika uweza wa Mungu?
2. Je, una uzoefu wowote wa "mashindano ya nguvu" katika kazi yako kama Mwinjilisti ambayo ungependa kutushirikisha?
3. Eleza uwiano kati ya mambo tunayopaswa kufanya sisi, na mambo ambayo Mungu peke yake anaweza kufanya, katika kuwasilisha Injili kwa ufanisi.
4. Eleza mafunzo muhimu ya kukumbuka unapofikiria "Vita vya Kiroho".

5. Kuna uhusiano gani kati ya ukweli na upendo?
6. Una mipango gani kwa ajili ya “kugusa maisha ya watu wengine’ hasa Waislamu?
7. Tumia maudhui ya Injili ya “Abraham, Rafiki wa Mungu” ukiwa na Mwislamu, kisha utoe ripoti ya uzoefu wako.
8. Linganisha Sikukuu mojawapo ya Kiislamu na Sikukuu ya Kikristo.Umeona zinatofautiana vipi?
9. Hebu fanya utafiti juu ya hofu gani zinamuathiri rafiki yako Mwislamu. Je wangeweza kuzishinda hofu hizo kwa njia gani katika maisha yao?
10. Linganisha “kanisa” na “umma” Je, sisi Wakristo kuna kipi tunachoweza kukionyesha ambacho Waislamu hawanacho?

***Sura ya 11 na 12***

1. Utatumia njia gani za kujitayarisha ili uweze kuwashuhudia Waislamu?
2. Utamjibuje Mwislamu, ambaye atakuuliza: “Mimi namwamini Yesu, lakini kwa nini wewe humwamini Muhammad?
3. Je, ungependa kuchukua Kurani wakati unapotembelea nyumba ya Mwislamu kwa mara ya kwanza? Toa sababu kuthitisha jibu lako.
4. Je, ni vyema kwa Mkristo kuhojiana kuhusu masuala ya dini? Eleza.
5. Mtu fulani alisema: “Ni vyema kuwaongoa Waislamu ‘hatua kwa hatua’. Je, unakubaliana na kauli hiyo?
6. Tupe fikra zako, kwa uchache, juu ya jinsi ya kuanzisha mazungumzo ya masuala ya kiroho na Mwislamu.
7. Rafiki Mkristo anakuuliza hivi: “Wewe una fikra gani juu ya Uislamu? Utamjibuje rariki yako juu ya swali kama hili?
8. Umepata furaha kubwa hivi punde ya kufanya sala pamoja na Mwislamu ambaye amekubali kumpokea Kristo kama Bwana katika maisha yake. Ni hatua gani zinazofuata zinastahili kuchukuliwa ili kumsaidia?
9. Eleza maana ya “haraam” na “halaal”. Kwa nini Mwislamu anayaona mambo haya kuwa ni ya maana sana, lakini sivyo ilivyo kwa Mkristo?
10. Kamilisha sentensi hii: Uinjilisti kwa Waislamu unatakiwa kuwa...”
11. Tupe fikra zako kwa ajili ya kupata mbinu juu ya kuwafikia Waislamu na Injili ya Kristo.

# ❺ Ushirika wa Mabinti wa Abrahamu

**1. MABINTI WA ABRAHAM NI NANI?**

- Mabinti wa Abraham (MWA) ni wanawake wa Kikristo ambao wana moyo wa kuwapenda wanawake wa Kiislamu wanaopenda kushikamana nao katika urafiki kwa ajili ya kuwahubiria Injili.
- Mabinti Abraham kutoka vikundi mbali mbali vya maombezi kwa ajili ya kusaidiana katika huduma ya mahubiri kwa wanawake wa Kiislamu.
- Wanawake wa Kiislamu ni wenye thamani sana machoni pa Mungu, nasi tunaamini thamani yao itazidi kuongezeka endapo watamfahamu Bwana.

**2. MALENGO NA MAKUSUDIO YA "MWA" NI YAPI?**


- Kuanzisha ufahamu miongoni mwa wanawake wa Kikristo kuhusu umaskini wa kiroho walio nao wanawake wa Kiislamu.
- Kuhamasisha wanawake wa Kikristo kuunga urafiki na angalau bibi mmoja au mabibi wawili wa Kiislamu wakati 'wanapokuwa pamoja' mahali wanapofanya kazi, katika eneo jirani na nyumbani kwao au wanapokutana nao madukani au sokoni.
- Kuandaa kwa kuwafundisha akina mama wa Kikristo jinsi ya kushirikiana Injili na wanawake wa Kiislamu kwa njia fulani, ili waweze kuelewa na kuweza kuamua kuchukua uamuzi na wenye manufaa.

**3. FAIDA YA KUWA NA MAOMBEZI NA VIKUNDI VYA MAB INTI WA ABRAHAMU NI ZIPI?**

- Ni kuthibitisha: Siko peke yangu katika 'kazi' hii.
- Inawapatia "Nyumba" (huko mbinguni) mabibi wa Kikristo wenye mawazo yanayofanana wanapokuwa peke yao, au pengine, "peke yao katika dhoruba" ya ushuhuda kwa marafiki na majirani zao wa Kiislamu.
- Ni chanzo muhimu cha sala za kutiana nguvu, unajenga urafiki na hisia ya kuwajibika kwa kila mmoja.
- Yanatoa nafasi ya mafunzo jinsi ya kupata majibu ya ki-Biblia kwa mapingamizi ya Waislamu na masuala mengine ya maisha.
- Inamfanya kila mmoja kuwajibika katika mahubiri kwa utaratibu na kuinua juu kiwango cha utendaji kwa kila mama mhusika.

*Mabinti wa Abrahamu wanakualika kuwa sehemu ya umoja wao kuhubiria wanawake katika nchi za Afrika kusini ya Sahara*

# Nyumba ya Mabinti wa Abrahamu





**Tafadhali tuwasiliane kwa habari zaidi**
*Mabinti wa Abrahamu*
P.O. Box 50770
00200 City Square, Nairobi / Kenya
**DoA@lifechallenge.de**
Mobile: 0721 - 962747

## ❻ Vitabu Vinavyopendekezwa

Kila mtu ana haja ya kuwa na rafiki anayeweza kumtegemea.
Hii haina tofauti kwa Waislamu pia. Wanatamani kuwa na mahusiano na watu wenye heshima, upendo na huruma. Je umewahi kufikiri katika matafakari ya sala zako nani angekuwa mtu huyo ambaye kwa faida yake ya milele Mungu anakuhitaji WEWE kuwa rafiki kama huyo.

Kitabu *"Contacts that Count for Eternity"* kitakupa mawazo ya utendaji juu ya jinsi ya kutumia mawasiliano yako ya kila siku kwa Waislamu ili uweze kuwavuta kumpokea Kristo.




*Angalizo:*
*Vitabu vyetu vingi vinapatikana pia katika lugha zifuatazo: Kifaransa, Kiswahili, Hausa, Kihabeshi na lugha nyingine nyingi.*
*Uliza Ofisi yetu.*

**<u>Maandiko Yanayohusu Uinjilisti</u>**

Al-Kitab (Masomo ya Biblia kwa njia ya Posta kwa Wainjilisti wa Uislamu)

Ushuhuda kwa Ukweli wa Maandiko Matakatifu.

Usafi Ndio utakatifu

Kulinganisha, Kutatanisha, Kuwaza, Kuamua.

Lengo na Kusudi.

Mwisho Usiofahamika

Mpendwa Abdallah

Acha Biblia Ijisemee Yenyewe


Ujumbe wa Nabii Isa

Msema Hadithi (vipeperushi 5).

Unafikiri Nini kuhusu Masihi?

Kwa nini Wahitaji Kufahamu Kitabu

## ❼ Vitabu vya Masomo ya Juu




**KUKABILIANA NA CHANGAMOTO YA UISLAMU**

Kukabili Changamoto za Waislamu ni kitabu kizuri chenye hoja mbali mbali zinazotolewa na Waislamu katika kujibu shuhuda za wastani za Wakristo. Wakristo wenye haja ya kutoa mahubiri ya maana kwa Waislamu, watahitaji kufahamu, siyo tu hoja kuu zinazoleta ubishani ni zipi, lakini vile vile wafahamu jinsi ya kuzipiku barabara.

Kitabu hiki kina majibu ya wazi wazi kabisa juu ya ushahidi na ukweli uliothibitishwa.


Kadhalika kitabu hiki kinaonyesha jinsi ya kupindua pingamizi za Waislamu kuwa sababu za kutoa ushuhuda wa kufaa kwa ajili ya kufafanua ukweli mkuu wa Injili.

**JIFUNZE NA KUSHUHUDIA (MUINJILISTI)**




Mkusanyiko wa majarida maarufu ya Jifunze na Kushuhudia (Muinjilisti). Ni mkusanyiko wa matoleo 20 yenye makala mbali mbali ya masuala ya Kiislamu, Maridhiano, Mawasiliano, Ulinganisho, Mahubiri sambamba na Shuhuda, Wasifu wa watu mbali mbali, Vielelezo na Mapitio ya Vitabu.

Ni imani yetu kwamba makala hizo fupi zenye tahariri safi za wazi siyo tu kuwa zitasaidia kupata elimu ya msingi kuhusu Uislamu na Waislamu, lakini pia kitakuhamasisha kutumia kivitendo uzoefu uliopata.




**KUSHIRIKIANA INJILI NA WAISLAMU**

Kushirikiana Injili na Waislamu kunakusindikiza katika safari ya kupitia Biblia, kinafunua njia ya mahubiri ya kufaa kwa Waislamu kutokana na hoja ya maeneo ya pamoja kati ya imani ya Kikristo na Kiislamu. Kinajumuisha masimulizi mbali mbali ya Agano la Kale na unabii ambao unasisitiza kazi ya wokovu ya Yesu Kristo na kuonyesha jinsi ya kutekeleza kwa vitendo mafundisho ya Agano Jipya kuhusu Yesu kuelekea lengo lile lile moja, hasa lengo kuu la neema kwa binadamu wote.

Kitabu hiki ni mwongozo wa Kibiblia wa utajiri wa Uinjilisti kwa Waislamu unaokuwezesha kutumia zana ya Bwana yenye nguvu sana ya kuwafikishia Waislamu Injili na kuwavuta wamwelekee mwokozi pekee wa ulimwengu.




**KARIBU NYUMBANI**

Kitabu cha mwongozo wa kazi ya Utume kwa Waislamu Waongofu – kitabu hiki cha mwongozo kimetungwa hasa kwa ajili ya Wachungaji, Viongozi na Washauri katika makanisa ambao wana majukumu ya kuhamasisha na kusaidia waumini waliokuwa Waislamu. Kitabu hiki kitawapa msimamo mzuri katika kazi hiyo. Watafaidika sana kutokana na uzoefu wa washauri kutoka sehemu mbali mbali za Afrika.

Kitabu hiki cha mwongozo kinatoa utangulizi mfupi wa uhakika juu ya maeneo mbali mbali ya huduma kwa waumini waliokuwa Waislamu. Mada katika kitabu hiki zinahusu maeneo muhimu katika maisha ya waumini waliokuwa Waislamu, kwa hivyo, huhitaji kuwa umekwisha kukisoma chote kabla ya kuanza kazi yenywe. Wewe anza popote kufanya kazi yako na kujaribu kuelewa maudhui yote hatua kwa hatua.

**MAPIGANO YA KUKONGA MOYO (Battle for the Hearts)**
**- Sasa DVD zake zinapatikana!**

Mfululizo wa mikanda hii imetungwa maalum kwa ajili ya kutia moyo uinjilisti kwa kuyapa uwezo makanisa ulimwenguni kote kuwahubiria Waislamu. Katika masimulizi ya matukio mbali mbali 12 yaliyotayarishwa na jopo la wataalam, jopo la vijana watendaji na waumini kadhaa waliokuwa Waislamu, tunapata uelewa wa kina wa vyanzo vya Uislamu, imani na vitendo vya Mwislamu, maisha ya Muhammad, hoja za maridhiano zinazotolewa na Waislamu na njia zinazofaa kutumiwa na Wakristo katika kushirikiana Habari Njema pamoja na majirani zao Waislamu.

Mfululizo huu maarufu ni matokeo ya ushirikiano wa miaka mitano kai ya Life Challenge na Trans World Radio. Ni kiongozi cha Mwalimu kwa viongozi wa vikundi kinachoimarisha ubora wa zana hii na kufikisha mafunzo kwenye kiwango cha juu kwa kutumia vielelezo vya ziada na kutoa mwongozo wa mafunzo kwa vitendo. Vitendeakazi hivi, ambavyo vinauzwa kwa bei nafuu ambayo ni rahisi kuimudu, kwa kweli vinapaswa kuwa zana bora na ya lazima kwa kila kanisa, taasisi ya Kikristo na Vyuo vya theologia katika kila nchi barani Afrika.

## 8 Vyanzo Vya Habari – Unavyoweza kutumia, ukipenda

***Mitandao ****

www.lifechallenge.de
www.answering-islam.org (mtandao mkubwa wenye uhusiano na vyanzo vingine vizuri vingi)
www.aboutisa.com (Mtandao wa kuwaambia Waislamu kuhusu Yesu)
www.apostatesofislam.com (sio wa Kikristo)
www.copts.net/index.asp (taarifa za kila siku za ukatili wa Kiislamu dhidi ya Wakristo barani Afrika)
URL: debate.org.uk/topics/coolcalm (Shuhuda za waliokuwa Waislamu, hupatikana pia kwa Kiarabu)
URL : injil.org (Mtandao wa kuwaambia Waislamu kuhusu Yesu)
www.itl.org.uk (KATIKA NURU – mahojiano ya chemsha bongo kati ya Wakristo na Waislamu)
www.islam-on-line.org (taarifa za mateso wanayo fanyiwa Wakristo na Waislamu)
www.islamreview.com (Kifumbua macho kwa uovu wanaofanyiwa watu weusi katika Uislamu)
www.light-of-life.com (Inachunguza Uislam kutokana na maoni ya Kikristo)
www.domini.org/lam/home.hmtl (kikundi cha wasaidizi)
URL: www.thruthnet.org/islam/souce.hmtl (SOURCE OF BOOKS, by W.St. Clair-Tisdall)
www.the-good-way.com (Uwanja mkubwa kwa Waislamu kuelewa imani ya Kikristo)
www.theKoran.com (taarifa nzuri juu ya Uislamu kutokana na mtazamo wa ki-Biblia)
www.islamexpose.com (Mahubiri ya amani na udugu)
***Angalizo: Hii haimaanishi kwamba Life Challenge Africa inakubaliana na hoja zote, fikra au hisia zinazotolewa katika mitandao hii. Tumia uamuzi wako mwenyewe. Tafadhali tuarifu juu ya mitandao mingine, kama unafahamu.***

***Semina na Masomo kwa Njia ya Posta:***

Wasiliana na ofisi yetu kwa ajili ya maelezo zaidi.
Utakubaliana nasi kwamba hakuna shida ya vyanzo ila kusubiri uvitumie. Kwa hivyo: NYOSHA MKONO!

**Hamasa Ya Milele**
S.L.P. 1601 Dodoma, Tanzania
**mail@milele.de**

**Life Challenge Africa**
Box 50770
Nairobi 00200, Kenya
e-mail: **info@lifechallenge.de**